**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Pili – Tarehe 1 Februari, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Katibu!

**NDG. THEONIST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali yetu na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na. 16

**Tatizo la Ajira kwa Vijana Nachingwea.**

**MHE. HASSAN E. MASSALA** aliuliza:-

Wilaya ya Nachingwea ina ardhi ya kutosha lakini vijana wengi bado wanakabiliwa na tatizo la ajira:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuwasaidia vijana hawa kujikwamua kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali katika kuwasaidia vijana wa Nachingwea kujikwamua kiuchumi ni pamoja na kufanya yafuatayo: Kuwashauri vijana wa Wilaya ya Nachingwea kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali na kubuni miradi mbalimbali ya uchumi katika nyanja za kilimo, ufugaji na viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao ya kilimo. Hii itasaidia kutengeneza nafasi za ajira kwa vijana na kuwakwamua vijana katika lindi ya umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba mpango huu unafanikiwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira inaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:-

(a) Kuhakikisha Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea zinatenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za vijana.

(b) Kusimamia utekelezaji wa utoaji wa mikopo kwa vijana ya 5% ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

(c) Kukopesha vikundi vya vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuchochea upatikanaji wa mitaji ya kuendeshea shughuli za kiuchumi za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii adhimu kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa yeye ni kijana na amekuwa mstari wa mbele katika masuala ya vijana kitaifa na kimataifa, basi tushirikiane kwa pamoja kuwaongoza vijana wa Wilaya ya Nachingwea katika kubuni miradi mbalimbali yenye tija ili kuwakwamua vijana wa Wilaya ya Nachingwea katika suala zima la ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kauli ya Serikali ni kuendelea kuunga mkono jitihada zitakazofanywa na vijana wa Nachingwea na nchi nzima kwa kusaidia upatikanaji wa mitaji na mikopo kupitia Mifuko ya Uwezeshaji ya Serikali na pia kwa kuwashirikisha wadau wapenda maendeleo ya vijana kuwasaidia vijana kujiinua kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Elias Masala kama una swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, lakini pia naomba nitoe pongezi kwa majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sambamba na haya, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa sababu Nachingwea tayari tumeshatenga maeneo na kupitia fedha ya Halmashauri peke yake kwa hizi 5% haiwezi kutosha kuwafikia vijana wengi, sijajua Serikali inatuambia nini ili tuweze kuona namna gani tunaweza kunufaika na fedha zinazotolewa na Mifuko ya Vijana kupitia Taifa badala ya kuachia Halmashauri peke yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, naomba nipate majibu juu ya jitihada gani ambazo zinafanywa kwa vijana wa Mikoa ya Lindi na Mtwara ukizingatia ziko baadhi ya Kanda tayari wameshaanza kuwasogezea huduma za kuwafungulia milango ya kupata ajira ikiwemo Kanda ya Ziwa, vijana wengi wanatakiwa waende kule kwa ajili ya kujiunga na vikundi vya kushona viatu. Lindi na Mtwara tunavyo Vyuo vya *VETA,* nini kauli ya Serikali juu ya vijana wa kanda hii na hasa vijana wanaotoka Nachingwea ambao hawana chuo cha namna hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza amesema kwamba, tayari wameshatenga maeneo kwa ajili ya shughuli za vijana na nichukue fursa hii kwanza kabisa kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kwa sababu mwaka 2014 Wakuu wa Mikoa wote walikutana hapa Dodoma na likawekwa Azimio la kuhakikisha kila Halmashauri nchi nzima inatenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za vijana ambayo tuliyapa jina la *Youth Special Economic Zones.* Mpaka sasa hivi ninavyozungumza tayari zimeshatengwa ekari 86,000 nchi nzima na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea nayo ni mojawapo. Kwa hiyo, niwapongeze kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake la msingi ni kwamba fedha ya Halmashauri haitoshi, ni kweli! Nataka nikiri kwamba fedha ile haiwezi kukidhi mahitaji. Hata hivyo, tunao Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao umetoa mwongozo wa kukopesha *SACCOS* za vijana katika kila Halmashauri. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awaandae vijana wake, tushirikiane kwa

pamoja, wabuni miradi, walete maombi kupitia mfuko ule tumekuwa tukitoa fedha kusaidia vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza tumeshakopesha takriban Sh.1,700,000,000 kwa vikundi mbalimbali nchini Tanzania. Ushahidi wa dhahiri kabisa ni katika Mkoa wa Simiyu chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa wa Mheshimiwa Anthony Mtaka, tumekabidhi fedha kwa vikundi viwili vya kutengeneza chaki na maziwa katika Wilaya ya Maswa na Meatu, takriban Sh. 30,000,000 kwa kila kikundi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge afanye jitihada hizo, sisi tutakuwa tayari kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anasema ni jitihada gani Serikali imezionesha katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Mheshimiwa Mbunge ni kweli, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tuna programu nyingi sana za vijana na sasa hivi tumetangaza programu ya vijana kwenda kupata mafunzo ya kutengeneza viatu na bidhaa za ngozi kule Mwanza lakini siyo kweli kwamba mikoa hii tumeisahau. Mwaka jana tumekuwa na programu kubwa sana katika Mikoa mitano ikiwemo Lindi na Mtwara ambapo tuliwafikia vijana takriban 9,100 kupitia programu inayoitwa *Youth Economic Empowerment* na mpaka ninavyozungumza hivi sasa vijana wengi wa Lindi na Mtwara walipata mafunzo kupitia *VETA* na sasa hivi wamejiajiri na wameajiri na vijana wengine. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kupanua wigo wa programu zetu ili ziweze kufika nchi nzima na vijana wote waweze kunufaika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini swali la nyongeza kwa mujibu wa swali la msingi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wilaya ya Rombo ni moja kati ya Wilaya ambazo zina tatizo kubwa sana la uhaba wa ardhi hapa nchini. Mwaka 1974 Mwalimu Nyerere aliwachukua baadhi ya vijana kuwatafutia ardhi maeneno ya Mpanda kule Mikese na Tanga kule Kilindi. Vijana wa Rombo wana nguvu na wana tamaa ya kujiajiri katika kilimo. Mheshimiwa Waziri yuko tayari nikimletea vikundi vya vijana wa Rombo ambao wako tayari kujiajiri katika kilimo kuwatafutia ardhi maeneo mengine ya nchi ili na wenyewe waweze kushiriki katika kujitafutia ajira kupitia kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, moja kati ya mkakati mkubwa ambao tumeuweka ni kuwapeleka vijana katika kilimo

cha umwagiliaji na kilimo biashara na katika utekelezaji wa programu hii hatuchagui maeneo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kushirikiana naye kwa wale vijana wa Rombo ambao wako tayari kufanya shughuli za kilimo tukawasaidia wakapata maeneo na sisi kama Serikali tukawa sehemu ya kuwawezesha ili haja yao itimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunao mpango wa kitaifa wa kilimo kati ya Wizara ya Kilimo na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu ambao lengo lake kubwa ni kwenda kuyatumia mashamba makubwa ya Serikali yale ambayo hayatumiki, yamekuwa mapori, kwa kuyatengenezea miundombinu ili vijana wengi sana waende kufanya shughuli za kilimo katika maeneo hayo. Kwa sasa tutaanzia eneo la Mkulazi Morogoro ambapo patajengwa Kiwanda cha Sukari kwa ushirika kati ya *NSSF* na *PPF,* maeneo yameshatengwa na hivi karibuni tutakwenda kuyasafisha yale maeneo na baadaye vijana watapewa maeneo hayo yakiwa yameshaboreshwa na miundombinu yake imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, vijana wa Rombo wakiwa tayari anione tu niko tayari kumsaidia. *(Makofi)*

**WENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kabla ya kuuliza swali, naomba niwape pole wananchi wa Kitongoji cha Chinyika na Kwamshango kwa maafa waliyopata ambapo watu watano wamefariki kwa kusombwa na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niulize swali. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa na anajua vijana wengi sana katika Wilaya ya Mpwapwa hawana ajira na hizo fedha zinazotolewa ni kidogo sana. Je, Naibu Waziri yuko tayari kuongeza fungu la fedha hizo ili vijana wengi waweze kupata ajira pamoja na wa Wilaya ya Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna changamoto ya Mifuko hii ya Uwezeshaji ya Mitaji na Mikopo kwa vijana hasa kwa kushindwa kukidhi mahitaji ya vikundi vingi ambavyo vimekuwa vikiomba mikopo hii. Tunachokifanya kama Serikali ni nini? Sisi kazi yetu kubwa tunayoifanya kwanza kabisa ni kuwatambua vijana

nchi nzima kutokana na mahitaji yao na kazi, pili ni kuwarasimisha na tatu ni kuwajengea uwezo wa kifedha kupitia mifuko mbalimbali ya Serikali lakini na kushirikiana na wadau mbalimbali. Nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na jitihada za kuwa-*invite* wadau wengi zaidi wa maendeleo ya vijana ili watusaidie katika eneo hili la uwezeshaji na kuongeza mfuko wetu ili tuweze kuwafikia vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, Bunge hili ndilo ambalo tunapanga bajeti, muone pia haja ya kutuongezea fedha kwa ajili ya Mfuko wa Mendeleo ya Vijana ili tuwafikie vijana wengi zaidi nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunamalizia na mtu wa mwisho, naomba swali kwa ufupi kabisa, Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa fedha hizi ambazo zimekuwa zikipelekwa katika Halmashauri ni kidogo sana kiasi kwamba hata hazitoi msaada mkubwa kwa wale vijana. Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna ubaya gani kama vijana hawa ambao walio wengi hawana ajira hasa wale wanaotoka kwenye vyuo vikuu na sehemu nyingine wakaanzishiwa Benki ya Vijana ambayo itakuwa rahisi kui-*control* na kuwapata wale wahitaji ambao kwa kweli wanataka kutumia hizo fedha vizuri hasa sehemu kama za Kilolo na hasa hapa kwake Dodoma, je, atakuwa tayari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuelekea katika uanzishwaji wa Benki ya Mendeleo ya Vijana lakini kabla hatujafikia hatua hiyo tukasema ni vyema kwanza tuwaanzishie vijana *SACCOS* mbalimbali ili tuanze kuwakopesha kupitia *SACCOS* hizo, wajifunze nidhamu ya fedha na matumizi yake na baadaye tutaenda kufikia katika uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Vijana wakati tayari tumeshaandaa kundi letu kubwa hili la vijana kwenda kushiriki katika masuala ya fedha. Vinginevyo, usipoanza na utaratibu huu wa kuwazoesha mwisho wa siku fedha ile ya mikopo inaweza kutumika katika mambo tofauti na ikawa haijamsaidia kijana huyu. Kwa hiyo, tumeanza katika *SACCOS* baadaye tutakwenda mpaka kwenye uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Vijana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 17

**Kufungwa kwa Vyuo vya Ufundi vya Watu Wenye Ulemavu Nchini**

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA** aliuliza:-

Katika miaka ya 60 na 90, Serikali yetu kwa ufadhili wa nchi rafiki kama Norway na Sweden ilijenga vyuo vya ufundi vilivyotoa mafunzo mbalimbali kwa watu wenye ulemavu hapa nchini kama vile Yombo - Dar es Salaam, Singida, Mtapika – Masasi, Masiwani – Tanga, Mbeya, Ruanzari – Tabora na Mwirongo-Mwanza; hivi sasa kati ya vyuo saba ni vyuo viwili tu vya Yombo na Singida ndiyo vinafanya kazi tena kwa kusuasua:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha vyuo hivyo vitano vifungwe wakati kuna mahitaji makubwa ya watu wenye ulemavu kupata mafunzo ya ufundi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua haraka vyuo hivyo vilivyofungwa ili viendelee kutoa mafunzo ya ufundi kwa watu wenye ulemavu?

(c) Ili kutoa fursa zaidi za mafunzo ya ufundi kwa watu wenye ulemavu, je, Serikali ina mkakati gani wa kujumuisha watu wenye ulemavu kwenye vyuo vyake vya *VETA* na *FDC?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zilizosababisha vyuo hivi kufungwa ni pamoja na uchakavu wa majengo na miundombinu isiyo rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu; upungufu wa watumishi ambapo baadhi yao wameshastaafu na wengine wamefariki.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu nchini wanapata mafunzo siyo tu ya ufundi, bali ya aina nyingine yatakayokidhi mahitaji ya ajira na kuondoa utegemezi kwa watu wenye ulemavu. Aidha, Serikali imewasilisha maombi maalum Hazina,

kuomba fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo fedha hizo zitatumika kufanya ukarabati na kuboresha miundombinu ya vyuo mbalimbali nchini. Vilevile, Wizara imewasilisha ikama ya watumishi ili utaratibu wa kuajiri watumishi ufanyike mapema kuziba nafasi zilizo wazi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali katika kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika Vyuo vya *VETA* na *FDC* ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuwa na walimu wenye mbinu za kufundisha watu wenye ulemavu. Katika kozi ya ualimu *MVTTC* ipo moduli inayohusu mbinu za kufundisha watu wenye ulemavu.

(ii) Ukarabati wa miundombinu ya njia za kutembelea na ukarabati wa majengo ili kuwapa fursa watu wenye ulemavu kushiriki katika mafunzo ya ufundi pasipo kikwazo chochote.

(iii) Kuwashirikisha wakufunzi wenye ujuzi wa lugha ya alama kupitia Chuo cha Watu Wenye Ulemavu – Yombo katika kutoa mafunzo ya ufundi kwa watu wenye ulemavu hasa katika kozi fupi fupi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kusema tu kwamba sikuridhika kabisa na nina hakika watu wenye ulemavu hawakuridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ameyatoa. Ina maana kwamba kwa kutokuwa na miundombinu au kutokuwa na watumishi ni sababu ya kutosha ya kusababisha vyuo vifungwe kwa miaka mingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupe *concrete* sababu kwa nini vyuo vimefungwa na vitafunguliwa lini, atupatie *time frame*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hawa watumishi ambao anasema wanatayarishwa, tunahitaji muda gani kuwatayarisha hawa watumishi kwa sababu watu wenye ulemavu wamekuwepo na vyuo vimekuwepo miaka mingi lakini vimefungwa kwa miaka mingi na inaonekana kama ni *business as usual but it is not business as usual.* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri umefahamu hayo maswali ya nyongeza. Naibu Waziri wa Elimu, naomba majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kimsingi, pamoja na kufungwa kwa vyuo hivyo jambo ambalo tayari limeshatolewa ufafanuzi namna gani litafanyika, kupitia mfumo wa elimu jumuishi sasa hivi vyuo vyote vya ufundi ikiwemo *VETA, FDC* lakini hata shule zinazotoa mafunzo ya ufundi tunahakikisha kwamba tunazingatia namna tunavyoweka miundombinu na namna ya kufundisha kwamba watu wenye ulemavu wanazingatiwa. Hao nawazungumzia hasa wale vijana wenye umri wa kuweza kuingia katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu kwamba, kwa hali ya sasa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia lakini pia kupitia ngazi zetu za juu kama tulivyoona Ofisi ya Waziri Mkuu, tunahakikisha kwamba walemavu wanapewa kipaumbele cha hali ya juu na yeye atakuwa shahidi hata sasa tunapotoa kwa mfano karatasi zetu humu Bungeni au taarifa zozote lazima tuzi-*print* kwa nukta nundu na mambo mengine. Kwa hiyo, walemavu wanapewa fursa nyingi na tunawajali kupita kiasi katika kila ngazi. Naomba atuvumilie aone namna ambavyo tutaweza kuendelea katika kuhakikisha tunarekebisha hali ambazo zipo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Amina Mollel swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto katika suala zima la elimu na hasa elimu jumuishi kwa watu wenye ulemavu ni kutokana na uhaba wa walimu katika vyuo mbalimbali hasa vyuo vikuu hapa nchini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba katika vyuo vyote vikuu hapa nchini vinakuwa na programu mahsusi kabisa kwa ajili ya kuwafundisha walimu watakaokwenda kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu hapa nchini ili tuondokane na tatizo hili la uhaba wa walimu pamoja na kuhakikisha kwamba ajira zinakuwepo kwa watu wenye ulemavu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ili kufanikisha hilo, kwa mfano ukiangalia katika

utoaji wa mikopo safari hii watu wenye ulemavu wote kwa ujumla wake bila kujali fani anayochukua wamepewa mikopo. Pili, tunacho chuo maalum, Chuo cha Patandi - Arusha ambacho ni kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa walimu ambao wanaenda kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu. Hali kadhalika, kwa upande wa vyuo vikuu tunayo maeneo ambayo yanahusika katika kuzingatia ufundishaji wa walimu kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake niseme tu kwamba eneo hili ni pana sana kwa sababu linahitaji walimu wa aina tofauti tofauti kwa ajili ya kufundisha watu wenye ulemavu wa aina tofauti tofauti. Kwa hiyo, ukiwachukua kwa ujumla wake useme kwamba walimu wenye ulemavu labda 200 ukafikiria ni wengi, hawatakuwa wengi kwa sababu mahitaji ya wale wanaoenda kuwafundisha inakuwa wanafunzi ni wachache katika eneo fulani lakini yale maeneo ni mengi sana. Kwa hiyo, juzi tu mimi mwenyewe nimefuatilia pale Patandi na kuona ni jinsi gani tutaweza kurekebisha hasa miundombinu na kuwawezesha walimu wengi zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ikupa Alex swali la nyongeza!

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mawaziri, kuna hivi vyuo viwili Chuo cha Yombo na Chuo cha Singida, pamoja na uwepo wa vyuo hivi viwili lakini bado kuna changamoto nyingi sana ambazo zinavikabili vyuo hivi. Naomba niongelee *specific* Chuo cha Yombo kwa sababu ni chuo ambacho nimekitembelea. Chuo hiki kina changamoto ya deni kubwa la umeme, miundombinu chakavu pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Naomba nisikie kauli ya Serikali ni hatua gani za haraka na za makusudi za kunusuru vyuo hivi ili visije vikafungwa kama ambavyo vimefungwa hivi vyuo vingine? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa upande wa chuo hicho nikiri pia hata mimi nimewahi kukitembelea kilikuwa na upungufu fulani lakini kama ilivyozungumzwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ni kwamba kimewekwa kwenye bajeti. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha tayari Wizara ya Elimu tulikuwa tumeagiza vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu vya gharama ya shilingi takribani bilioni tatu na tayari vimeshawasili. Kwa hiyo, tutaangalia katika ugawaji na wao waweze kufikiriwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa tunaendelea na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Na. 18

**Muda wa Kuegesha Magari kwa Kibali**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB (K.n.y. MHE. IBRAHIMU HASSANALI MOHAMMEDALI)** aliuliza:-

Wenye maduka waliopewa kibali cha kuegesha magari yao kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni wameonekana wakihodhi nafasi hiyo kwa saa 24:-

(a) Je, ni lini watu wenye tabia hiyo watachukuliwa hatua za kisheria?

(b) Katika Jiji la Dar es Salaam wakati wa usiku inakuwa kama mji huo hauna sheria kwa sababu wenye magari huegesha magari hovyo na kusababisha adha kwa watu wengine. Je, ni lini Serikali itawachukulia hatua watu wa aina hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Mohammedali, Mbunge wa Kiembe Samaki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo ya Maegesho ya Magari *GN*. Na. 60 ya mwaka 1998 kifungu cha 6(1) kinaipa mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Saalam kudhibiti na kusimamia maeneo ya maegesho ya magari yaliyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria ili kuondoa kero, usumbufu na msongamano katika mitaa na barabara za umma. Kwa mujibu wa sheria hiyo, maegesho yote ya magari ya kulipia na maegesho yaliyohifadhiwa yanatumika kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni. Baada ya muda huo maeneo hayo huwa huru kwa matumizi ya umma. Pale inapobainika mtu kuhodhi maeneo hayo baada ya saa 12.00 jioni, Halmashauri ya Jiji huchukua hatua kwa mujibu wa sheria.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ukaguzi na udhibiti wa maeneo ya maegesho imetolewa kwa Mawakala katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda

kutoa wito kwa wamiliki wote wa magari kuacha kuegesha magari bila utaratibu hasa wakati wa usiku na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wengine. Serikali haitasita kuchukua hatua kwa wote watakaobainika kukiuka taratibu za maegesho ya magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa sababu kufanya hivyo ni kusababisha msongamano na kero kubwa kwa wengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Muuliza swali.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali ya nyongeza, mji umebadilika, je, Serikali haioni haja nayo ibadilike kuleta sheria nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa baadhi ya watendaji wake wanaokusanya zile shilingi mia moja hamsini, mia mbili wamekuwa na kauli ambazo haziridhishi kwa wananchi, je, anatoa wito gani?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jaku, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mji umebadilika lakini kama nilivyosema kwamba Halmashauri ya Jiji kuna sheria ambayo inaongoza utaratibu katika maeneo hayo nayo ni Sheria Ndogo yenye GN Na.60. Naamini kwa sababu kuna wadau mbalimbali na Mheshimiwa Jaku najua ni mdau wa Jiji la Dar es Salaam lakini na Wabunge na Waheshimiwa Madiwani wa maeneo hayo kama wakiona kuna haja ya kurekebisha Sheria Ndogo hiyo basi wafanye hivyo na sisi Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambao ndiyo wenye jukumu la kufanya mchakato huu uweze kukamilika tutalishikia bango jambo hili liweze kuwa mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine alilosema ni kuhusu kero ya ukusanyaji wa fedha hizo lakini hata uaminifu wa upelekaji fedha zile haupo. Kwa bahati nzuri sasa hivi katika Jiji la Dar es Salaam tuna Mkurugenzi makini sana naamini kwa hizi changamoto ndogondogo zinazobainika tutazisimamia kwa pamoja ili kuzitatua. Lengo ni wananchi wanaoegesha magari yao katika Jiji lile kupata huduma bora bila kupata usumbufu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jiji la Dar es Salaam linashangaza kwani wamechukua kampuni ya kutoka Kenya ili kukusanya fedha za maegesho ya magari Dar es Salaam. Vilevile hawatumii mashine za *EFD* kukusanya pesa na kupandisha kutoka Sh.300 kwenda Sh.500. Hivi kweli nchi nzima ya watu milioni 50 wamekosa kampuni yoyote katika nchi yetu mpaka kuchukua Kampuni ya Kenya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue *concern* hii ya Mheshimiwa Keissy lakini ninavyojua katika suala la ukusanyaji Manispaa za Ubungo, Ilala na Kinondoni zinakusanya zenyewe lakini kwa ukubwa wake Manispaa ya Temeke na Kigamboni, Halmashauri ya Jiji yenyewe inasimamia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kampuni kutoka Kenya kukusanya nadhani huo ni mchakato wao lakini ninavyojua ni kwamba kuna utaratibu maalum kwa Jiji la Dar es Salaam, kila Manispaa kwa maana ya Ilala, Kinondoni na Ubungo zina utaratibu wake wa kukusanya ila Manispaa ya Temeke na Kigamboni Jiji lenyewe linasimamia kwa taarifa nilizokuwa nazo, wanasimamia kama Wakala wa Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy kuhusu hii kampuni kutoka Kenya kukusanya fedha hizi ngoja tuzi-*cross check* zaidi lakini inawezekana ni taarifa za kimagazeti zaidi kuliko uhalisia wake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 19

**Vitendo vya Kikatili Kukithiri Nchini**

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI** aliuliza:-

Kumekuwa na tabia za watu kupiga watu wengine hovyo kila siku, vipigo hivyo vinafikia kiasi cha utesaji *(torture)* kama ilivyotokea Mbeya Sekondari kwa walimu kumshambulia mwanafunzi au mtu kumtoa macho kama ilivyotokea huko Buguruni na maeneo mengine:-

(a) Je, Serikali inaona mateso haya wanayopata Watanzania kutoka kwa Watanzania wenzao?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuwalinda wananchi na vitendo hivi vya kikatili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hivi karibuni kumekuwepo na vitendo vya kusikitisha katika nchi yetu na kwa jamii ambavyo ni kinyume cha sheria na havikubaliki. Aidha, Serikali haikubaliani na vitendo vya namna hii vinavyofanywa na mtu/watu/ kikundi kwani vitendo hivyo ni kinyume na sheria na utaratibu mzima wa haki za binadamu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuzuia na kuwalinda raia na mali zao. Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Polisi hupokea taarifa za matukio mbalimbali na kuyafanyia uchunguzi wa kina na inapobainika upo ushahidi wa kutosha, mtuhumiwa huchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria. Nichukue fursa hii kuwaasa sana wale wote ambao wanakiuka taratibu, kanuni na sheria za nchi waache tabia hiyo mara moja. Wizara yangu haitakuwa na suluhu na mtu yeyote atakayetenda uhalifu huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, napenda niipongeze Serikali kwa kukubali kwamba kuna tatizo la utesaji na *torture* kwa sababu siku hizi kumekuwa na utaratibu na utamaduni wa kukataa na kukanusha kila kitu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kukubali kwamba kuna tatizo la utesaji na *torture*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu limejibiwa kwa wepesi na ujumla sana. Kwenye swali langu la msingi nili-*cite* kwa mfano, kinachoendelea kuhusu Mwalimu Msigwa na wenzake ambao walimfanyia *torture* au shambulio la kudhuru mwanafunzi wa Mbeya Sekondari ambapo mpaka leo hii wazazi wana hofu na watoto wao katika shule ile kiasi kwamba wanamsukuma Mbunge kutaka kujua ni nini hatma ya wale walimu kwa sababu maneno

yamekuwa mengi. Mara wanasema amri kutoka juu imesema kwamba waachiwe na kadhalika...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiuliza sana na juzi nimeuliza kwenye Kamati lakini Waziri wa Elimu anasema hana habari.

**MWENYEKITI:** Naomba umuulize swali Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali usizungumzie masuala ya Kamati.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tafadhali naomba swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimeuliza kwenye Kamati wanasema chuo kimeunda tume, chuo kinafanya uchunguzi wa jinai toka lini wakati suala hili liko wazi kwenye *video* ilienda *viral* wale walimu walitesa watoto tunawatetea walimu lakini wanapovunja sheria ni lazima hatua zichukuliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kujua ni nani aliyetoa amri kwamba wale walimu waachiwe wasichukuliwe hatua za kisheria kwa kosa la jinai walilofanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Watanzania wanaowatesa wenzao ni pamoja na Polisi. Watanzania hawa Polisi, kwa mfano wakati wa Operesheni UKUTA ambayo tuliisitisha kwa maslahi ya Taifa, walikamata watu, waka-*torture* mfano Mtanzania Nyagali maarufu kama Mdude wa Mbozi ambaye mpaka leo hii amevunjwa miguu na hayuko sawasawa. Sasa Taifa hili limekuwa Taifa la *disappearance* watu wanapotea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uulize swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue kwa nini isiundwe Tume ya Kimahakama kama ile aliyounda Mheshimiwa Kikwete ya kuchunguza Operesheni TOKOMEZA ili kuchunguza maovu haya yanayofanywa na Watanzania ambao wana *uniform* za kipolisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la walimu ambao wamewanyanyasa wanafunzi kwenye shule ya Mbeya *Day* niseme ni mtambuka kwa hiyo hatua mbalimbali zinachukuliwa na mamlaka husika. Kwa upande wa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Mashtaka *DPP* kuna hatua ambazo zinaendelea kuchukuliwa na pale ambapo ushahidi na uchunguzi utakapokamilika watafikishwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu kuundwa Tume ya UKUTA, kwanza tulishazungumza mapema kwamba mkusanyiko wowote ambao si halali hautaruhusiwa na hivyo Jeshi la Polisi litasimamia kuhakikisha kwamba linalinda usalama wa nchi hii kwa kuzuia mikusanyiko yoyote ambayo siyo halali. Kwa hiyo, kama ikiwa Jeshi la Polisi limetekeleza majukumu yake kuzuia mkusanyiko ambao si halali limefanya hivyo katika kutekeleza majukumu ya kawaida na tunawasihi wananchi pale wanapoelekezwa kutii sheria za nchi, basi watii sheria za nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Msabaha halafu tutamalizia na Mheshimiwa Faida.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na tabia ya wananchi au vyombo vya ulinzi na usalama na wengine ambao wanakwenda kwenye mafunzo ambayo siyo halali kutesa raia wasiokuwa na hatia na kuwasababishia maumivu makali na hatimaye kupelekwa rumande bila kupatiwa huduma za kiafya. Je, Serikali hamuoni kama mnavunja haki za binadamu na utawala bora? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Maryam Msabaha liko *too general,* nadhani si sahihi kusema Polisi kazi yao ni kutesa raia. Polisi wamekuwa wakifanya kazi ya kulinda raia na kazi hii imefanyika kwa mafanikio makubwa sana na ndiyo maana mpaka leo nchi yetu iko salama. Ningemwomba Mheshimiwa Maryam Msabaha kama ana tukio *specific* ambalo linamhusisha Polisi kwa kufanya tendo lolote ambalo limekwenda kinyume na sheria basi aliwasilishe ili hatua zichukuliwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendela na Mheshimiwa Faida.

**MHE FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mbali na kujitokeza watu ambao wanawanyanyasa binadamu wenzao kwa kuwapiga lakini kuna baadhi ya watu hususani kule Pemba wanachoma mashamba ya mikarafuu, wanawapiga watu na kuwachomea nyumba. Je, Serikali imechukua hatua gani ya kuwalipa fidia watu waliodhalilishwa kwa matukio kama hayo? Vilevile imewachukulia hatua gani wahalifu hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwepo na matatizo ya wananchi kujichukulia sheria mkononi na hili si tu kwenye mikarafuu lakini tumeshuhudia hata kwenye upande wa wakulima na wafugaji. Tamko letu kama Wizara na kama Serikali tunasema hakuna sababu yoyote ile inayotosha kuhalalisha mwananchi kuchukua sheria mkononi dhidi ya mwenzake iwe kwa kudhuru maisha yake ama kwa kudhuru mali zake. Yeyote atakayefanya hivyo tumesema atafika kwenye mkono wa sheria na wale ambao walishafanya hivyo tumesema wachukuliwe hatua ili iwe mfano na kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelekeza na Waheshimiwa Wabunge nawaomba kwenye hili tukubaliane, ili Serikali ionekane ipo na inatetea wale wanaoonewa tutachukua hatua kali kwa wale wanaofanya vitendo hivi vya kihalifu dhidi ya wenzao. Hii ndiyo itakuwa njia pekee ya kuweza kuhakikisha kwamba wananchi hawajichukulii sheria mkononi kwa sababu duniani kote sheria isipochukua mkondo wake ndipo wananchi huchukua sheria mkononi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Na. 20

**Chuo cha MCH - Wilaya ya Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru kulikuwa na Chuo cha *MCH* kilichokuwa kikitoa mafunzo ya taaluma mbalimbali za afya kwa vijana wengi

wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru lakini mwaka 1980 chuo hicho kiliungua moto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukikarabati chuo hicho ili kiweze kuendelea kutoa wataalam wa afya kama hapo awali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Tunduru ni mojawapo wa vyuo vilivyokuwa vimefungwa baada ya kusitisha mafunzo ya *Martenal and Child Health Aider* mwaka 1998. Chuo hiki ambacho kipo katika eneo la Hospitali ya Tunduru kiliungua moto sehemu ya bweni na bwalo la chakula. Katika utekelezaji wa mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) vyuo vinne vya aina hii ambavyo vilikuwa vimefungwa vilifanyiwa tathmini mwezi Agosti 2008 kwa nia ya kuvifufua kuanza kutoa mafunzo kwa wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tathmini hiyo ilipendekezwa Vyuo vya Nzega, Nachingwea na Kibondo vifufuliwe na kuanza kutoa mafunzo ili kuchangia kuongeza idadi ya wataalam kutokana na mahitaji ya Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya Chuo cha Tunduru hakikukidhi vigezo vya kufufuliwa kutokana na gharama kubwa iliyohitajika kufanya ukarabati. Aidha, nafasi ya upanuzi wa chuo ilikuwa ndogo hivyo kupendekeza sehemu hiyo ya chuo kujumuishwa kwenye hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Mheshimiwa Daimu Mpakate swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa chuo kile hakikukidhi haja ya kukikarabati na kwa kuwa katika majibu ya msingi yamesema kwamba eneo la chuo lilikuwa dogo. Je, Serikali haioni haja ya kujenga chuo kipya kwa

sababu Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina maeneo mengi ambayo yangeweza kujengwa chuo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi katika Idara ya Afya kwa zaidi ya 70%. Ni kwa nini sasa Serikali isitoe upendeleo maalum kwa ajili ya Wilaya ya Tunduru na kwa vijana wa Tunduru ili waweze kuhudhuria mafunzo hayo katika vyuo ambavyo vimefufuliwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo haja ya kujenga vyuo vipya kwa ajili ya kutoa mafunzo ya watumishi kwenye sekta ya afya, si tu kwa Tunduru lakini ni kwa nchi nzima. Bahati mbaya sana Mpango wa *MCH Aider Training* ulipoanzishwa mwaka 1973 ulilenga kuzalisha wataalam wa kutoa huduma za uzazi kwa akinamama vijijini kwenye zahanati ambazo zilikuwa zinaanzishwa kwenye mpango ule kutokana na Azimio la Alma-Ata miaka hiyo na Azimio la Afya kwa Wote enzi za miaka ya 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ule umebadilika na hatuwezi kujenga tena chuo kwenye kila mkoa kwa sababu mpango wa kujenga Vyuo vya *MCH* Serikali iliazimia kujenga chuo kwenye kila mkoa ili kuwazalisha hawa *MCH Aider* kwa kuwapa kozi ya mwaka mmoja na nusu kwa haraka ili tuwapate kwa wingi zaidi waweze kuwahi kwenda kuokoa maisha ya akinamama wajawazito na watoto. Mpango ule haupo tena na kwa maana hiyo vyuo vya afya sasa hivi haviwezi kuwa ni vyuo vya afya kwa kila mkoa bali vinakuwa ni vyuo vya afya vya kitaifa na utaratibu sasa hivi tunashirikisha pia sekta binafsi ambao nao wanaanzisha vyuo kwa ajili ya kutoa mafunzo ya taaluma mbalimbali za kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kwamba Tunduru wapate watumishi kwenye sekta ya afya, hili ni katika mipango ya Serikali ambayo ni endelevu. Kadri ambavyo tutapewa vibali vya kuajiri watumishi kwenye sekta hii ndivyo ambavyo tutaendelea kuajiri watumishi wapya na kuwatawanya si Tunduru peke yake bali ni kwenye wilaya zote hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mbali na changamoto ambayo inakikabili Chuo cha Maendeleo ya Jamii - Kisangwa kuhusiana na kutopata fedha za uendeshaji, karakana na kadhalika lakini chuo hicho pia hakina gari. Hivi tunavyozungumza aliyekuwa Mkuu wa Chuo alijiuzia *VX* kwa Sh. 600,000/= na kufanya Mkuu wa Chuo wa sasa hivi asiwe na gari na kusababisha shughuli za chuo zisiende. Je, Serikali iko tayari kushughulikia ufisadi huu kwa sababu hakuna *VX* inayouzwa Sh. 600,000/= na kupeleka gari ili chuo hicho kiendeshe shughuli zake vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali kutoka kwa rafiki yangu Mheshimiwa Ester Amos Bulaya kuhusu kile anachopenda kukiita ufisadi. Majibu ya Serikali ni kwamba kwenye kuuza mali za umma ambazo zimemaliza muda wake na ama zimekuwa *classified* kama ni *dilapidated* ama mali zilizochoka unajulikana na umeandikwa. Kwa hivyo, kama Mheshimiwa Mbunge ana ushahidi kwamba utaratibu huu ambao umeandikwa kwenye sheria mbalimbali za kuuza mali za Serikali zilizochakaa haukufuatwa, naomba anikabidhi nyaraka alizonazo ili niweze kufuatilia na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa sasa wanafunzi wa vyuo vikuu wamekuwa wengi ukizingatia Chuo hiki cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kimeanza kujaa. Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha vyuo vidogo vya diploma kama vile vya Monduli *CDTI* ili kuwa *university* kuweza kuwa-*accommodate* vijana waweze kusoma kwa wingi maana elimu inayotolewa na vyuo hivi ni nzuri sana kwa ajili ya Taifa letu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali haina utaratibu wa kuendelea kuvipandisha vyuo vya taaluma za kati kuwa vyuo vya kutoa *degree* kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano haiamini kwamba inahitaji watu wengi zaidi wenye *degree* kwenye soko la ajira, hapana! Serikali ya Awamu ya Tano inahitaji watu wengi zaidi wenye ujuzi kwa ajili ya ku-*support* uchumi wa

viwanda na maendeleo ya kilimo na maendeleo ya biashara na ujasiriamali vijijini. Kwa hivyo, tutaendelea kuvijengea uwezo vyuo vyetu vya *CDTI* nchi nzima ili viendelee kutoa kozi kwenye ngazi hii ya wanataaluma na watu wenye ujuzi wa kati ili ku-*support* uchumi wa viwanda ambao tunaujenga kwa sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa naomba uniruhusu dakika moja tu kabla Serikali haijatoa majibu ya swali namba 21. Nimshukuru Mheshimiwa Chenge siku ya tarehe 4 Novemba, alipouliza swali la nyongeza, swali namba 45 lililozaa swali hili la Mheshimiwa Faida Mohamed na likajibiwa na Wizara ya Fedha, lakini hatimaye leo hii naona linapigwa danadana na likatupwa Wizara ya Elimu. Swali liko wazi kwa Wizara ya Fedha inatakiwa itoe majibu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umepewa ruhusa ya kusema swali lako lijibiwe sasa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niendelee tena kumshukuru Mheshimiwa Chenge anapokalia Kiti chake…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba useme tu naomba swali langu lijibiwe.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Kwa hekima na busara anazotumia kwenye Kiti hicho na akawajali Watanzania kuhusu suala hili la msingi kwa Watanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku…

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Naomba Serikali itoe majibu ya swali hili sasa.

Na. 21

**Ulipaji wa Ada kwa Fedha za Kigeni**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya wanafunzi wa elimu ya juu Tanzania ambao ni wazawa kulipishwa ada ya masomo yao kwa fedha za kigeni badala

ya fedha za Kitanzania wakati wao ni Watanzania na vyuo hivyo viko hapa nchini licha ya Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* kulipigia kelele sana jambo hilo:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa kuna tatizo hili na kama inatambua imechukua hatua gani dhidi ya tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa kilio hiki kipo kwenye taasisi mbalimbali kama vile bandarini, uwanja wa ndege, hoteli na taasisi za fedha na kadhalika, je, Serikali inatoa tamko gani juu ya jambo hili?

(c) Je, kuna sheria yoyote ya nchi inayomtaka mwanachuo wa Kitanzania kulipa ada kwa pesa ya kigeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, kutoka Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa swali kama hili lilijibiwa Bungeni mnamo tarehe 7/9/2016 na lilikuwa ni swali namba 24. Baada ya maagizo yaliyotolewa kwa wamiliki wa vyuo kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa hakuna malalamiko kuhusiana na vyuo kutoza ada kwa Watanzania kwa fedha za kigeni yaliyowasilishwa. Hivyo, kama kuna chuo chochote kinachotoza ada kwa Watanzania kwa fedha za kigeni naomba tupate taarifa rasmi ili hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, sarafu inayotakiwa kutumika Tanzania ni Shilingi ya Kitanzania kwa mujibu wa kifungu cha 25 na 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* ya mwaka 2006. Aidha, kwa Tanzania malipo ya kitu au huduma yoyote inapaswa kulipwa kwa Shilingi ya Kitanzania kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 28 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni hakuna.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ally Saleh, aah Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na kutotaka kuniona naomba niulize maswali madogo sana mawili ya nyongeza na niombe Waziri wa Fedha awe tayari kumsaidia Naibu Waziri. Ninachozungumza ni Kiswahili wala si Kihindi. Waziri wa Fedha ningeomba akainuka yeye maana hili swali linamhusu yeye. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge ni chombo kizito cha Tanzania na Watanzania wametutuma ili tuyasemee matatizo yao. Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri atakuwa yuko tayari kujiuzulu pindi nikimletea ushahidi wa kutosha juu ya suala hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kujiuzulu pindi nikimletea ushahidi wa kutosha juu ya kadhia hii kwa vijana wa Tanzania kutozwa fedha za kigeni katika vyuo hivyo na anajibu hapa hamna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, amefanya utafiti kwenye vyuo gani mpaka akatueleza hakuna utaratibu wa kutoza fedha za kigeni ili Bunge lako liweze kuridhia tatizo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, swali la tatu, hakuna sheria…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni maswali mawili tu ya nyongeza tafadhali, yametosha hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote anayekuwa hatendewi haki kwa mujibu wa sheria anayo fursa ya kuchukua hatua. Hatua mojawapo ni pamoja na kutoa taarifa kwa ngazi zinazohusika. Ndiyo maana nimesema kwamba kwa kipindi chote hiki Wizara yetu haijaweza kupata taarifa na hata wewe ulivyoendelea kuuliza umeshindwa hata kutuambia mfano wa chuo ambacho kinafanya hivyo. Kwa misingi hiyo, mimi nachukulia hilo suala halipo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio!

**WABUNGE FULANI:** Lipo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Ni mpaka tutakapopata taarifa.

**MWENYEKITI:** Jamani naomba utulivu tafadhali tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusiana na kufanya utafiti, ni sawa, ni jambo jema, hilo nalichukua kuendelea kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Kuhusu Utaratibu. Mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja.

**MWENYEKITI:** Mwongozo saa hizi! Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri aendelee.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja.

**MWENYEKITI:** Kuna majibu kwa ufupi anajibu Mheshimiwa Waziri halafu utaendelea.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mwongozo, mwongozo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili limekuwa likijirudia mara nyingi na naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 inamruhusu mtu yeyote kupokea na kumiliki na kutumia fedha za kigeni kwa shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo, hao wenye shule siyo kwamba hawaruhusiwi, hilo la kwanza tuelewane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 inaweka bayana kabisa kwamba *legal tender* ya nchi yetu ni Shilingi ya Kitanzania. Nilikwishalieleza Bunge lako Tukufu kwamba ni makosa kwa mtu yeyote kukataa Shilingi ya Tanzania kwa malipo hapa nchini. Kwa hiyo, narudia tena, pale ambapo kuna Mtanzania yeyote anakwenda kulipa ada au malipo mengine akadaiwa kwa dola lakini yeye akatoa Shilingi za Kitanzania akakataliwa, atoe taarifa mara moja ili tuchukue hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Benki Kuu tumeshafanya utafiti na nilikwishalitolea taarifa hapa ni 3% tu ya shughuli mbalimbali ambazo wana-*quote* bei zao kwa dola. Kwa hiyo, kosa ni kukataa shilingi kosa sio ku-*quote* bei zao kwa dola.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, umeeleweka, kwa vile nilishamtaja Mheshimiwa Ally Saleh tumalizie moja.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwa kuwa umeshanitaja nina haki ya kuuliza swali la nyongeza pengine ndiyo unanipa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Zama hizi si rahisi kukataa kuja kwa wawekezaji kuwekeza katika shule za kigeni na vyuo vikuu mfano ni Shule za Sekondari kama Feza na nyinginezo. Serikali haioni kuna haja kwa utata huu unaotokezea, kwa mfano Chuo cha *KIU,* Chuo Kikuu cha Zanzibar kiliwahi kutoza kwa dola na Serikali inasema haijui kuwa na sera ya vyuo au shule zinazokuja hapa ili waelewe nini wafanye na nini wasifanye ikiwa ni pamoja na kutolazimishwa na nchi za kigeni kufunga shule kwa sababu ya maslahi yao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi vyuo vyote vimeshaelekezwa na vimejua nini wajibu wao kufuatana na kanuni na taratibu na sheria hizi. Labda jambo ambalo naweza

nikalichukua ni kuendelea kuvikumbusha vyuo kama ambavyo tumekuwa tukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia nafasi hii niombe tu kuvisisitiza vyuo pamoja na kwamba wanao uhuru huo wa kuweza kutumia fedha za kigeni lakini suala liwe ni kwamba mwananchi wa Tanzania sarafu yake ni Shilingi ya Kitanzania. Kwa hiyo, hiyo ipewe kipaumbele badala ya kutoa kipaumbele kwa fedha za kigeni.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 22

**Kujenga Miundombinu Mipya Chuo Kikuu Mzumbe**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Chuo Kikuu cha Mzumbe ni chuo kikongwe chenye historia tangu mwaka 1953 kipindi cha ukoloni na mwaka 1972 kupandishwa hadhi kuwa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo *(IDM)* kikiwa na miundombinu ya kukidhi wanafunzi wasiozidi 1,000. Kwa sasa chuo hiki kina jumla ya wanafunzi 11,282 ambapo idadi hii ni sawa na ongezeko la 874.3% wakati hali ya majengo na miundombinu kwa kiasi kikubwa bado ni ile ile ya mwaka 1972:-

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga miundombinu mipya ikiwemo madarasa, mabweni, ofisi za Wahadhiri, jengo la utawala na kadhalika ili kukidhi mahitaji ya ongezeko kubwa la wanafunzi na Wahadhiri waliopo na watakaokuja na kukifanya chuo hiki chenye historia kubwa kiwe na taswira ya chuo cha kisasa na hadhi ya kimataifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshaanza kujenga miundombinu mipya kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kudahili na kuleta tija kwa Chuo Kikuu

cha Mzumbe. Kati ya mwaka 2010/2011 hadi 2015/2016, Serikali ilitenga na kutoa jumla ya Sh. 8,075,490,199 fedha za maendeleo kwa ajili ya ukarabati na kujenga majengo na miundombinu mipya katika Kampasi za Mzumbe, Mbeya na Dar-es-Salaam. Aidha, kwa mwaka 2016/2017, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na majengo katika Kampasi Kuu ya Mzumbe na shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya katika Kampasi ya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilidhamini chuo kujenga jengo jipya la ghorofa tano lenye thamani ya shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kumbi za mihadhara, maktaba, ukumbi wa mikutano na ofisi katika Kampasi ya Dar-es-Salaam ambalo limekamilika na linatumika. Katika Kampasi ya Mbeya jengo jipya la ghorofa mbili la maktaba lenye vyumba vya maabara ya *computer* na ofisi limekamilika na limeanza kutumika mwaka 2015/2016. Vilevile ujenzi wa jengo la taaluma na utawala lenye ghorofa mbili unaendelea na unafadhiliwa na Serikali pamoja na mkopo kutoka kwa Mamlaka ya Elimu *(TEA)* kwa thamani ya shilingi bilioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi hizi za ukarabati, ujenzi na mipango inayoendelea kutekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Mzumbe ni dhahiri kwamba Serikali ina nia ya dhati ya kuinua hadhi ya chuo hiki na hivyo kuweka mazingira stahiki ya kufundishia na kujifunzia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jasmine swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati unahitaji fedha za kutosha na Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa muda mrefu kina madai halali sana kutoka Serikalini ambapo chuo kinaidai Serikali kama vile fedha za ada kutoka Bodi ya Mikopo. Fedha hizi zingeletwa mapema zingeweza kusaidia kufanya ukarabati. Je, ni lini sasa Serikali itaweza kulipa madeni haya ili Chuo Kikuu cha Mzumbe kiweze kufanya marekebisho haya madogo madogo na kukifanya chuo hiki kiweze kuwa na muonekano mzuri kuliko ilivyo sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama ambavyo amezungumza Mheshimiwa Mbunge Dkt. Jasmine ni kweli kuna umuhimu mkubwa sana wa kufanya marekebisho katika chuo hiki, lakini pia katika suala la ada kuna wakati tulikuwa tumeagiza vyuo vyote kufanya uhakiki hasa kwa wale wanafunzi ambao walikuwa hawastahili kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, alishatoa maagizo kwamba Bodi ya Mikopo ipeleke fedha hizo wakati uhakiki ukiwa unaendelea ili wasikwamishe shughuli zinazoendelea. Kwa hiyo, naamini muda wowote ule hizo fedha watakuwa wamezipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imedhamiria kuona kwamba vyuo vyote vikuu vinaongezewa fedha ili kuongeza udahili unaostahili kwa wanafunzi ili kwenda kusoma kwenye chuo binafsi iwe ni hiyari zaidi ya mwanafunzi kuliko kuwa ni sababu ya kukosa nafasi katika vyuo vyetu vya Serikali. Kwa hiyo, naamini mpango huu ukikamilika hali itazidi kuwa nzuri zaidi kwa vyuo vyote ikiwepo Mzumbe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo, halafu atafuata Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Saddiq Murad atamalizia.

**MHE. SUSAN J. A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Katika siku hizi za karibuni, Tanzania tumepata sifa kubwa sana ya kuwa na chuo kikubwa sana Afrika Mashariki na Kati, Chuo Kikuu cha Dodoma; na chuo hiki kinaweza kuchukua takribani wanafunzi 40,000. Kwa mshangao mkubwa sana, leo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeamua kufanya Chuo Kikuu cha Dodoma kuwa sehemu ya majengo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, Serikali kwa kuleta utaratibu wa kubadili au wa kuchanganya wanafunzi na majengo ya Serikali (Wizara), maana yake ni kwamba tunachukua wanafunzi wetu kuwapekeleka kwenye simba. Nataka kujua huu ndiyo utaratibu wa kuhamia Dodoma kwa maana ya kubadilisha miundombinu ya elimu kuwa Ofisi za Serikali? Naomba majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumfahamisha Mheshimiwa Suzan Lyimo kwamba pamoja na hayo aliyoyazungumza, ukweli ni kwamba chuo maana yake siyo majengo peke yake. Chuo maana yake ni majengo, Walimu pamoja na vitendea kazi vingine vya kufundisha na kufundishia. Kwa hali hiyo Chuo cha *UDOM* kilipojengwa kilijiwekea utaratibu wa namna gani kitakuwa kinakua sambamba na majengo. Kwa hiyo, kwa taasisi au Wizara kuhamia katika majengo haya ni kwa vile ni suala la muda mfupi na kwa sababu majengo hayo yalitokana na…

**WABUNGE:** Aaaaah!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu, tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Kulingana na utaratibu na mipango yake ya kukua yalikuwa kwa sasa hayatumiki. Wizara zinatafutiwa maeneo yake ya kujenga, *CDA* wakishakamilisha kuleta viwanja hivyo, kila Wizara itakuwa na majengo yake katika eneo lake.

Kwa hiyo, niwaombe tu kwamba suala la kuhamia Dodoma, sisi kwetu tunaona ni suala lenye tija na litaongeza ufanisi mkubwa hasa kwa wananchi wetu kwa sababu sasa watakuwa wanapata huduma kiurahisi zaidi, ikizingatiwa kwamba Dodoma hata foleni hakuna na ni Makao Makuu ya nchi. Kwa hiyo, sisi Wizara tumejipanga na tutahakikisha kwamba tutahamia kwenye maeneo yetu muda ukifika. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru. Mheshimiwa Jenista.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa hapa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba nia ya Serikali katika kukiendeleza Chuo cha Dodoma ilijidhihirisha kutokana na nia njema ya Chama cha Mapinduzi kutoa… *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Nia njema ya Chama cha Mapinduzi kutoa…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Acha porojo wewe!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Kutoa ukumbi wake na kubadilisha matumizi…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Acha porojo, jibu hoja!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Kutoka kwenye matumizi ya Chama kuwa Chuo Kikuu cha Watanzania wote.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mmepeleka wanaume wazee bila wake zao! Jibuni hoja!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, naomba upunguze sauti tafadhali. Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hiyo hiyo ya nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunaendelea na mpango wa Taifa wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya kuhamishia Serikali Dodoma. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge… *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nakupeleka chuoni…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Majengo yatakayotumika na Serikali ni majengo…

**MBUNGE FULANI:** Ni majengo ya chuo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Ni majengo ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilishayajenga na yakawa mengi. Kwa sababu majengo yale ni mengi na yamejengwa na Serikali hii, badala ya kuyaacha yaharibike bila kutumika, yatatumika na baadhi ya Wizara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, majengo yale hayaingiliani na shughuli zozote za elimu pale *UDOM*. Nawahakikishia Watanzania wote, nazipongeza Wizara hizo kwa kuyalinda kwa kuyatumia majengo hayo… *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Peleka mtoto wako...

**MBUNGE FULANI:** Peleka na binti yako…

**MBUNGE FULANI:** Hizo bangi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Serikali itaendelea kuongeza…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Peleka mtoto wako wa kike pale basi, mbona humpeleki?

**MWENYEKITI:** Jamani naomba heshima na utulivu Bungeni, tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** Wavuta bangi, wavuta bangi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Uhamiaji wa Serikali Dodoma upo palepale! *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Peleka mwanao…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tafadhali tuwe na uvumilivu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Peoples! (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu tafadhali…

**MBUNGE FULANI:** *Peoples!*

**MWENYEKITI:** Jamani tunaendelea. Siyo vibaya Waheshimiwa Wabunge na nyie mkahamia mmoja mmoja Dodoma ili mambo yawe mazuri zaidi. Tunaendelea na Mheshimiwa Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza, naishukuru Wizara ya Elimu iliweza kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Ualimu pale Korogwe ambapo kilileta wanachuo karibu 800 na kitu kwa ajili ya mafunzo pale. Hata hivyo, naiomba Serikali, kwa kuwa chuo kile kina maktaba ndogo na sisi wananchi tumeweza kujenga maktaba kubwa ambayo ingeweza kuwasaidia wanachuo ambao ni wengi sasa pale chuoni, pamoja na wananchi wa Korogwe kwa ujumla: Je, Serikali itakuwa tayari kutupa fedha ili tuweze kukamilisha lile jengo la maktaba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Chatanda kwa kufuatilia masuala ya kielimu na Mheshimiwa Mbunge anapofanya jitihada kama hizo sisi Serikali tunao wajibu wa kusaidia. Kwa hiyo, tutachukua hilo jukumu la kusaidiana nao kuhakikisha maktaba hiyo inakamilika vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Saddiq

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nami naomba niulize swali dogo la nyongeza kuhusu Chuo Kikuu cha Mzumbe. Kwa kuwa Serikali inaongeza wanafunzi kila mwaka; na kwa kuwa kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipokuja Mzumbe kwamba Serikali itatoa fedha kwa ajili ya Ofisi za Walimu na nyumba za wafanyakazi; na kwa kuwa ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne pamoja na kuongeza nyumba za watumishi pale *main campus* Mzumbe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo ilielezwa hapo awali, niseme tu kwamba katika Vyuo Vikuu ambavyo vina kipaumbele katika uongezaji wa miundombinu kwa mwaka huu unaokuja wa fedha 2017/2018 ni pamoja na Chuo Kikuu cha Mzumbe. Kwa hiyo, naomba ajue hilo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na sasa namkaribisha Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 23

**Sheria ya Kuzuia Walanguzi Kununua Mazao Shambani**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Serikali inatakiwa kuweka mkakati wa kuhakikisha mazao yanauzwa katika vituo maalum vinavyotambuliwa ili kuzuia walanguzi kufuata mazao shambani na kununua kwa bei ndogo:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutunga sheria kuzuia walanguzi kwenda kununua mazao shambani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna umuhimu wa kutungwa Sheria ya Kuzuia Walanguzi kwenda kununua mazao ya wakulima mashambani. Aidha, kutokana na umuhimu huo, Serikali imeweka sheria ya kuzuia kununua mazao yakiwa mashambani kwa mazao yote yanayosimamiwa na Bodi za Mazao. Mazao hayo ni kahawa, chai, pareto, pamba, korosho, mkonge na tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Wilaya zimepewa mamlaka kamili ya kutunga sheria ndogo *(bylaws)* au kuweka kanuni na taratibu zinazofaa za kuuza mazao ya wakulima katika vituo vilivyowekwa na Halmashauri hizo. Vituo hivyo ni pamoja na magulio na minada, ambapo mazao mbalimbali ya wakulima na wafugaji huuzwa kwa ushindani na kwa kutumia vipimo rasmi. Vituo Maalum vya kununua mazao vinawezesha kusimamia ubora na kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imefanya marekebisho ya Sheria ya Vipimo kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments)(No. 3)* uliopitishwa na Bunge hili mwezi Novemba, 2016. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, itawezesha Halmashauri kutunga sheria ndogo za usimamizi wa vipimo kwa kuhakikisha kila kijiji kinaaanzisha vituo vya kuuza mazao na kusimamia matumizi ya vipimo rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna umuhimu wa kuwa na sheria hii na pia imesema imetunga sheria kwa ajili ya mazao yale yanayosimamiwa na bodi ya mazao: Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kufanya marekebisho katika sheria hiyo ili hata mazao mengine mchanganyiko yaweze kulindwa ili wakulima waweze kufanikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; ni wazi kwamba bado ulanguzi wa mazao unaendelea, walanguzi wanafuata wakulima mashambani na siyo sahihi kusema kwamba magulio ni sehemu ya ushindani wa bei na Halmashauri zenyewe hazijawa na mkakati maalum wa kuweza kuunda sehemu za kuuzia mazao na kuweza kuzisimamia…

**MWENYEKITI:** Swali tafadhali.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inachukua hatua zipi kuhakikisha kwamba vituo hivi vinakuwepo na vinakuwa na usimamizi ili wakulima waweze kunufaika kwa kupata bei nzuri kuweza kubadilisha maisha yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama ambavyo nimeeeleza katika jibu la swali la msingi kwamba Serikali inaona umuhimu wa kuanzisha sheria.

Kwa hiyo, ombi lake tumelipokea na Serikali imeshaonesha nia kwamba hilo inalishughulikia na imeshaanza kufanya kwa mazao hayo mengine. Kwa maana nyingine tutaendelea kushughulikia na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kule kwetu Namtumbo magulio kwa kweli huwa yanaleta ushindani. Kwa hiyo, naungana kabisa na jibu la msingi kwamba Halmashauri waimarishe magulio na sehemu za minada kwa kweli maeneo hayo yanaleta ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna njia nyingine kutokana na mazao mbalimbali mengine, tuwasiliane na Halmashauri hizo na sisi ni wajumbe wa Halmashauri, tuweze kuboresha kanuni zetu, *bylaws* zetu, ili tuhakikishe mkulima anapata haki yake kwa jasho analolitoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Tutakuwa na swali la msingi na swali moja la nyongeza kwa mwuliza swali. Tunaendelea na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Hitaji la Kupanua Daraja la Mto Wami**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Serikali inajitahidi kujenga na kuimarisha madaraja ili kuondoa kero na kupunguza maafa; Daraja la Mto Wami lililopo barabara ya Tanga ni jembamba sana kiasi kwamba magari mawili hayawezi kupishana kwa wakati mmoja:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipanua daraja hilo la Mto Wami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa Daraja la Wami katika barabara ya Chalinze – Segera ni kiungo muhimu kati ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Mikoa ya Kaskazini mwa Tanzania. Daraja lililopo sasa ambalo ni jembamba lilijengwa miaka mingi, hivyo halikidhi mahitaji ya magari yanayopita kwenye barabara hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa daraja hili katika kukuza uchumi wa nchi, Serikali kupitia *TANROADS* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hili. Zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja jipya la Mto Wami zitaitishwa mwezi Februari, mwaka 2017. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Jadi.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya nyongeza, ninayo maswali mawili. Kwa kuwa Serikali inaitisha zabuni mwezi wa Februari kama ilivyosema na imetenga shilingi bilioni tatu kwa mwaka wa fedha 2016/2017: Je, Serikali haioni kuwa ni muda mfupi unaobakia mpaka kumalizika bajeti? Je, daraja hilo kweli litajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili: Je, Serikali haioni kuchelewesha kujenga daraja hilo ni kuzorotesha maendeleo na kuongezeka kwa ajali na hicho ndiyo kilio cha watu wa Tanga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumhakikishia Mheshimiwa Jadi Kadika kwamba huo muda unatosha sana. Taratibu ni lazima zifuatwe kabla ujenzi haujaanza. Kwa hiyo, hatua za kwanza zilikuwa ni kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hatimaye kuandaa nyaraka za zabuni, kazi hiyo tumeikamilisha. Sasa mwezi wa Pili, tunaitisha tenda na mambo yakikamilika tukampata mkandarasi, hiyo shilingi bilioni tatu itatoka na kazi ya ujenzi itaanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 25

**Ujenzi wa Barabara ya *TAMCO* - Mapinga**

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Barabara ya *TAMCO* hadi Mapinga katika Mji wa Kibaha, Mkoani Pwani imekuwa kwenye maandalizi ya kujengwa kwa kiwango cha lami kwa takriban miaka kumi (10) sasa:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo kwa lami.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *TAMCO* hadi Mapinga yenye urefu wa kilometa 23 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania kupitia Ofisi ya Meneja wa Mkoa wa Pwani. Ili kujenga kwa kiwango cha lami, barabara ya *TAMCO* hadi Mapinga kupitia Vikawe kuunganisha na barabara ya Bagamoyo, Serikali imefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo, hadi sasa tayari ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa moja kuanzia njia panda ya *TAMCO* umekamilika kwa kuwa eneo hili halikuwa na tatizo la ulipaji wa fidia. Eneo lote lililobaki katika barabara hii linahitaji kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa barabara hiyo. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha za kulipa fidia kabla ya kuendelea na ujenzi wa barabara sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 22.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silverstry, swali la nyongeza.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Wananchi wa Kata ya Tangini na Pangani ambapo ndiko barabara hii inapita, wamekuwa wakipata adha kubwa sana. Takriban zaidi ya miaka mitano iliyopita upembuzi yakinifu, usanifu pamoja na tathmini kwa maana ya *evaluation* ilishafanyika na wananchi hawa wanadai kiasi cha fidia ya shilingi

8,552,777,000/= na hadi leo hawajapata fidia hiyo na hawajui wataipata lini. Mbali na hili jitihada za…

**MWENYEKITI:** Naomba swali la nyongeza kwa ufupi tafadhali.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** *Yah.* Jitihada za *RCC* kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii zimekwama kwa sababu ya fidia hii haijalipwa. Je, Serikali italipa lini fidia hii kupisha maendeleo ya barabara hii kwa wananchi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sasa barabara hii imezuiwa kupitisha magari zaidi ya tani 10: Je, *TANROADS* ina mpango gani wa kurekebisha barabara hii ili shughuli za kiuchumi za wananchi hawa ziweze kufanyika kwa kupitisha magari ambayo ni zaidi ya tani 10?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Koka kwamba mara tutakapopata hizo shilingi bilioni 8.65 tutazitoa na kuanza kulipa fidia. Lini? Kama nilivyosema katika jibu la msingi, tunazitafuta hizo fedha na mara tutakapopata tutazilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kitu kimoja; anafahamu kwamba barabara hii ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020, nimhakikishie, tuliahidi na tutatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuiwezesha barabara hii ibebe magari ya zaidi ya tani 10, nimelipokea, nitawasiliana na Meneja wa *TANROADS* Mkoa tuone nini kifanyike ili ombi la Mheshimiwa Mbunge, ambapo ni mahitaji ya wananchi wake hasa wa Kata za Tangini na Pangani waweze nao kupata unafuu kiuchumi. Namwomba tu, kama anaweza kuharakisha, kama hawa wananchi wanaweza wakasamehe hiyo shilingi bilioni nane, nimhakikishie mwezi ujao tutaanza kujenga.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii; na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Norman Sigalla King, Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza swali langu la msingi, niombe kuwapa pole wananchi wa Kata ya Isapulano kwa maafa yaliyowakumba siku chache zilizopita ambapo kimbunga kiliezua nyumba karibu 16. Sasa naomba swali langu lipatiwe majibu.

Na. 26

**Kuboresha Miundombinu ya Hifadhi ya Kitulo**

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING** aliuliza:-

Hifadhi ya Kitulo ni muhimu sana kwa Taifa lakini mpaka sasa *TANAPA* haijaweka miundombinu ya hoteli na barabara ili kuwezesha watalii wanaokwenda Kitulo wawe na mahali pa kukaa:-

(a) Je, ni lini Serikali itawezesha ujenzi wa hoteli ya kitalii katika Tarafa ya Matamba?

(b) Je, ni lini Serikali itawezesha ujenzi wa barabara ya Chimala – Matamba – Kitulo ili kuinua utalii katika Hifadhi ya Kitulo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Kitulo inasimamiwa kwa kufuata mpango wa jumla *(General Management Plan)* wa miaka 10 ulioandaliwa mwaka 2008. Mpango huo umetoa fursa ya kujenga *lodge* ya vitanda 50 ndani ya hifadhi. Kulingana na taratibu za Hifadhi za Taifa, ujenzi wa huduma za malazi ya aina hiyo hufanywa na sekta binafsi. Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika kutangaza fursa za utalii, hivyo kuvutia uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu ya hoteli ili kuboresha shughuli za utalii katika eneo la magharibi na kusini mwa Tanzania ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Chimala – Matanda – Kitulo ni sehemu ya mipango ya Serikali ya kuendeleza na kusimamia miundombinu inayoelekea kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili kuweka kipaumbele katika ujenzi wa barabara zinazoelekea kwenye maeneo

yenye vivutio vya utalii zikiwemo za Chimala – Matamba – Kitulo ambayo ni muhimu kwa Hifadhi ya Kitulo, lakini vilevile Iringa – Tungamalenga – Ruaha mahsusi na muhimu kwa Hifadhi ya Ruaha na nyinginezo kwa kiwango cha lami ili kuchochea maendeleo ya utalii.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa majibu kama haya yasije yakarudiwa mwakani. Kwanza, nini kauli ya Serikali kufanya *commitment* ya ujenzi hasa wa barabara hii? Kwa sababu nafahamu Hifadhi za Ngorongoro, Manyara na Serengeti zina sifa kubwa kwa sababu ya miundombinu kuwa imeboreshwa na hasa ya barabara.

Pili, sambamba na hilo, Pori la Mpanga Kipengere, mipaka imerekebishwa kiasi kwamba inaumiza Kata za Ikuo, Kigala, Mfumbi, hivyo kusumbua wananchi kiasi kwamba hakuna hata eneo la kujenga miundombinu. Nini kauli ya Serikali kuhusu hili? Kwa sababu upande wa TAMISEMI najua wameshalishughulikia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Profesa Norman King juu ya uwepo wa uwezekano wa kurudiwa kwa jibu nililolitoa leo. Nia njema ya Serikali kwanza ni kuhakikisha kwamba Hifadhi ya Kitulo inaboresha au Serikali inaboresha utalii kwenye Hifadhi ya Kitulo, siyo kwa faida ya Kitulo peke yake na wananchi wa Kata tulizozitaja na Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, lakini pia kwa ajili ya Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Kitulo tunaiboresha kwanza kwa kuboresha miundombinu ya ndani ambako tayari tumeboresha barabara za ndani na mageti ya kuingia ndani ya hifadhi, nyumba za wafanyakazi pamoja na ofisi. Pia tumeboresha upatikanaji wa bidhaa za utalii. Kwa sasa hivi hifadhi hii ni maarufu kwa ajili ya maua na hali ya miinuko *(terrain)* ya pale na hali ya hewa ambayo inafanana tu na nchi nyingine za Ulaya tofauti na hapa kwa maana ya baridi ya muda mrefu na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tayari tunataka kurudisha wanyama ambao walikuwepo zamani lakini baadaye kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ujangili, wanyama hao wametoweka. Sasa tuna mpango

wa kurudisha tena wanyama wakiwemo pundamilia, swala na nyumbu ili kuweza kuifanya hifadhi hii iweze kupanda hadhi, tuweze kupata watalii zaidi, ambayo itachangia kwa kiasi kikubwa kukuza utalii kwenye eneo la kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba ni nia ya Serikali na kwa kweli tumepania kuweza kupandisha hadhi ya utalii, siyo kwa Kitulo peke yake, bali kwa utalii wa eneo la Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili; Mpanga Kipengere ni mojawapo ya maeneo ambayo tuna migogoro ya mipaka, lakini nataka kusema kwamba kama ilivyo kwa maeneo mengine kadhaa ambayo tumekwisha yaorodhesha, yanaendelea kushughulikiwa na Tume Maalum ya Serikali ambayo tumeiunda ya kushughulikia migogoro ya namna hii. Nafikiri tuwape muda mfupi tu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ilipata changamoto mbalimbali, mojawapo ikiwa ni ya kifedha, lakini sasa hivi tumetatua changamoto hiyo ya kifedha, wapo kazini na wanakwenda kwa kasi ili kuweza kutatua migogoro inayofanana na huu ambao uko pale Mpanga Kipengere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ziada tu namwomba Mheshimiwa Mbunge, baada ya *session* hii nikutane naye ili niweze kupata *details* za *status* ya Mpanga Kipengere ili niweze kuwashauri wale ambao wanaendelea na kazi hii kwa maana ya Kamati ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda, tutaendelea na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, naomba sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Wananchi Kupewa Vibali vya Kuvua Samaki Ndani ya Hifadhi**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

Sheria zinatoa ridhaa kwa watu kuwinda ndani ya hifadhi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kutoa ridhaa kwa wananchi waishio maeneo ya hifadhi kupata ruhusa kisheria ili kuweza kuvua samaki ndani ya mabwawa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kwa wanakijiji waishio maeneo ya hifadhi hususan Kata za Mwaseni, Mloka na nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 wananchi wa Kata za Mwaseni, Mloka, Ngoroko na Kipungila Wilayani Rufiji waliruhusiwa kuingia ndani ya Pori la Akiba Selous na kuvua samaki. Hata hivyo, baadhi ya wanavijiji walikiuka taratibu zilizokuwa zimewekwa kwa kuingia ndani ya hifadhi bila kujiandikisha na kuvua samaki kinyume cha sheria. Aidha, baadhi yao walibainika kujihusisha na vitendo vya ujangili wa wanyamapori kama vile utoaji wa taarifa za mwenendo wa doria na uwindaji wa wanyamapori, uvuvi haramu wa kutumia sumu, ukataji miti ovyo kwa ajili ya kukaushia samaki na kutengeneza mitumbwi na uharibifu wa mazingira kutokana na uchomaji wa moto ovyo kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali ya usalama katika maeneo ya uhifadhi ya wanyamapori, kwa sasa Wizara yangu itaendelea kutoruhusu uvuvi kufanyika ndani ya Pori la Akiba Selous. Hata hivyo, Wizara yangu inawashauri wananchi wa Kata za Mwaseni, Mloka na nyinginezo zilizo jirani kutumia mabwawa mengineyo yaliyopo nje ya pori yenye fursa kubwa ya kufanya shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mabwawa hayo ni Zumbi katika Vijiji vya Nyaminywili, Kipugira na Kipo, Bwawa la Ruwe karibu na Mkongo, Bwawa la Lugongo katika Kijiji cha Mtanza na Bwawa la Zimbwini katika Mji wa Kibiti.

Mabwawa hayo na Mto Rufiji vinatoa fursa ya shughuli za uvuvi, hivyo kusaidia kuinua kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mahitaji ya wananchi katika maeneo haya, ya kufanya kazi na kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Wizara yangu inaendelea kushauriana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kuhusu namna ya kutekeleza mpango wa kuwajengea mabwawa ya samaki ili pamoja na mabwawa ya asili yaliyopo yawawezeshe kufanya shughuli za uvuvi endelevu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mchengerwa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi waliokuwa na umri wa kuelewa mambo, mwaka 1956 Mwalimu Nyerere aliahidi ujenzi wa Bwawa la *Stiegler's Gorge* ili kuweza kutatua tatizo la umeme. Bwawa hili lingejengwa pale katika Kata ya Mwaseni. Ahadi hii ina miaka 61.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu kama ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri aliyotuahidi hapa ujenzi wa mabwawa katika Kata za Mwaseni, Kipugira, Kilimani pamoja na Mkongo itachukua pia miaka 61 au itakuwa muda mfupi kidogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Wizara ya Maliasili na Utalii inachangia pato la Taifa asilimia 19 na Rufiji yetu iko ndani ya hifadhi kwa zaidi ya nusu ya Rufiji, yaani *square kilometer* 6,500 ipo ndani ya hifadhi ya Maliasili na Utalii. Naomba kufahamu, mchakato wa ujenzi wa vyoo katika eneo la Selous pale Rufiji, leo hii watalii wanajisaidia katika maeneo ya hifadhi bila kuwa na vyoo. Naomba kufahamu, hili pato la Taifa mgawanyo wake ukoje katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii ili kuweza kusaidia wanyama hawa ambao wapo ndani ya hifadhi ikizingatia kwamba watalii wetu leo hii wanajisaidia sehemu ambazo ni za wazi bila kujisaidia eneo la vyoo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza la wasiwasi au mashaka ya kwamba pengine hata ahadi hii tuliyoitoa hapa inaweza ikachukua muda mrefu ule alioutaja zaidi ya miaka 60 akifananisha na suala la mradi wa *Stiegler's Gorge;* kwanza nataka tu nimpe taarifa kwamba mradi wa *Stiegler's Gorge* akileta swali ambalo ni mahsusi kwa

mujibu wa Kanuni za Bunge litajibiwa vizuri sana na Wizara ya Maji kwa sababu lina majibu sahihi kabisa na mahsusi ya kwa nini imechukua muda mrefu kiasi hicho kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na majibu haya ya utekelezaji wa ujenzi wa mabwawa matano; kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwamba hivi ninavyozungumza, kutokana na jitihada zake, wananchi wa Jimbo lake wanaelekea kupata majawabu ya changamoto kubwa hii ya kupata maeneo ya uvuvi hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi karibuni kwa sababu ninavyozungumza sasa hivi tayari mawasiliano yameshafanyika kati ya Wizara yangu na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Tumeshabadilishana uzoefu na taarifa na tayari tuna makisio ya awali ya gharama za ujenzi wa mabwawa hayo matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na kiwango cha fedha kile ambacho tumekiona katika hatua za awali, tunafanya mapitio ili tujue ukubwa wa mabwawa yale lakini pia tujue namna ya kuyajenga ili kuweza kutumia gharama ambazo zitakuwa zina unafuu, lakini bado tufikie malengo ya kuweza kuwapatia mabwawa hayo wananchi.

Kwa hiyo, wananchi wa Rufiji wasiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Mchengerwa anawapigania na watapata maeneo ya kuvua samaki mbadala nje ya Hifadhi ya Selous. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili; ni kweli utalii unachangia asilimia zaidi ya 17 katika pato la Taifa; lakini pia niongeze kwamba robo ya upatikanaji wa fedha za kigeni katika muda wa miaka mitatu mfululizo lilitokana na pato linalotokana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto aliyoisema ya eneo la maingilio ndani ya hifadhi, changamoto ambayo inaleta usumbufu kwa watalii, nataka kusema kwamba changamoto hii imeshamalizika kwa sababu tayari ni miongoni mwa mambo ambayo tumeyapa kipaumbele hivi karibuni, yale ambayo tunatakiwa kuyashughulikia kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua unapokuwa na changamoto kuna nyingine ni kubwa sana zinahitaji labda jitihada kubwa na rasilimali nyingi, lakini hizi nyingine ndogo ndogo kama hii, hizi ni *quick wins,* kwa hiyo, tunazifanyia

utaratibu wa haraka. Nataka nimhakikishie kwamba kabla mwaka huu haujakwisha, tutakuwa tumetatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Sasa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Namkaribisha Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 28

**Kuvuta Maji Kutoka Ziwa Tanganyika**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta mradi wa maji Ziwa Tanganyika ili maji yaweze kuvutwa mpaka Mpanda na Mkoa wa jirani wa Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuweza kutatua changamoto za upatikanaji wa maji nchini. Hatua zinazochukuliwa kutatua changamoto ya maji katika Mikoa ya Rukwa na Katavi zimegawanyika katika mipango ya muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mfupi, Serikali imekamilisha usanifu na uandaaji wa kabrasha za zabuni kwa ajili ya mradi wa maji kwa Mji wa Inyonga Mkoa wa Katavi, Miji ya Chala, Laela, Namanyere na Matai katika Mkoa wa Rukwa.

Katika usanifu huo, vyanzo mbalimbali vimeainishwa vikiwemo mabwawa, chemchemi na visima virefu. Aidha, kwa Mji wa Mpanda, Serikali imetekeleza mradi wa maji wa Ikolongo wenye thamani ya shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kuboresha hali ya huduma ya maji Mjini Mpanda. Mradi huu umekamilika mwezi Julai mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, Serikali imejielekeza katika kutumia vyanzo vya maji vya Ziwa Tanganyika na mito mikubwa kwa ajili ya kuhudumia Miji ya Mpanda na Sumbawanga, Miji mingine pamoja na vijiji vitakavyokuwa kando kando ya Bomba kuu. Hivyo Wizara imeziagiza Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda na Sumbawanga kufanya tathmini ya awali na kuiwasilisha Wizarani ili kuweza kuajiri wataalam washauri watakaofanya usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Majisafi Sumbawanga wameshaandaa andiko hilo na Mamlaka ya Majisafi Mpanda pia nao wameandaa andiko hilo ambalo linawasilishwa mwezi Februari mwaka 2017. Kazi ya usanifu itaanza wakati wa utekelezaji wa programu ya maendeleo ya Sekta ya Maji, Awamu ya Pili iliyoanza Julai, 2016.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska kama una swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mradi wa maji wa Ikorongo umeshindwa kutosheleza mahitaji ya wananchi wa Wilaya ya Mpanda; Kuna vijiji 20 vilivyoko Wilaya ya Nsimbo havina maji; kuna vijiji 13 na vitongoji viwili vilivyoko pale Mpanda Mjini havina maji; kuna vijiji tisa vilivyoko Wilaya ya Tanganyika, havina maji. Je, Serikali ni lini itachimba visima kwenye vijiji hivi na Kata hizi ili imtue ndoo mwanamke wa Mkoa wa Katavi?

Swali la pili; Mradi wa kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika ni programu ya muda mrefu ambayo haiwezi ikatekelezwa leo au kesho na wananchi na akinamama wa Mkoa wa Katavi wanaendelea kuteseka: Je, Waziri anaweza akatueleza hiyo programu ya kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika itaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwamba mradi wa Ikorongo haujitoshelezi, ni kweli. Mradi wa Ikorongo unatoa lita milioni 3.5 kwa siku wakati mahitaji ya Mji wa Mpanda pekee ni lita milioni 11 kwa siku. Kwa hiyo, kuna upungufu mkubwa. Wakati tunasubiri huu mpango wa muda mrefu, tumeendelea na uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali ya vijiji ambavyo amevitaja. Kwa mfano, tayari tumeshachimba visima katika Halmashauri ya Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaendelea kuchimba visima katika Halmashauri ya Mpimbwe na tayari tumechimba visima katika Halmashauri ya Mlele na Halmashauri ya Tanganyika, sasa hivi tunaendelea kufanya mazungumzo nao ili tuweze kupeleka fedha kwa ajili ya kuchimba visima ikiwa ni hatua ya muda mfupi.

Swali la pili; Mpango huu wa muda mrefu unaanza lini? Mpango huu unaanza katika mwaka wa fedha 2017/2018. Tumeshapokea maandiko tayari, kwa hiyo, katika bajeti inayokuja, tuombe tu Mheshimiwa Mbunge na wewe upitishe hiyo bajeti ili tuweze kuweka Mhandisi mshauri aweze kusanifu ili kuandaa Makabrasha ya Zabuni ya kutoa maji kutoka Karema katika Ziwa Tanganyika kuleta Mji wa Mpanda na kutoa maji upande wa Sumbawanga kuleta Mji wa Sumbawanga kutoka kule Kasanga.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Namkaribisha Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, aulize swali lake.

Na. 29

**Ukosefu wa Maji Mji wa Bagamoyo**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la ukosefu wa maji safi na salama katika Mji Mkongwe wa Bagamoyo katika Kata za Magomeni na Dunda:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa Mji Mkongwe Bagamoyo maji kwa kiwango cha kuridhisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mji Mkongwe wa Bagamoyo katika Kata ya Magomeni na Dunda wanapata huduma ya maji ya mgao kutoka katika chanzo cha Ruvu Chini.

Tangu tarehe 23 Machi, 2016 Serikali ilikamilisha upanuzi wa chanzo hicho na ujenzi wa bomba kuu kutoka Ruvu Chini hadi matanki yaliyoko Makongo eneo la Chuo cha Ardhi, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuwezesha wananchi hao kupata huduma ya maji kwa uhakika, Serikali tayari imemwajiri Mkandarasi anayejulikana kwa jina la *Jain Irrigation System* kwa kazi ya kujenga tanki kubwa Bagamoyo Mjini. Ataweka mabomba ya kutoa maji kutoka bomba kuu na kuyaleta kwenye Tanki na atalaza Mabomba ya kusambaza maji kwa wananchi katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na Kata ya Magomeni na Dunda. Kazi hii imeanza mwezi Machi, 2016 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Moja, kwa vile Waziri amekiri kwamba maji yanapatikana kwa mgao: Je, Waziri atakuwa tayari kuiagiza *DAWASCO* ili iiondoe hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo katika utaratibu wa mgao ili kuweza kuboresha huduma ya afya katika hospitali hii ya Wilaya?

Swali la pili; je, mradi huo wa usambazaji mabomba utajumuisha kata zote tisa za Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa nikuhakikishie, baada ya mradi huu kukamilika mwezi Juni, 2017 Hospitali ya Bagamoyo haitakuwa na matatizo ya maji tena. Katika Mkataba unaoendelea, suala hili limeainishwa kuhakikisha kwamba Hospitali ya Bagamoyo isiwe na matatizo ya maji tena.

Swali la pili; mpango huu ukikamilika Mheshimiwa Kawambwa ni kwamba Kata zote tisa za Jimbo lako Bagamoyo zitapata huduma ya maji kutokana na mradi huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Kutokana na muda tunamalizia na Mheshimiwa Halima James Mdee, aulize swali lake.

Na. 30

**Tatizo la Maji Baadhi ya Maeneo ya Jimbo la Kawe**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Jimbo la Kawe ni miongoni mwa Majimbo ambayo (baadhi ya maeneo) yamekuwa yanakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa maji safi na salama kwa kipindi kirefu ambayo ni Kata ya Mabwepande (Mtaa wa Mbopo, Mabwepande na Kinondo), Kata ya Makongo (Mtaa wa Changanyikeni na baadhi ya maeneo ya Mtaa wa Makongo Juu), Kata ya Wazo, Mbweni na Mbezi Juu; na changamoto hii sugu ilitarajiwa kupungua na kumalizika kabisa baada ya mradi mkubwa wa maji wa Ruvu chini kukamilika ambao kwa sasa tayari umeshakamilika:-

(a) Je, mikakati ya usambazaji maji pamoja na Mabomba (katika maeneo ambayo hayana mtandao wa mabomba) ikoje ili kutatua kero husika?

(b) Je, ni miradi gani inayotarajiwa kutekelezwa, muda wa utekelezaji, gharama za kila mradi na nani anayewajibika katika utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa maji wa Ruvu Chini umekamilika na umeanza kutumika rasmi tarehe 23 mwezi Machi, 2016. Mradi huu ulihusu upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini na ujenzi wa Bomba kuu kutoka Ruvu Chini kwenda Dar es Salaam. Hivi sasa uzalishaji wa maji kutoka Ruvu Chini ni mita za ujazo milioni 270 kwa siku ikiwa ni ongezeko la mita za ujazo milioni 90 kwa siku. Kutokana na kukamilika kwa mradi huu, kumekuwa na ongezeko la upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa hayapati maji licha ya kuwa na mabomba ya *DAWASCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza, Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji na usambazaji wa maji unaogharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni 32.772 kutoka Benki ya *Exim*-India. Katika Jimbo la Kawe la Mheshimiwa Mbunge, mradi huu utatekelezwa katika maeneo ya Changanyikeni, Makongo, Salasala, Wazo, Tegeta, Ununio, Bunju na Mabwepande. Kazi zitakazofanyika ni

pamoja na ujenzi wa kituo cha kusukumia maji katika Kata ya Mabwepande na matanki ya kuhifadhia maji katika Kata za Makongo na Wazo pamoja na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa kwa muda wa miezi 15 chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam *(DAWASA)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye (b) ya swali langu niliuliza, ni miradi gani inayotarajia kutekelezwa, muda wa utekelezaji, gharama za kila mradi na nani anayewajibika katika utekelezaji? Sasa majibu ya Serikali hayajanielezea mradi, ila ameelezea maeneo ambayo mradi utatekelezwa. Sasa nataka niambiwe katika maeneo haya ambayo miradi itatekelezwa, kuna miradi gani *specifically,* kuna Kampuni gani *specifically?* Hilo la kwanza.

La pili, zimetajwa dola bilioni 32, nami nilivyouliza swali, nilikuwa nataka nijue gharama za kila mradi kwenye Jimbo langu. Sasa swali langu la pili: Je, hizi bilioni 32 ndiyo zote zinaenda kwenye mradi wa Jimbo la Kawe na kama siyo, nataka nijue Jimbo la Kawe *specifically* katika hii dola bilioni 32 mgao wake ni kiasi gani na kwa miradi ipi? Nadhani nimeeleweka.

**MWENYEKITI:** Imetosha, maswali mawili tayari.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Swali langu nataka uchambuzi ili wananchi wangu wanaosikia kila mmoja ajue kwake anastahiki gani. Sasa Serikali ikinipa kiujumla jumla nitashindwa kuja kuwabana.

**MWENYEKITI:** Imeeleweka Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa hiyo, nataka uchambue, siyo unajibu kiujumla jumla.

**MWENYEKITI:** Imeeleweka. Mheshimiwa Waziri mwenyewe, majibu kwa ufupi tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa katika jibu la msingi, tumeshasema mradi ambao unaendelea, Mkandarasi anaitwa *Jain Irrigation Company* na tumesema gharama ya mradi ni *US Dollar* milioni 32. Tunapokuwa tunapanga miradi, huwa hatupangi Kijimbo. Tunapanga mradi kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na sehemu kubwa ya…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Huo ni wa Bagamoyo, siyo wa huku.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** ...na sehemu kubwa ya mradi huu uko kwenye Jimbo lake.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hapa hujasema Mzee.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Ndiyo maana tumetaja hayo maeneo ya Kawe, Mabwepande, yote yote yako kwenye Jimbo la Kawe. Kwa hiyo, tumelijibu kikamilifu kama alivyouliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu yake ya pili alikuwa anataka kujua kama hizo *US Dollar* milioni 32 ni kwa Jimbo la Kawe tu peke yake? Hapana, siyo kwa Jimbo la Kawe peke yake, ni pamoja na bomba kubwa ambalo litaenda baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Bagamoyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Muda wetu wa maswali umemalizika. Mheshimiwa Halima, naomba uzime *microphone*.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi cha maswali na hapa nina matangazo kama matatu tu. Kwanza ni matangazo ya wageni. Leo tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Nachukua fursa hii kuwakaribisha sana katika Bunge letu, karibuni sana.

Kuna tangazo la Mheshimiwa Dkt. Marry Nagu, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa leo tarehe Mosi mwezi wa Pili saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 227 ulioko jengo la utawala ghorofa ya pili.

Tangazo la pili ni la Mheshimiwa Cecilia Paresso, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wakristo Wakatoliki, kwamba leo tarehe 1 Februari, 2017 kutakuwa na ibada ya Misa mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge

saa 7.00 mchana katika Kanisa dogo lililopo ghorofa ya pili Ukumbi wa Msekwa. Wabunge wengine Wakristo mnakaribishwa kushiriki ibada hii takatifu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Dkt. Macha na Mheshimiwa Waitara.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya mwongozo. Nasimama kwa kanuni ya 46(1), sitaisoma. Naomba mwongozo wako kuhusu majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri katika swali langu la msingi Na. 17 leo asubuhi kuhusu Vyuo vya Ufundi na Utengemao kwa watu wenye ulemavu ambavyo vimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Vyuo vingi vimefungwa kwa miaka mingi. Kwa mfano, Chuo cha Masasi kimefungwa zaidi ya miaka 10. Sasa hivi madirisha, milango vyote vimetolewa. Tukija Chuo cha Tabora, kimefungwa zaidi ya miaka 10 na tulitumia pesa nyingi sana kutoka kwa Wafadhili wa Serikali ya Sweden kukikarabati.

Hali kadhalika, Chuo cha Mbeya, Mwanza, Chuo cha Masiwani kimefungwa na kuna wafanyakazi wanakwenda pale wanalipwa mshahara lakini hakuna wanafunzi. Wakati Serikali inajitahidi kufungua *VETA,* Vyuo vya Ufundi, kuongeza mafunzo ya ufundi kwa Watanzania, lakini Vyuo vya Watu wenye Ulemavu vinafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mfano. Sikutakii hivyo, lakini kwa bahati mbaya, wewe ukipoteza *sight* leo, utahitaji *rehabilitation,* utahitaji *new skills* ili uweze kupambana na maisha.

Sasa hivi pia kuna ajali nyingi sana za bodaboda watu wanakatika mikono, miguu, migongo, wanatakiwa wapatiwe *rehabilitations,* wapatiwe *new skills* waweze kupambana na maisha. Hivi Vyuo ndiyo vilikuwa vinafanya mambo kama hayo, sasa vimefungwa na sababu zilizotolewa hazikuniridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako na nataka kujua ni *concrete action* gani zimechukuliwa na vitafunguliwa lini? Kwa sababu mahitaji

ni makubwa na walemavu wanazihitaji hizo huduma za *rehabilitation* pamoja na *skills.* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Naomba nitumie kanuni ya 68(7). Leo asubuhi niliwahi sana hapa nikawa naangalia *television* ya Taifa *(TBC1)* sasa nikamwona Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili amevaa kijeshi, ni *Brigadier* Milanzi, amevaa kijeshi na akawa anafanya kazi zake za kiongozi kama Katibu Mkuu wa Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi pia nilimwona Mkuu wa Wilaya nadhani Kakonko akiwa anakutana na wakimbizi kule, lakini pia anapata taarifa za wale Maafisa Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Katiba, Ibara ya 147 pamoja na mambo mengine, inapiga marufuku Wanajeshi kuwa Wanasiasa na tunajua uteuzi uliofanyika wa Makatibu Wakuu, Ma-*Ras*, Ma-*Das*, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya sifa mojawapo kubwa ilikuwa ni kuangalia Ukada wake ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako kwa sababu hawa viongozi ambao wanavaa nguo za kijeshi na wanafanya shughuli za kiraia, kama kweli ni kutumikia wananchi, wanawatisha. Huyu ni *Brigadier,* akienda mahali, badala ya kupokea malalamiko, anaanza kupokea *salute* na amri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utusaidie mwongozo wako ili tujue sasa nchi hii inatawaliwa kiraia au ni kijeshi kimya kimya ila hamtangazi hadharani? Naomba mwongozo wako, utusaidie ili tuelewe. Tukikutana na Katibu Mkuu ana viongozi kama hawa tuongee nao kama raia wa kawaida au tuongee nao kama Wanajeshi na wanaweza wakaanza kutupa mateso ambayo kimsingi yanatisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ili tusaidie Watanzania katika utendaji wa nchi hii. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Msigwa, halafu Mheshimiwa Esther.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7), wakati wa kipindi cha maswali na majibu, swali lililoulizwa na

Mheshimiwa Susan Lyimo lilihusiana na jinsi ambavyo Serikali imehamia katika majengo ya Chuo Kikuu Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ametetea kwamba kuna majengo ya kutosha na kwamba hakuna usumbufu wowote ambao wanafunzi wanaupata kwa Serikali kuhamia katika majengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwongozo ninaoutaka kutoka kwako taratibu za elimu kwa mfano haziruhusu watu wanaosoma elimu ya juu kukaa na watu wanaosoma elimu ya chini kwa mfano shule za msingi au sekondari. Sasa je, ni sera ya Chama cha Mapinduzi kwamba inaona ni halali kuchanganya shughuli za Serikali na mahali ambapo ni kitivo cha elimu ambapo tunategemea watu wasome, wajifunze na mimi kwa mtazamo wangu na kwa mtazamo wa walio wengi, kuhamia Dodoma *is more of a political move than an economical move*. Sasa tunataka wanafunzi wasome, wawe katika mazingira mazuri, je ni halali kwa Bunge hili na mwaka jana katika mpango wa Serikali kulikuwa hakuna mahali popote ambapo Serikali iliweka mpango huo wa kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema Serikali imekurupuka, hatukuwa na bajeti ya kuhamia Dodoma, tumezungumza hapa kwamba Serikali imekurupuka kutuleta Dodoma na hii inadhihirisha kwamba Serikali imekurupuka kuja Dodoma sasa inakwenda kuvuruga wanafunzi wanavyosoma. Sasa mwongozo ninaouomba, je, ni Sera ya Chama cha Mapinduzi kwamba wanafunzi wale badala ya ku-*graduate* na A wa-*graduate* na *AIDS* kwa sababu wanakwenda kuchanganyikana na michanganyiko ya watu wengi wanaokwenda kuhamia pale na uzoefu unaonesha…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** CCM ilitoa jengo la Chimwaga kwa nini?

**MWENYEKITI:** Ahaa! Sasa tuheshimiane tafadhali. Naomba uendelee Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. PETER S. MSIGWA:** Uzoefu unaonesha kwamba watu wanapohama kutoka sehemu nyingine kwenda sehemu nyingine huwa wanatangulia wanaume, wake zao wanawaacha na hii inaonesha kwamba wanaenda ku-*disturb* watoto wa shule kule Dodoma. Naomba mwongozo wako, ni kwa nini Serikali imeamua kukurupukia Dodoma na kwenda ku-*disturb* mipango mingine ambayo tulijiwekea katika utaratibu badala ya kufuata utaratibu kwa sababu kuhamia Dodoma sio jambo la dharura na hatukuwa na bajeti nalo, haliko

kwenye mpango. Ni kwa nini Bunge hili libariki mambo ya hovyo ambayo Serikali inafanya. Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI** Umeeleweka. Tumemaliza miongozo? Haya Mheshimiwa Ester Bulaya wa mwisho.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba mwongozo wako, hivi karibuni kumekuwa na utaratibu na sintofahamu katika utungaji wa Sheria. Mara nyingi Wabunge wanapopeleka *amendments* zao kwa ajili ya kuhakikisha tunaisaidia Serikali kutunga Sheria. Kumekuwa na kigezo kwamba wamechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe mfano. Mheshimiwa Susan Lyimo, jana saa tano amepeleka *amendment* kwenye Ofisi ya Katibu, amekataliwa kupokelewa. Hata hivyo, wote tunajua na Waheshimiwa Wabunge ambao mlikuwepo kwamba hata kama yalitolewa maelezo kwamba lazima Mbunge apeleke *amendment* kabla Waziri hajasoma mabadiliko ya Sheria Mbalimbali, tunajua hii Miswada tunaipata mapema hata kama Mbunge unaamua kufanya mabadiliko inawezekana yale mabadiliko yakawa yameshughulikiwa na Kamati husika au Waziri husika. Kwa nia njema ya kuendesha vikao vya Bunge na kuisaidia Serikali katika kuhakikisha tunatunga Sheria bora, ni vyema utaratibu ukarudi kama ulivyo kwa sababu Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86, 88 haijataja hicho kipengele kwamba lazima Mbunge alete *amendment* kabla Waziri hajawasilisha mabadiliko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tunakuwa kama tunaviziana. Lengo letu ni kuisaidia nchi. Kama Mbunge atapewa muda, baada ya kuahirishwa Bunge aidha, saa moja au ile saa saba baada ya Waziri kusoma, baada ya Mwenyekiti wa Kamati kusoma, tayari anajua ni mabadiliko gani yamefanywa na Serikali, mabadiliko gani yamefanywa na Kamati ili yeye ajikite katika yale ambayo hayajafanyiwa mabadiliko. Huo ndio utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao tuliokuwepo nyuma hata Bunge lililopita nakumbuka kuna utaratibu ambao uliwekwa katika *Financing Bill* kwamba baada ya kuwasilisha mabadiliko mbalimbali, Waziri kusoma na Mbunge anaweza akaonana na Kamati baada ya kila kitu kusoma ili kujua ni kitu gani anatakiwa afanyie mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa ajili ya kuisaidia Serikali na kwa ajili ya Bunge kutimiza majukumu yake ya kikanuni, ya kikatiba ya kutunga Sheria, utaratibu ufuatwe ili Mbunge apewe nafasi baada ya Waziri

kusoma, Kamati kuwasilisha hoja na maoni ya Kambi ya Upinzani ili 86(11) na 88 zifuatwe kwa mujibu wa kanuni tulizojiwekea. Huu ni utaratibu mgeni kabisa! Tunakuwa kama tunaviziana wakati lengo ni kujenga nchi yetu moja. Kwa nini tunakaa tunagombania siti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea miongozo minne. Mwongozo wa kwanza wa Mheshimiwa Elly Marco kwa mujibu wa Kanuni ya 68(10) nitautolea majibu baadaye.

Mwongozo ambao ameomba Mheshimiwa Waitara huu siwezi kuutolea mwongozo Bungeni kwa sababu ni suala ambalo halijatokea hapa Bungeni, huo ndiyo mwongozo wangu.

Suala la Mheshimiwa Peter Msigwa, suala hili ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Susan Lyimo, ambalo mimi nasema mwongozo wake ni kwamba jibu la Mheshimiwa Jenista Mhagama limejitosheleza. Kwa kuongezea ni kwamba, sio vibaya hata Waheshimiwa Wabunge tukaanza mmoja mmoja kuhamia Dodoma ili mambo yawe mazuri zaidi. *(Makofi)*

Namalizia na Mheshimiwa Ester Bulaya, mwongozo ambao aliuomba wa kuhusu *schedule of amendment* kuletwa hapa Bungeni. Jibu hili la mwongozo huu lilitolewa jana na Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa hiyo, huo ndiyo mwongozo wangu, nimemaliza, Katibu tuendelee.

**NDG. THEONEST RUHIRABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa (2016) *[The Written Laws Miscellaneous Amendement No. 4 Bill (2016)]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* tafadhali naomba utoe hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Act, 2016)* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali

la Marekebisho sasa usomwe Mara ya Pili; na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu katika Bunge hili. Nakupongeza wewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyoendelea kuliongoza Bunge letu. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali. Pia, nawashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi Dimani. Nawapongeza Mheshimiwa Abdallah Majula Bulembo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Profes Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Wabunge. Nawatakia kila kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ya Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu. Mwisho, nawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ushirikiano kwa njia mbalimbali ikiwemo ushauri, maombi, sala, dua, taarifa muhimu na kadhalika na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.4) Act, 2016)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mbunge wa Rufiji) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kazi nzuri ilifanywa na Kamati hii kwa kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau walioitwa kwenye Kamati hiyo kabla ya kutoa mapendekezo yake kwa Serikali kwa nia ya kuboresha Muswada huu. Ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati hiyo, vimesaidia kuuboresha Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria sita (6). Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa kutumia masharti ya Sheria hizo na pia kuoanisha masharti ya Sheria zinazorekebishwa na masharti yaliyoko katika sheria nyingine zilizopo.

Baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika Muswada huu, ni kubadilisha vifungu vya Sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo-

(1) Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura ya 134; Sheria *(The Government Loans, Guarantees and Grants Act, Cap.134);*

(2) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178 *(The Higher Education Students' Loans Board Act, Cap. 178);*

(3) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 *(The Income Tax Act, Cap. 332);*

(4) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 *(The Land Act, Cap. 113);*

(5) Sheria ya Sukari, Sura ya 251 *(The Sugar Industry Act, Cap.251);* na hatimaye

(6) Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283 *(The Wildlife Conservation Act, Cap. 283)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu saba ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya Utangulizi, ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 *(The Government Loans, Guarantees and Grants Act, Cap.134)*. Ibara ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho ya ujumla kwa kufuta maneno "kutoka

nje ya Tanzania *(from outside Tanzania)* popote yanapojitokeza katika Sheria hiyo na kuweka badala yake maneno "kutoka vyanzo ambayo siyo vya ndani" (*from non-resident sources*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuwa na tafsiri sahihi ya maana ya mikopo kutoka nje kulingana na Miongozo ya *International Monetary Fund* (IMF)/*World Bank/Public Debt Management Guidelines* ambayo kimsingi inatumika katika nchi zote wanachama wa Taasisi hizi. Mwongozo huo unaelekeza kama ifuatavyo; nanukuu:

*"To qualify as external debt, the debt liabilities must be owed by a resident to a non resident. Residence is determined by where the debtor and creditor have their center of predominant economic interest-typically, where they are ordinarily located and-not by their nationality."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha pili kinachotoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria hiyo. Marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza tafsiri ya maneno "Mfuko Mkuu wa Hazina" (*Consolidated Fund)* kuwa ni Mfuko Mkuu wa Hazina ambao umetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri nyingine inayopendekezwa kuongezwa katika kifungu hicho ni ya maneno "*on lending*" ambayo yatamaanisha utaratibu ambapo Serikali hukopa kutoka chanzo cha nje au ndani na kisha kutoa mkopo huo kwa mamlaka nyingine kama vile Shirika la Umma au Serikali za Mitaa na inapobidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho na kwa kuzingatia ushauri wa Kamati, tumependekeza kuongeza tafsiri ya maneno "mkopo mama" yaani *primary loan* na "vyanzo vya ndani" yaani *resident sources* ambayo yametumika katika Sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri ya maneno hayo ili kurahisisha matumizi ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ilivyo sasa inatoa tafsiri kuwa "mkopo wa nje" yaani *foreign loan* ni mkopo ambao Serikali inaupata kutoka nje ya Tanzania na kwamba "Mkopo wa ndani" yaani *local loan* ni mkopo ambao Serikali inaupata ndani ya Tanzania. Ibara ya tano ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya tafsiri ya maneno "mkopo wa nje" (*foreign loan*) na "mkopo wa ndani" (*local loan*) ili kutoa tafsiri inayoainisha chanzo cha mkopo husika kama ni ndani au nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, inapendekezwa kuwa tafsiri ya maneno "mkopo wa nje" iwe mkopo ambao Serikali inaupata kutoka chanzo ambacho siyo cha ndani yaani, *non-resident sources* na "mkopo wa ndani" iwe mkopo ambao Serikali inaupata kutoka chanzo cha ndani yaani, *resident sources*. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri sahihi ya maana ya mikopo kutoka nje na ndani kulingana na Mwongozo wa *IMF/World Bank Public Debt Management Guidelines* ambao unatumika katika nchi zote wanachama wa Taasisi hizo kama nilivyoeleza awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tatu kinampatia Waziri mwenye dhamana ya fedha mamlaka ya kutafuta mkopo wa nje (*foreign loan*) kwa masharti ikiwemo riba, marejesho na masharti mengine ambayo yatakubaliwa wakati wa majadiliano. Kifungu hiki hakielezi kama katika kutekeleza mamlaka haya Waziri atashauriwa na chombo kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria hiyo imeanzisha Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa (*The National Debt Management Committee*) ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 17(a) cha Sheria hiyo, moja ya kazi zake ni kumshauri Waziri juu ya masuala yanayohusiana na mkopo wa nje na mkopo wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya sita ya Muswada inapendekeza kuwa Waziri atekeleze mamlaka hayo baada ya kupata ushauri wa Kamati hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha Waziri mwenye dhamana ya fedha anashauriwa na Kamati hiyo katika masuala yote yanayohusu mikopo, dhamana na Misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo pia inapendekeza kuongeza maneno "*concessional*" na "*non-concessional*" kwa lengo la kufafanua aina ya mkopo wa nje unaoweza kuombwa kuwa unaweza kuwa wa kibiashara au mkopo usiokuwa wa kibiashara. Pia, Ibara hiyo ya sita kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha 3(2) cha Sheria hiyo kwa lengo la kuweka masharti yanayoainisha kuwa mkopo wa nje unaweza kupatikana kwa kukopa kutoka chanzo cha nje, kutoa hati fungani au njia nyingine kama ambavyo Waziri ataona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kutambua au kurahisisha matumizi ya Sheria kufuatia uamuzi wa Serikali kuanza kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka kutoka soko la fedha la nje ili kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya saba ya Muswada iliyokuwa inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 5(b) cha Sheria hiyo imefutwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine katika Sehemu hii yanahusu kifungu cha sita cha Sheria hiyo kinachoweka masharti kuhusu mamlaka ya kutafuta mkopo wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nane ya Muswada inapendekeza kuongeza masharti yatakayomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kutekeleza mamlaka yake ya kukopa mikopo ya ndani baada ya kupata ushauri wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha saba cha Sheria hiyo ili kumpatia Waziri mwenye dhamana ya fedha uwezo wa kukasimu mamlaka yake ya kukopa ndani ya nchi kupitia amana za Serikali zinazotolewa na Benki Kuu kwa Gavana wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kumpatia Waziri mwenye dhamana ya fedha uwezo wa kukasimisha mamlaka hayo. Kwa utaratibu wa sasa, amana za Serikali zinatolewa na Benki Kuu kwa niaba ya Serikali bila ya kuwa na msingi wa kisheria.

Pia, inapendekezwa vifungu vya nane na 10 vya Sheria hiyo virekebishwe kwa lengo la kuongeza masharti yatakayomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kutekeleza mamlaka yake ya kukubali au kutoa masharti ya riba na dhamana baada ya kupata ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa kama inavyoonekana katika Ibara ya 10 na 11 ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12 ya Muswada kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kufuta rejea ya Sheria ya "*The Lotteries Act*, inayotajwa katika maneno ya pembeni (*marginal note*) ya kifungu cha 11 na kuweka badala yake "*The Gaming Act*" kwa kuwa masuala ya bahati nasibu kwa sasa yanasimamiwa na hiyo sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kufuta kifungu cha 12 kinachoweka masharti kuhusu riba kutegemea na kodi ya zuio yaani *interest subject to withhoding tax* ili masuala ya kodi hiyo yashughulikiwe kupitia Sheria za kodi husika. Kutokana na kifungu hicho kufutwa na kwa kuzingatia kuwa suala la mikopo ya nje ni moja ya Mambo ya Muungano ambayo kwa mujibu

wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanasimamiwa na kutekelezwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza masharti mapya kuhusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuingia utaratibu wa *on-lending* pale Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapochukua mikopo kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mkopeshaji akahitaji masharti ya utaratibu wa *on-lending* yawepo kabla ya kutoa mkopo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa pia kuwa kabla Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijakopa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itajiridhisha kuwa mkopo huo unaweza kulipwa. Lengo la marekebisho haya katika Ibara ya 13 ya Muswada ni kuweka utaratibu wa kisheria utakakaoiwezesha Serikali ya Tanzania kukidhi masharti ya baadhi ya wakopeshaji wanaohitaji masharti hayo na pia kuhakikisha mikopo inalipwa kwa mujibu wa makubaliano ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kifungu kipya cha 12A ambacho kinaweka masharti kuhusu Serikali za Mtaa, Shirika la Umma kukopa mkopo ambao Serikali imeupata chini ya Sheria hiyo baada ya kujiridhisha kuhusu makadirio ya kupata fedha itakayokidhi masharti ya mkopo mama na kwamba mkopo husika utatumika kama mtaji wa uwekezaji katika miradi inayolipa ambayo ni muhimu kiuchumi. Aidha, Serikali za Mtaa, Shirika la Umma inayotaka kukopa chini ya kifungu hicho itapaswa kuingia utaratibu wa *on-lending arrangement* ambao masharti yake yatakaribiana na masharti ya mkopo mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu maalum wa kisheria *(on-lending arrangement)* utakaoiwezesha taasisi husika kupata mkopo na kuhakikisha kuwa fedha za mkopo utakaochukuliwa unatumika kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi yenye uwezo wa kuzalisha mapato ya kulipia mkopo na gharama ya mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unapendekeza pia kuongeza kifungu kipya cha 12B kinachoweka masharti kuwa Taasisi yoyote ya Serikali inapotaka kukopa ni sharti ipate kwanza kibali cha Waziri mwenye dhamana ya fedha kuhusiana na malengo, kiasi na masharti ya mkopo huo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinakopa kwa malengo yanayoeleweka na masharti yenye maslahi na unafuu kwa taasisi hizo na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 15 kama ilivyoboreshwa zaidi kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 cha Sheria hiyo kinachoweka masharti kuhusu mamlaka ya kutoa dhamana ya mikopo chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma. Sheria ilivyo sasa inampatia Waziri mwenye dhamana ya fedha mamlaka ya kutoa dhamana ya mkopo unaoombwa na shirika la umma baada ya kupokea ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa na kwa kuzingatia maslahi ya umma juu ya mkopo huo.

Muswada unapendekeza kuongeza masharti mapya kwamba Serikali itafanya tathmini kabla ya kutoa dhamana husika na kwamba Waziri atawajibika pia kusimamia dhamana inayotolewa kwenye miradi ya ubia wa sekta binafisi ya sekta ya umma. Pia, inapendekezwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha awe na mamlaka ya kuandaa Kanuni zitakazobainisha ada ya dhamana ambayo itatozwa kwa mkopeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kudhibiti ukuaji wa madeni yanayotokana na dhamana za Serikali, kuiwezesha Serikali kukabiliana na athari zitakazojitokeza kutokana na dhamana iliyotolewa na kupunguza idadi ya wakopeshaji wanaoomba dhamana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 13A cha Sheria hiyo kinarekebishwa kama inavyoonekana katika Ibara ya 16 ya Muswada ili kuelekeza kwamba mkopo utakaochukuliwa kwa dhamana ya Serikali utumike kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi yenye uwezo wa kuzalisha mapato ya kulipia deni na dhamana ya mikopo. Aidha, inapendekezwa kuwa Waziri atatoa dhamana itakayofikia asilimia 85 kwenye masuala yanayohusu majanga ya kitaifa kama mafuriko, tetemeko la ardhi na kadhalika na hivyo kuondoa utata uliopo hivi sasa kuhusu mazingira ambayo Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana zaidi ya asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 17 cha Sheria hiyo ili kuweka masharti yatakayoipatia Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana ya fedha katika kuandaa mkakati wa usimamizi wa madeni ikiwemo mpango wa ukopaji wa Serikali kwa mwaka na kusimamia masuala yote yanayohusu usimamizi wa madeni, dhamana na misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 kimefanyiwa marekebisho kama inavyoonekana katika Ibara ya 18 ya Muswada na Jedwali la Marekebisho ili kulinda maslahi ya Zanzibar kuhusiana na mikopo kwa kuongeza wajumbe wa

Zanzibar katika Kamati ya Kitaifa ya kusimamia deni la Taifa. Wajumbe wanaopendekezwa kuongewa katika Kamati hiyo ni Katibu wa Tume ya Mipango-Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuwa wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya kusimamia deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, inapendekezwa kuwa Kamati hiyo iwe na uwezo wa kumwalika (*co-opt*) mtu mwenye uwezo na utaalam katika jambo ambalo Kamati inahitaji utaalam huo na kwamba mjumbe huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utendaji kazi wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 22 cha Sheria hiyo ili kuweka masharti kuhusu akidi ya vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa deni la Taifa ambayo inapendekezwa iwe ni nusu ya wajumbe wa Kamati. Pia, Ibara hiyo inapendekeza kuweka masharti yatakayowataka wajumbe wa Kamati hiyo kuhudhuria vikao vya Kamati wao binafsi na pale mjumbe anaposhindwa kuhudhuria kutokana na ugonjwa au kutokuwepo ndani ya Tanzania, ateue Afisa Mwandamizi atakayehudhuria kwa niaba yake. Marekebisho haya yanalenga pia kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza marekebisho madogo katika kifungu cha 25 cha Sheria kwa kufuta neno *fiscal* na kuweka badala yake neno *financial* kwa lengo la kukifanya kifungu hicho kisomeke vizuri. Aidha, Ibara hiyo inapendekeza masharti yanayomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha Serikalini taarifa ya utekelezaji wa mpango wa deni kwa kipindi cha robo mwaka yafutwe kwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha anawasilisha taarifa ya utekelezaji ya mpango mkakati ya ukopaji baada ya kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha na siyo kwa kipindi cha robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 30 cha Sheria ambacho kinaweka masharti kuhusu Waziri mwenye dhamana ya fedha kukasimu madaraka yake chini ya Sheria hiyo. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa Waziri anaweza kukasimu mamlaka yake ya kujadili mkopo (*negotiating loan*), kuingia makubaliano ya kukopa mkopo na kutoa dhamana. Muswada unapendekeza kuwa Waziri awe na uwezo wa kukasimu pia mamlaka ya kujadili au kuingia makubaliano ya msaada kwa Mamlaka au mtu mwingine. Lengo la marekebisho haya ni

kurahisisha taratibu za upokeaji misaada kwa kuwa sheria hiyo ilikuwa kimya kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya mwisho katika Sheria hiyo ni kuongeza kifungu kipya cha 30A kinachoweka masharti kuhusu makosa kama ifuatavyo:-

(a) Mtu yeyote atakayeingia Mkataba wa mkopo pasipo kupata kibali cha Waziri mwenye dhamana ya fedha anatenda kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi milioni ishirini au kifungo gerezani kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka sita au vyote kwa pamoja.

(b) Mkuu wa Taasisi za Umma, Shirika la Umma, Idara au Wakala wa Serikali ambayo ilipata dhamana ya Serikali na ikashindwa kurejesha mkopo atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma; na

(c) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya Sheria hiyo ambayo adhabu haijaainishwa, adhabu yake itakuwa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi milioni kumi au kifungo gerezani kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya ambayo yako katika Ibara ya 22 ya Muswada yanalenga kuhakikisha kuwa watendaji na watumishi wanaohusika na utekelezaji wa sheria hiyo wanazingatia ipasavyo masharti ya Sheria hii kwa mikopo na dhamana inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178 (*The Higher Eduaction Students' Loan Board Act, Cap. 178)*. Sheria ilivyo sasa inatoa tafsiri kuwa "Taasisi iliyothibitishwa" (*Accredited Institution*) ni taasisi ambayo inatoa kozi ya *postgraduate diploma* ya mafunzo ya sheria kwa vitendo, shahada (*degree*), stashahada ya juu (*higher diploma*), stashahada (*diploma*) ya ualimu wa Sayansi, Hisabati, Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanafunzi wanaosoma katika taasisi zilizothibitishwa ndiyo wenye sifa ya kupatiwa mkopo wa elimu, Ibara ya 25 ya Muswada kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuboresha tafsiri ya maneno "Taasisi iliyothibitishwa" (*Accredited Institution*) kwa lengo la kuwezesha wanafunzi wanaosomea kozi ya stashahada

(*diploma*) katika maeneo mengine ya kitaaluma ambayo hayajaainishwa katika Sheria ya sasa kuwa na sifa ya kupata mkopo wa elimu kama itakavyoelekezwa na Waziri na kwa kuzingatia uhitaji, uwezo na vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ili kuweka uwazi, inapendekezwa kuwa aina ya *diploma* ambazo wanafunzi husika watakuwa na sifa ya kupata mkopo wa elimu zitachapishwa katika Gazeti la Serikali. Kwa maana ya marekebisho kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho hakutakuwepo tena na suala la hiki kitu kinachoitwa *higher diploma*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (*The Income Tax Act, Cap 332*). Kifungu cha 10(3) cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa bila kujali masharti ya sheria hiyo, msamaha usitolewe kwa kodi inayotozwa chini ya Sheria hiyo na kwamba makubaliano yoyote yanayoathiri utekelezaji wa Sheria hiyo yasiingiwe isipokuwa kwa masharti ya Sheria hiyo au marekebisho ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 27 ya Muswada inapendekeza kifungu hicho cha 10(3) kifutwe na kuandikwa upya ili kuongeza masharti yatakayowezesha msamaha wa kodi ya mapato kutolewa na Serikali kwa kuingia Mkataba kwa ajili hiyo katika mradi ya kimkakati (*strategic project*) au kwa maslahi ya umma baada ya kibali cha Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kufanikisha, pale inapobidi, utekelezaji wa miradi hiyo ipasavyo bila kukwamishwa na masharti ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura 113 (*The Land Act, Cap 113*). Kifungu cha 19(2) cha Sheria hiyo kinaelekeza pamoja na mengineyo kuwa mtu ambaye siyo raia wa Tanzania anaweza kupata hati ya kumiliki ardhi au haki ya kutumia ardhi (*derivative rights)* kwa ajili ya uwekezaji chini ya Sheria ya Uwekezaji na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ya *The Export and Processing Zones Act* katika kifungu chake cha 13 inaipatia *EPZA* mamlaka ya kutwaa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya ardhi na Serikali ya Mtaa na kisha kutoa haki ya kutumia (*derivatie rights)* kwa wawekezaji, Ibara ya 29 ya Muswada inapendekeza kifungu hicho cha 19(2) cha Sheria ya Ardhi kirekebishwe ili kuongeza masharti yatayowezesha haki ya kutumia ardhi inayomilikiwa chini ya Sheria ya *the Export*

*and Processing Zones Act* kutolewa kwa wawekezaji. Marekebisho haya yanalenga kuoanisha masharti ya Sheria hizo mbili na kuziwezesha Sheria hizo kutekelezeka kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ambayo ilikuwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220 (*The Road and Fuel Tolls Act, Cap. 220*) imeondolewa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ni iliyokuwa Sehemu ya Saba ya Muswada na inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Sukari, Sura ya 251 (*The Sugar Industry Act, Cap 251*). Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, kifungu cha tatu cha Sheria hiyo kinarekebishwa kwa ajili ya kuongeza tafsiri ya neno "*blending*" ambalo limetumika kupitia marekebisho ya Sheria hiyo katika Muswada huu ili kurahisisha matumizi ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha nne cha Sheria hiyo kinaainisha kazi na majukumu mbalimbali ya Bodi ya Sukari. Muswada unapendekeza katika Ibara ya mpya ya 31 (awali ilikuwa Ibara ya 39) kuwa kifungu hicho kirekebishwe ili kuiongezea Bodi hiyo mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo na upanuzi wa wazalishaji wa sukari. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Bodi kuhakikisha kuwa wazalishaji wanatekeleza mpango huo ipasavyo na kuongeza uzalishaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara mpya ya 32 ya Muswada (awali ilikuwa Ibara ya 40) inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 7A na 7B katika Sheria hiyo. Kifungu kipya cha 7A kinaweka masharti kuhusu Vyama vya Wakulima wa Miwa (*Sugarcane Growers Organisations*). Inapendekezwa kuwa wakulima wa miwa wajiunge pamoja katika mfumo wa vyama vya ushirika vilivyosajiliwa chini ya Sheria ya Ushirika ndani ya miezi sita tangu kuanza kutumika kwa marekebisho ya Sheria hiyo. Ibara hii imeboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho kwa kuondoa sharti la wakulima wa miwa kupata kwanza kibali cha Bodi ya Sukari kabla ya kujiunga katika mfumo wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Bodi imepewa mamlaka ya kuongeza muda huo kwa kipindi kingine cha miezi sita iwapo itaona kuna umuhimu kuongeza muda huo upo. Vilevile, ili kuhakikisha kuwa miwa inayozalishwa inakidhi viwango, Bodi baada ya kushauriana na wakulima wa miwa na wazalishaji wa sukari itaainisha kiwango cha miwa inayotakiwa kuzalishwa na kila chama cha ushirika. Marekebisho haya yanalenga kuwezesha usimamizi mzuri wa kilimo cha miwa pamoja na kuwaweka pamoja wakulima wa miwa ili

kulinda maslahi yao na pia kuongeza uwazi na uwajibikaji katika vyama vya wakulima wa miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kipya cha 7B kinaweka masharti kuhusu Jukwaa la Mashauriano la Wakulima wa Miwa (*Sugarcane Growers Consulative Forum*) ambalo litawajibika kwa masuala yote yanayohusu kilimo cha miwa. Inapendekezwa kuwa Bodi itaainisha muundo, sifa, muda na namna Jukwaa hilo litakavyoendeshwa. Kwa ujumla marekebisho katika Ibara ya 32 ya Muswada yanalenga kuboresha mfumo wa wakulima ili kuongeza ufanisi na faida katika biashara ya sukari, kuboresha uwezo wa kufanya majadiliano ya mikataba ya ununuzi wa miwa, kuweka uwazi katika usimamizi na kuondoa ubadhirifu wa mali za wakulima wa miwa zinazomilikiwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya mpya ya 33 ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 41) inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 11A kinachoweka masharti kuhusu bei elekezi ya miwa, sukari na bidhaa nyingine zitokanazo na miwa. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, kifungu hicho kipya kinaeleza kuwa Bodi ya Sukari baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya kilimo pamoja na wadau inaweza kuchapisha katika Gazeti la Serikali bei ya chini au bei elekezi kwa lugha nyingine ambayo wazalishaji watalipa kwa miwa inayozalishwa na wakulima pamoja na bei ya juu ya sukari na bidhaa zitokanazo na miwa kutoka kwa wazalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha wakulima wa miwa wanauza miwa yao kwa bei inayoendana na soko na kuwezesha watumiaji na wazalishaji wa sukari kununua au kuuza sukari kwa bei inayoendana na soko na hivyo kulinda maslahi ya wadau wote ambao ni mkulima wa miwa, mzalishaji wa sukari na watumiaji wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara mpya ya 34 ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 42) inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 17A katika Sheria hiyo kinachoweka masharti yanayomtaka kila mzalishaji wa sukari kuwasilisha kwenye Bodi ya Sukari mpango wake wa maendeleo na upanuzi. Mpango huo, utajumuisha, upanuzi wa mashamba na kuongeza uzalishaji wa miwa, kuleta teknolojia mpya kwa lengo la kuongeza tija na mbegu mpya za miwa, kuongeza uwezo wa uwekezaji katika uchakataji na taarifa nyingine ambayo Bodi inazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, inapendekezwa kuwa mzalishaji atakayeshindwa kutekeleza masharti hayo apewe notisi ya kujieleza kwa maandishi sababu za kushindwa

kutekeleza masharti hayo. Iwapo mzalishaji husika atashindwa kutoa maelezo hayo ndani muda ulioainishwa katika notisi au iwapo Bodi haitaridhishwa na maelezo yake, Bodi ya Sukari inaweza kumtoza faini isiyopungua milioni thelathini na isiyozidi shilingi milioni mia moja. Mzalishajji ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Bodi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri na pia kuomba nafuu Mahakamani iwapo hataridhishwa na uamuzi utakaotolewa na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yanalenga kuiwezesha Bodi kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kusimamia utekelezaji wa Mpango huo kwa wazalishaji wa sukari na hivyo kuendeleza sekta ya sukari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya mwisho yanayopendekezwa katika Sehemu hii ni kuongeza kifungu kipya cha 34A kinachoweka masharti kuhusu zuio la uchanganyaji sukari (*blending process*) kama inavyoonekana katika Ibara ya 35 ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 43) inaweka katazo la uchanganyaji sukari baada ya miezi sita tangu marekebisho katika Sheria hiyo kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, inapendekezwa kuwa mtu atakayekiuka masharti hayo atakuwa anatenda kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni mia moja au kiasi kinacholingana na thamani ya milioni mia moja na thamani ya sukari iliyochanganywa au kifungo gerezani kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano. Mbali ya adhabu hiyo, Bodi ya Sukari inaweza kusitisha au kufuta leseni iliyotolewa kwa mtu huyo. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia sukari iliyochanganywa ili kulinda soko la miwa na viwanda vya ndani kwa kuwa sukari iliyochanganywa inazalishwa kwa kutumia sukari ya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura ya 283 (*The Wildlife Conservation Act, Cap 283*). Kifungu cha 101 cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa katika hatua yoyote ya kesi Mahakama inaweza kwa kuamua yenyewe au kwa maombi ya upande wa mashtaka kutoa amri kuwa mnyama, nyara ya Serikali, silaha, gari au kitu chochote kilichotolewa kama ushahidi ambacho kinaweza kuharibika au kupoteza thamani kiuzwe au kuharibiwa *(dispose off)* na Mkurugenzi wa Wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yanaweza kutokea mazingira ambayo vitu hivyo vinaweza kuharibika au kupoteza thamani wakati taratibu za kufungua kesi mahakamani ikiwemo kukamilisha upelelezi zikiendelea, Ibara ya mpya ya 37 ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 45) inapendekeza

kufuta kifungu hicho kirekebishwe ili kuongeza masharti yatakayoipatia Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kuuza au kuharibu vitu hivyo baada ya kupokea maombi ya upande wa mashtaka hata kama kesi haijafunguliwa Mahakamani na kwamba amri hiyo itatumika kama ushahidi kuhusu suala hilo wakati wa usikilizaji wa kesi husika ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kutunza na kupata ushahidi utakaotumika katika kesi itakayofunguliwa dhidi ya mshtakiwa aliyekutwa na mnyama, nyara ya Serikali au kitu chochote kinachoweza kuharibika mapema au kupoteza thamani kabla ya taratibu za kufungua kesi ya jinai kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments)* (No.4) Act, 2016) na naomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, naona hoja imeungwa mkono tutajadili baadaye kuhusiana na hilo.

**HOTUBA YA NDUGU GEORGE M. MASAJU, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.4) WA MWAKA 2016 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.4) ACT, 2016) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa Hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Act, 2016)** kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe Mara ya Pili; na Bunge lako

Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu katika Bunge hili. Ninakupongeza wewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyoendelea kuliongoza Bunge letu. Pia, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali. Pia, ninawashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Nchini.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi, Dimani. Ninawapongeza Mhe. Abdallah Majula Bulembo, Mhe. Anne Kilango Malecela na Mhe. Prof Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Wabunge. Ninawatakia kila kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ya Kibunge.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu. Mwisho, ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuipatia Ofisi ya Mwasheria Mkuu wa Serikali ushirikiano kwa njia mbali mbali ikiwemo ushauri, Maombi, Sala, Dua, taarifa muhimu n.k. na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.4) Act, 2016)** ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mbunge wa Rufiji) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kazi nzuri ilifanywa na Kamati hii kwa kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau walioitwa kwenye Kamati hiyo kabla ya kutoa mapendekezo yake kwa Serikali kwa nia ya kuboresha Muswada huu. Ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati hiyo, vimesaidia kuuboresha Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali ya Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016, (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.4) Act, 2016**, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Sita (6). Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati kutumia masharti ya sheria hizo na pia kuoanisha masharti ya Sheria zinazorekebishwa na masharti yaliyoko katika sheria nyingine zilizopo. Baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika Muswada huu, ni kubadilisha vifungu vya Sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo-

7. Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura ya 134; Sheria(**The Government Loans, Guarantees and Grants Act, Cap.134**);
8. Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178(**The Higher Education Students' Loans Board Act, Cap. 178**);
9. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (**The Income Tax, Cap. 332**);
10. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (**The Land Act, Cap. 113**);
11. Sheria ya Sukari, Sura ya 251 (**The Sugar Industry Act, Cap.251**); na
12. Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283 (**The Wildlife Conservation Act, Cap. 283**).

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu saba ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya Utangulizi, ikiwa ni pamoja na, jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 (**The Government Loans, Guarantees and Grants Act, Cap.134**). **Ibara ya 4** ya Muswada inapendekeza marekebisho ya ujumla kwa kufuta maneno "kutoka nje ya Tanzania (*from outside Tanzania*) popote yanapojitokeza katika Sheria hiyo na kuweka badala yake maneno "kutoka vyanzo ambayo siyo vya ndani" (*from non-resident sources*). Lengo la marekebisho haya ni kuwa na tafsiri sahihi ya maana ya mikopo kutoka nje kulingana na Miongozo ya *International Monetary Fund* (IMF)*()/World Bank Public Debt Management Guidelines*

ambayo kimsingi inatumika katika nchi zote wanachama wa Taasisi hizi. Mwongozo huo unaelekeza kama ifuatavyo;

> *"To qualify as external debt, the debt liabilities must be owed by a resident to a non resident. Residence is determined by where the debtor and creditor have their center of predominant economic interest-typically, where they are ordinarily located and-not by their nationality."*

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2 kinachotoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria hiyo. Marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza tafsiri ya maneno "Mfuko Mkuu wa Hazina" (*Consolidated Fund)* kuwa ni Mfuko Mkuu wa Hazina ambao umetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Tafsiri nyingine inayopendekezwa kuongezwa katika kifungu hicho ni ya maneno "*on lending*" ambayo yatamaanisha utaratibu ambapo Serikali hukopa kutoka chanzo cha nje au ndani na kisha kutoa mkopo huo kwa mamlaka nyingine kama vile Shirika la Umma au Serikali za Mitaa na inapobidi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kama inavyooenakana katika Jedwali la Marekebisho na kwa kuzingatia ushauri wa Kamati, tumependekeza kuongeza tafsiri ya maneno "mkopo mama" (*primary loan*) na "vyanzo vya ndani" (*resident sources*) ambayo yametumika katika Sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri ya maneno hayo ili kurahisisha matumizi ya Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ilivyo sasa inatoa tafsiri kuwa "mkopo wa nje" (*foreign loan*) ni mkopo ambao Serikali inaupata kutoka nje ya Tanzania na kwamba "Mkopo wa ndani" (*local loan*) ni mkopo ambao Serikali inaupata ndani ya Tanzania. **Ibara ya 5** ya Muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya tafsiri ya maneno "mkopo wa nje" (*foreign loan*) na "mkopo wa ndani" (*local loan*) ili kutoa tafsiri inayoainisha chanzo cha mkopo husika kama ni ndani au nje ya Tanzania. Hivyo, inapendekezwa kuwa tafsiri ya maneno "mkopo wa nje" iwe mkopo ambao Serikali inaupata kutoka chanzo ambacho siyo cha ndani yaani, *non resident sources* na "mkopo wa ndani" iwe mkopo ambao Serikali inaupata kutoka chanzo cha ndani yaani, *resident sources*. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri sahihi ya maana ya mikopo kutoka nje na ndani kulingana na Mwongozo wa *IMF/World Bank Public Debt Management Guideliness* ambao unatumika katika nchi zote wanachama wa Taasisi hizo kama nilivyoeleza awali.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 3 kinampatia Waziri mwenye dhamana ya fedha mamlaka ya kutafuta mkopo wa nje (*foreign loan*) kwa masharti ikiwemo riba, marejesho na masharti mengine ambayo yatakubaliwa wakati wa majadiliano. Kifungu hiki hakielezi kama katika kutekeleza mamlaka haya

Waziri atashauriwa na chombo kingine chochote. Kwa kuwa Sheria hiyo imeanzisha Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa (*The National Debt Management Committee*) ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 17(a) cha Sheria hiyo, moja ya kazi zake ni kumshauri Waziri juu ya masuala yanayohusiana na mkopo wa nje na mkopo wa ndani, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza kuwa Waziri atekeleze mamlaka hayo baada ya kupata ushauri wa Kamati hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha Waziri mwenye dhamana ya fedha anashauriwa na Kamati hiyo katika masuala yote yanayohusu mikopo, dhamana na Misaada.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara hiyo pia inapendekeza kuongeza maneno "*concessional*" na "*non concessional*" kwa lengo la kufafanua aina ya mkopo wa nje unaoweza kuombwa kuwa unaweza kuwa wa kibiashara au mkopo usiokuwa wa kibiashara. Pia, Ibara hiyo ya 6 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha 3(2) cha Sheria hiyo kwa lengo la kuweka masharti yanayoainisha kuwa mkopo wa nje unaweza kupatikana kwa kukopa kutoka chanzo cha nje, kutoa hati fungani au njia nyingine kama ambavyo Waziri ataona inafaa. Lengo la marekebisho haya ni kutambua au kurahisisha matumizi ya Sheria kufuatia uamuzi wa Serikali kuanza kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka kutoka soko la fedha la nje ili kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 7** ya Muswada iliyokuwa inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 5(b) cha Sheria hiyo imefutwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho mengine katika Sehemu hii yanahusu kifungu cha 6 cha Sheria hiyo kinachoweka masharti kuhusu mamlaka ya kutafuta mkopo wa ndani. **Ibara ya 8** ya Muswada inapendekeza kuongeza masharti yatakayomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kutekeleza mamlaka yake ya kukopa mikopo ya ndani baada ya kupata ushauri wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 9** ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 7 cha Sheria hiyo ili kumpatia Waziri mwenye dhamana ya fedha uwezo wa kukasimu mamlaka yake ya kukopa ndani ya nchi kupitia amana za Serikali zinazotolewa na Benki Kuu kwa Gavana wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kumpatia Waziri mwenye dhamana ya fedha uwezo wa kukasimisha mamlaka hayo. Kwa utaratibu wa sasa, amana za Serikali zinatolewa na Benki Kuu kwa niaba ya Serikali bila ya kuwa na msingi wa kisheria.

Pia, inapendekezwa vifungu vya 8 na 10 vya Sheria hiyo virekebishwe kwa lengo la kuongeza masharti yatakayomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kutekeleza mamlaka yake ya kukubali au kutoa masharti ya riba na dhamana baada ya kupata ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa kama inavyoonekana katika **Ibara ya 10** na **11** ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12** ya Muswada kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kufuta rejea ya Sheria ya "*the Lotarries Act*, inayotajwa katika maneno ya pembeni (*maginal note*) ya kifungu cha 11 na kuweka badala yake "*the Gaming Act*" kwa kuwa masuala ya bahati nasibu kwa sasa yanasimamiwa na Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, **Ibara ya 13** kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kufuta kifungu cha 12 kinachoweka masharti kuhusu riba kutegemea na kodi ya zuio yaani *interest subject to withhoding tax* ili masuala ya kodi hiyo yashughulikiwe kupitia Sheria za kodi husika. Kutokana na kifungu hicho kufutwa na kwa kuzingatia kuwa suala la mikopo ya nje ni moja ya Mambo ya Muungano ambayo kwa mujibu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanasimamiwa na kutekelezwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano Tanzania, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza masharti mapya kuhusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuingia utaratibu wa *on-lending* pale Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapochukua mikopo kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mkopeshaji akahitaji masharti ya utaratibu wa *on-lending* yawepo kabla ya kutoa mkopo husika.

Inapendekezwa pia kuwa kabla Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijakopa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itajiridhisha kuwa mkopo huo unaweza kulipwa. Lengo la marekebisho haya katika Ibara ya 13 ya Muswada ni kuweka utaratibu wa kisheria utakakaoiwezesha Serikali ya Tanzania kukidhi masharti ya baadhi ya Wakopeshaji wanaohitaji masharti hayo na pia kuhakikisha mikopo inalipwa kwa mujibu wa Makubaliano ya Mkopo.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 14** ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kifungu kipya cha 12A ambacho kinaweka masharti kuhusu Serikali za Mtaa, Shirika la Umma kukopa mkopo ambao Serikali imeupata chini ya Sheria hiyo baada ya kujiridhisha kuhusu makadirio ya kupata fedha itakayokidhi masharti ya mkopo mama na kwamba mkopo husika utatumika kama mtaji wa uwekezaji katika miradi inayolipa ambayo ni muhimu kiuchumi. Aidha, Serikali za Mtaa, Shirika la Umma inayotaka

kukopa chini ya kifungu hicho itapaswa kuingia utaratibu wa *on-lending arrangement* ambao masharti yake yatakaribiana na masharti ya mkopo mama. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu maalumu wa kisheria *(on-lending arrangement*) utakaoiwezesha taasisi husika kupata mkopo na kuhakikisha kuwa fedha za mkopo utakaochukuliwa unatumika kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi yenye uwezo wa kuzalisha mapato ya kulipia mkopo na gharama ya mkopo.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada unapendekeza pia kuongeza kifungu kipya cha 12B kinachoweka masharti kuwa Taasisi yoyote ya Serikali inapotaka kukopa ni sharti ipate kwanza kibali cha Waziri mwenye dhamana ya fedha kuhusiana na malengo, kiasi na masharti ya mkopo huo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinakopa kwa malengo yanayoeleweka na masharti yenye maslahi na unafuu kwa taasisi hizo na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15** kama ilivyoboreshwa zaidi kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 cha Sheria hiyo kinachoweka masharti kuhusu mamlaka ya kutoa dhamana ya mikopo chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma. Sheria ilivyo sasa inampatia Waziri mwenye dhamana ya fedha mamlaka ya kutoa dhamana ya mkopo unaoombwa na shirika la umma baada ya kupokea ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa na kwa kuzingatia maslahi ya umma juu ya mkopo huo. Muswada unapendekeza kuongeza masharti mapya kwamba Serikali itafanya tathmini kabla ya kutoa dhamana husika na kwamba Waziri atawajibika pia kusimamia dhamana inayotolewa kwenye miradi ya ubia wa sekta binafisi ya sekta ya umma. Pia, inapendekezwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha awe na mamlaka ya kuandaa Kanuni zitakazobainisha ada ya dhamana ambayo itatozwa kwa mkopeshaji. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti ukuaji wa madeni yanayotokana na dhamana za Serikali, kuiwezesha Serikali kukabiliana na athari zitakazojitokeza kutokana na dhamana iliyotolewa na kupunguza idadi ya wakopeshaji wanaoomba dhamana ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu 13A cha Sheria hiyo kinarekebishwa kama inavyoonekana katika **Ibara ya 16** ya Muswada ili kuelekeza kwamba mkopo utakaochukuliwa kwa dhamana ya Serikali utumike kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi yenye uwezo wa kuzalisha mapato ya kulipia deni na gharama ya mkopo. Aidha, inapendekezwa kuwa Waziri atatoa dhamana itakayofikia asilimia 85 kwenye masuala yanayohusu majanga ya kitaifa kama mafuriko, tetemeko la ardhi n.k na hivyo kuondoa utata uliopo hivi sasa kuhusu mazingira ambayo Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana zaidi ya asilimia 70.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 17** ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 17 cha Sheria hiyo ili kuweka masharti yatakayoipatia Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana ya fedha katika kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Madeni ikiwemo mpango wa ukopaji wa Serikali kwa mwaka na kusimamia masuala yote yanayohusu usimamizi wa madeni, dhamana na misaada.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 18 kimefanyiwa marekebisho kama inavyoonekana katika **Ibara ya 18** ya Muswada na Jedwali la Marekebisho ili kulinda maslahi ya Zanzibar kuhusiana na mikopo kwa kuongeza wajumbe wa Zanzibar katika Kamati ya Kitaifa ya kusimamia Deni la Taifa. Wajumbe wanaopendekezwa kuongewa katika Kamati hiyo ni Katibu wa Tume ya Mipango-Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuwa wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya kusimamia Deni la Taifa. Vilevile, inapendekezwa kuwa Kamati hiyo iwe na uwezo wa kumwalika (*co-opt*) mtu mwenye uwezo na utaalam katika jambo ambalo Kamati inahitaji utaalam huo na kwamba mjumbe huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha utendaji kazi wa Kamati hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 19** ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 22 cha Sheria hiyo ili kuweka masharti kuhusu akidi ya vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa ambayo inapendekezwa iwe ni nusu ya wajumbe wa Kamati. Pia, Ibara hiyo inapendekeza kuweka masharti yatakayowataka wajumbe wa Kamati hiyo kuhudhuria vikao vya Kamati wao binafsi, na pale mjumbe anaposhindwa kuhudhuria kutokana na ugonjwa au kutokuwepo ndani ya Tanzania, ateue Afisa Mwandamizi atakayehudhuria kwa niaba yake. Marekebisho haya yanalenga pia kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 20** ya Muswada inapendekeza marekebisho madogo katika kifungu cha 25 cha Sheria kwa kufuta neno "*fiscal*" na kuweka badala yake neno "*financial*" kwa lengo la kukifanya kifungu hicho kisomeke vizuri. Aidha, Ibara hiyo inapendekeza masharti yanayomtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha Serikalini taarifa ya utekelezaji wa mpango wa deni kwa kipindi cha robo mwaka yafutwe kwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya fedha anawasilisha taarifa ya utekelezaji ya mpango mkakati ya ukopaji baada ya kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha na siyo kwa kipindi cha robo mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 21** ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 30 cha Sheria ambacho kinaweka masharti kuhusu Waziri

mwenye dhamana ya fedha kukasimu madaraka yake chini ya Sheria hiyo. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa Waziri anaweza kukasimu mamlaka yake ya kujadili mkopo (*negotiating loan*), kuingia makubaliano ya kukopa mkopo na kutoa dhamana. Muswada unapendekeza kuwa Waziri awe na uwezo wa kukasimu pia mamlaka ya kujadili au kuingia makubaliano ya misaada kwa Mamlaka au Mtu mwingine. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha taratibu za upokeaji misaada kwa kuwa sheria hiyo ilikuwa kimya kuhusu suala hilo.

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya mwisho katika Sheria hiyo ni kuongeza kifungu kipya cha 30A kinachoweka masharti kuhusu makosa kama ifuatavyo:

(d) Mtu yeyote atakayeingia Mkataba wa mkopo pasipo kupata kibali cha Waziri mwenye dhamana ya fedha anatenda kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi milioni ishirini au kifungo gerezani kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka sita au vyote kwa pamoja.

(e) Mkuu wa Taasisi za Umma, Shirika la Umma, Idara au Wakala wa Serikali ambayo ilipata dhamana ya Serikali na ikashindwa kurejesha mkopo atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma; na

(f) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya Sheria hiyo ambayo adhabu haijaainishwa, adhabu yake itakuwa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi milioni kumi au kifungo gerezani kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho haya ambayo yako katika **Ibara ya 22** ya Muswada yanalenga kuhakikisha kuwa watendaji na watumishi wanaohusika na utekelezaji wa sheria hiyo wanazingatia ipasavyo masharti ya Sheria hii kwa mikopo na dhamana inayotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178 (*The Higher Eduaction Students' Loan Board Act, Cap. 178)*. Sheria ilivyo sasa inatoa tafsiri kuwa "Taasisi iliyothibitishwa" (*Accredited Institution*) ni taasisi ambayo inatoa kozi ya *postgraduate diploma* ya mafunzo ya sheria kwa vitendo, shahada (*degree*), stashahada ya juu (*higher diploma*), stashahada (*diploma*) ya ualimu wa Sayansi, Hisabati, Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Kwa kuwa wanafunzi wanaosoma katika taasisi zilizothibitishwa ndiyo wenye sifa ya

kupatiwa mkopo wa elimu, **Ibara ya 25** ya Muswada kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuboresha tafsiri ya maneno "Taasisi iliyothibitishwa" (*Accredited Institution*) kwa lengo la kuwezesha wanafunzi wanaosomea kozi ya stashahada (*diploma*) katika maeneo mengine ya kitaaluma ambayo hayajaainishwa katika Sheria ya sasa kuwa na sifa ya kupata mkopo wa elimu kama itakavyoelekezwa na Waziri na kwa kuzingatia uhitaji, uwezo na vipaumbele vya Taifa. Pia, ili kuweka uwazi, inapendekezwa kuwa aina ya diploma ambazo wanafunzi husika watatakuwa na sifa ya kupata mkopo wa elimu zitachapishwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (*The Income Tax Act, Cap 332*). Kifungu cha 10(3) cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa bila kujali masharti ya sheria hiyo, msamaha usitolewe kwa kodi inayotozwa chini ya Sheria hiyo na kwamba makubaliano yoyote yanayoathiri utekelezaji wa Sheria hiyo yasiingiwe isipokuwa kwa masharti ya Sheria hiyo au marekebisho ya Sheria hiyo. **Ibara ya 27** ya Muswada inapendekeza kifungu hicho cha 10(3) kifutwe na kuandikwa upya ili kuongeza masharti yatakayowezesha msamaha wa kodi ya mapato kutolewa na Serikali kwa kuingia Mkataba kwa ajili hiyo katika mradi ya kimkakati (*strategic project*) au kwa maslahi ya umma baada ya kibali cha Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kufanikisha, pale inapobidi, utekelezaji wa miradi hiyo ipasavyo bila kukwamishwa na masharti ya kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura 113 (*The Land Act, Cap 113*). Kifungu cha 19(2) cha Sheria hiyo kinaelekeza pamoja na mengineyo kuwa mtu ambaye siyo raia wa Tanzania anaweza kupata hati ya kumiliki ardhi au haki ya kutumia ardhi (*derivative rights)* kwa ajili ya uwekezaji chini ya Sheria ya Uwekezaji na si vinginevyo. Kwa kuwa Sheria ya *the Export and Processing Zones Act* katika kifungu chake cha 13 inaipatia EPZA mamlaka ya kutwaa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya ardhi na Serikali ya Mtaa na kisha kutoa haki ya kutumia (*derivatie rights)* kwa wawekezaji, Ibara ya 29 ya Muswada inapendekeza kifungu hicho cha 19(2) cha Sheria ya Ardhi kirekebishwe ili kuongeza masharti yatayowezesha haki ya kutumia ardhi inayomilikiwa chini ya Sheria ya *the Export and Processing Zones Act* kutolewa kwa wawekezaji. Marekebisho haya yanalenga kuoanisha masharti ya Sheria hizo mbili na kuziwezesha Sheria hizo kutekelezeka kwa ufanisi ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ambayo ilikuwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220 (*The*

*Road and Fuel Tolls Act, Cap. 220*) imeondolewa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ni iliyokuwa Sehemu ya Saba ya Muswada na inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Sukari, Sura ya 251 (*The Sugar Industry Act, Cap 251*). Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, kifungu cha 3 cha Sheria hiyo kinarekebishwa kwa ajili ya kuongeza tafsiri ya neno "*blending*" ambalo limetumika kupitia marekebisho ya Sheria hiyo katika Muswada huu ili kurahisisha matumizi ya sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 4 cha Sheria hiyo kinaainisha kazi na majukumu mbalimbali ya Bodi ya Sukari. Muswada unapendekeza katika **Ibara ya mpya ya 31** (awali ilikuwa Ibara ya 39) kuwa kifungu hicho kirekebishwe ili kuiongezea Bodi hiyo mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo na upanuzi wa wazalishaji wa sukari. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Bodi kuhahakisha kuwa wazalishaji wanatekeleza mpango huo ipasavyo na kuongeza uzalishaji wa sukari nchini.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara mpya ya 32** ya Muswada (awali ilikuwa Ibara ya 40) inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 7A na 7B katika Sheria hiyo. Kifungu kipya cha 7A kinaweka masharti kuhusu vyama vya wakulima wa miwa (*sugarcane growers organisations*). Inapendekezwa kuwa wakulima wa miwa wajiunge pamoja katika mfumo wa vyama vya ushirika vilivyosajiliwa chini ya Sheria ya Ushirika ndani ya miezi sita tangu kuanza kutumika kwa marekebisho ya Sheria hiyo. Ibara hii imeboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho kwa kuondoa sharti la wakulima wa miwa kupata kwanza kibali cha Bodi ya Sukari kabla ya kujiunga katika mfumo wa vyama vya ushirika. Aidha, Bodi imepewa mamlaka ya kuongeza muda huo kwa kipindi kingine cha miezi sita iwapo itaona kuna umuhimu kuongeza muda huo. Vile vile, ili kuhakikisha kuwa miwa inayozalishwa inakidhi viwango, Bodi baada ya kushauriana na wakulima wa miwa na wazalishaji wa sukari itaainisha kiwango cha miwa inayotakiwa kuzalishwa na kila chama cha ushirika. Marekebisho haya yanalenga kuwezesha usimamizi mzuri wa kilimo cha miwa pamoja na kuwaweka pamoja wakulima wa miwa ili kulinda maslahi yao na pia kuongeza uwazi na uwajibikaji katika vyama vya wakulima wa miwa.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu kipya cha 7B kinaweka masharti kuhusu Jukwaa la Mashauriano la Wakulima wa Miwa (*Sugarcane Growers Consulative Forum*) ambalo litawajibika kwa masuala yote yanayohusu kilimo cha miwa. Inapendekezwa kuwa Bodi itaainisha muundo, sifa, muda na namna Jukwaa hilo litakavyoendeshwa. Kwa ujumla marekebisho katika Ibara ya 32 ya

Muswada yanalenga kuboresha mfumo wa wakulima ili kuongeza ufanisi na faida katika biashara ya sukari, kuboresha uwezo wa kufanya majadiliano ya mikataba ya ununuzi wa miwa, kuweka uwazi katika usimamizi na kuondoa ubadhirifu wa mali za wakulima wa miwa zinazomilikiwa kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya mpya ya 33** ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 41) inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 11A kinachoweka masharti kuhusu bei elekezi ya miwa, sukari na bidhaa nyingine zitokanazo na miwa. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, kifungu hicho kipya kinaeleza kuwa Bodi ya Sukari baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya kilimo pamoja na wadau inaweza kuchapisha katika Gazeti la Serikali bei ya chini ambayo wazalishaji watalipa kwa miwa inayozalishwa na wakulima pamoja na bei ya juu ya sukari na bidhaa zitokanazo na miwa kutoka kwa wazalishaji wa sukari. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha wakulima wadogo wa miwa wanauza miwa yao kwa bei inayoendana na soko na kuwezesha watumiaji na wazalishaji wa sukari kununua au kuuza sukari kwa bei inayoandana na soko na hivyo kulinda maslahi ya wadau wote ambao ni mkulima wa miwa, mzalishaji wa sukari na mtumiaji wa sukari.

**Mheshimiwa Spika, Ibara mpya ya 34** ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 42) inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 17A katika Sheria hiyo kinachoweka masharti yanayomtaka kila mzalishaji wa sukari kuwasilisha kwenye Bodi ya Sukari mpango wake wa maendeleo na upanuzi. Mpango huo, utajumuisha, upanuzi wa mashamba na kuongeza uzalishaji wa miwa, kuleta teknolojia mpya kwa lengo la kuongeza tija na mbegu mpya za miwa, kuongeza uwezo wa uwekezaji katika uchakataji na taarifa nyingine ambayo Bodi itazihitaji. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, inapendekezwa kuwa mzalishaji atakayeshindwa kutekeleza masharti hayo apewe notisi ya kujieleza kwa maandishi sababu za kushindwa kutekeleza masharti hayo. Iwapo mzalishaji husika atashindwa kutoa maelezo hayo ndani muda ulioainishwa katika notisi au iwapo Bodi haitaridhishwa na maelezo yake, Bodi ya Sukari inaweza kumtoza fine isiyopungua milioni thelathini na isiyozidi shilingi milioni mia moja. Mzalishajji ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Bodi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri na pia kuomba nafuu Mahakamani iwapo hataridhishwa na uamuzi utakaotolewa na Waziri. Marekebisho haya yanalenga kuiwezesha Bodi kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kusimamia utekelezaji wa Mpango huo kwa wazalishaji wa sukari na hivyo kuendeleza sekta ya sukari nchini.

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya mwisho yanayopendekezwa katika Sehemu hii ni kuongeza kifungu kipya cha 34A kinachoweka masharti kuhusu zuio la uchanganyaji sukari (*blending process*) kama inavyoonekana katika Ibara ya 35 ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 43) inaweka katazo la uchanganyaji sukari baada ya miezi sita tangu marekebisho katika Sheria hiyo kuanza kutumika. Pia, inapendekezwa kuwa mtu atakayekiuka masharti hayo atakuwa anatenda kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni mia moja au kiasi kinacholingana na thamani ya sukari iliyochanganywa au kifungo gerezani kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano. Mbali ya adhabu hiyo, Bodi ya Sukari inaweza kusitisha au kufuta leseni iliyotolewa kwa mtu huyo. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia sukari iliyochanganywa ili kulinda soko la miwa na viwanda vya ndani kwa kuwa sukari iliyochanganywa inazalishwa kwa kutumia sukari ya viwandani.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Sura ya 283 (*The Wildlife Conservation Act, Cap 283*). Kifungu cha 101 cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa katika hatua yoyote ya kesi Mahakama inaweza kwa kuamua yenyewe au kwa maombi ya upande wa mashtaka kutoa amri kuwa mnyama, nyara ya Serikali, silaha, gari au kitu chochote kilichotolewa kama ushahidi ambacho kinaweza kuharibika au kupoteza thamani kiuzwe au kuharibiwa *(dispose off)* na Mkurugenzi wa Wanyapori. Kwa kuwa yanaweza kutokea mazingira ambayo vitu hivyo vinaweza kuharibika au kupoteza thamani wakati taratibu za kufungua kesi mahakamani ikiwemo kukamilisha upelelezi zikiendelea, **Ibara ya mpya ya 37** ya Muswada (ambayo awali ilikuwa Ibara ya 45) inapendekeza kifungu hicho kirekebishwe ili kuongeza masharti yatakayoipatia Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kuuza au kuharibu vitu hivyo baada ya kupokea maombi ya upande wa mashtaka hata kama kesi haijafunguliwa Mahakamani na kwamba amri hiyo itatumika kama ushahidi kuhusu suala hilo wakati wa usikilizaji wa kesi husika ya jinai. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kutunza na kupata ushahidi utakaotumika katika kesi itakayofunguliwa dhidi ya mshtakiwa aliyekutwa na mnyama, nyara ya Serikali au kitu chochote kinachoweza kuharibika mapema au kupoteza thamani kabla ya taratibu za kufungua kesi ya jinai kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2016 (**The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.4) Act, 2016**) na ninaomba Bunge lako tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa

kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**(HAPA KUNA MUSWADA WA MISCELLANEOUS AMENDMENT)**

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada nianze kwa kumtakia kila mmoja ndani ya Bunge lako hili Tukufu heri ya mwaka mpya ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili kwa mwaka huu 2017 naomba nimtakie heri ya kustaafu vyema Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othmani. Pia nimpongeze Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Juma kwa kuteuliwa kukaimu nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatu niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa mbele ya Bunge hili Tukufu akiwemo Profesa Kabudi, naamini kabisa kwamba watatoa mchango mkubwa katika Bunge lako hili Tukufu hususan katika masuala ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Namba 4 ya Mwaka 2016 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Act of 2016]*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati naendelea kusoma yale yote ambayo nitayapita, basi naomba yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea Muswada huu Mwezi Novemba, baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 10 Novemba 2016 ili iufanyie kazi na tarehe 18 Januari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu Malengo na Madhumuni ya Muswada huu wenye marekebisho katika Sheria Saba mbalimbali kwa madhumuni ya kuondoa upungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura ya 134; Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178; Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Barabara na Tozo za Mafuta, Sura ya 220; Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251; pamoja na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni kuhusu Muswada huu. Kwa upande wa Serikali Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wataalam mbalimbali wa Wizara na Taasisi za Serikali zinazosimamia utekelezaji wa Sheria zinazofanyiwa marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia iliona kuna umuhimu mkubwa, Kama ilivyo katika uendeshaji wa shughuli za Bunge lako Tukufu, kupokea na kuchambua maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika Bunge kabla ya Muswada huu kusomwa Bungeni kwa mara ya Pili. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye alihudhuria vikao vya uchambuzi wa Muswada huu kama Mjumbe Mwalikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mikopo ya Misaada ya Dhamana, Sura 134 kwa kurekebisha Kifungu cha pili ili kubainisha tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika ndani ya Sheria hiyo. Lengo la marekebisho hayo ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria hiyo. Aidha, Kifungu cha 3, 6, 8, 10 na 13A vinafanyiwa marekebisho ili kuweka sharti kwa Waziri wa Fedha kushauriwa na Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa kabla ya kufanya uamuzi wa kukopa pamoja na kuweka utaratibu kwa Serikali kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii pia inapendekeza kurekebisha Kifungu cha saba ili kumpa uwezo Waziri wa Fedha kukasimu Mamlaka yake

kwa Gavana wa Benki Kuu kuhusu kukopa ndani ya nchi kupitia Amana za Serikali zinazotolewa na Benki Kuu. Vilevile, Sehemu hii inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 12 ili kuweka utaratibu kwa Serikali kuzikopesha kwa utaratibu maalum, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi za Umma pindi Serikali inapochukua mikopo kwa niaba yao, ambapo marekebisho husika yamebainisha taratibu zinakazotumika na Taasisi husika katika kurejesha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 12A na 12B vimeongezwa ili kuweka sharti kwa Wizara nyingine na Taasisi za Serikali ambazo zinaruhusiwa kwa mujibu wa Sheria nyingine kukopa, kupata idhini ya Waziri wa Fedha kabla ya kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Kifungu cha 13 yana lengo la kumpa Mamlaka Waziri wa Fedha kuandaa Kanuni zitakazobainisha ada ya dhamana ambayo itatozwa kwa kiwango cha mkopo ili kuiwezesha Serikali kukabiliana na athari zitakazojitokeza kwa dhamana iliyotolewa na kupunguza idadi ya wakopeshaji wanaoomba dhamana ya Serikali. Pili, kuweka utaratibu ili dhamana itakayotolewa na Serikali iwe ni kwa ajili ya mikopo pekee bila kujumuisha gharama nyingine za mkopo na tatu, kumpa Mamlaka Waziri wa Fedha kutoa na kusimamia dhamana zitakazotolewa kwenye miradi ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, inapendekezwa kurekebisha Kifungu 13A ili kuweka sharti kwamba mkopo utakaochukuliwa kwa dhamana ya Serikali utumike kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi yenye uwezo wa kuzalisha mapato ya kulipa deni na gharama ya Mkopo. Aidha, kupitia marekebisho husika Waziri atatoa dhamana itakayofikia asilimia 85 kwenye masuala yanayohusu majanga ya Kitaifa kama mafuriko, tetemeko la ardhi na kadhalika na hivyo kuondoa utata uliopo hivi sasa kuhusu mazingira ambayo Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana zaidi ya asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuipa majukumu Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa kumshauri Waziri wa Fedha katika kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Madeni ikiwemo mpango wa ukopaji wa Serikali kwa mwaka na kusimamia masuala yote yanayohusu usimamizi wa madeni na dhamana na misaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 18 kinafanyiwa marekebisho ili kumwongeza Katibu wa Tume ya Mipango, Zanzibar, kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya kusimamia Deni la Taifa. Vilevile, kupitia marekebisho katika Kifungu

hiki, Kamati imepewa uwezo wa kujumuisha Mjumbe mwingine yeyote pale itakapoona kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 22 kinafanyiwa marekebisho ili kubainisha akidi ya vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa ambayo itakuwa ni nusu ya Wajumbe wa Kamati na kuweka sharti kwa Wajumbe kuhudhuria vikao vya Kamati wao binafsi na endapo watashindwa kuhudhuria kutokana na ugonjwa au kutokuwepo ndani ya Tanzania, watateua Maafisa Waandamizi kuhudhuria kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 30 kinafanyiwa marekebisho ili kumwezesha Waziri wa Fedha kukasimu Madaraka yake ya upokeaji Misaada kwa Mawaziri wengine na Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 30A kimeongezwa ili kubainisha adhabu kwa Wakuu wa Taasisi za Umma pindi watakapochukua mikopo bila kupata ridhaa ya Waziri wa Fedha. Aidha, kupitia marekebisho haya, Wakuu wa Taasisi za Umma watakaoshindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa na Serikali watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Vilevile Mtumishi mwingine yeyote wa Umma atakayekiuka masharti ya Sheria atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178. Marekebisho haya yanakusudia kuruhusu wanafunzi wa Stashahada na Astashahada katika fani ambayo Waziri ataamua ili kupata mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Marekebisho haya yanakusudia kurekebisha Kifungu cha 10(3) ili kuruhusu Miradi ya Kimkakati au yenye maslahi ya umma kupata msamaha chini ya Sheria hii endapo kuna Mkataba uliofungwa na Serikali na kupata kibali cha Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113, ambapo Kifungu cha 19 kinarekebishwa ili kuipa Mamlaka ya *EPZ* uwezo wa kuitoa ardhi yake itumiwe na mtu mwingine bila kutoa Hati Miliki. Utaratibu huu utapunguza urasimu unaojitokeza kwa Wawekezaji wakati wa kufuatilia Hati Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220, Kifungu cha tano kifanyiwe marekebisho ili kuongeza Vifungu vipya vya 5A na 5B ambavyo vinaipa Mamlaka Bodi ya kukasimu baadhi ya kazi zake kwenye Kamati. Vile vile, Bodi imepewa Mamlaka ya kutengeneza Miongozo na kuweza kuteua Mjumbe yeyote kuhudhuria kwenye vikao vyake, lakini Mjumbe huyo aliyechaguliwa hatakuwa na haki ya kupiga kura. Kifungu cha 14 nacho kinarekebishwa kwa kukataza Wafanyakazi wa Mfuko wasiweze kutumia vibaya fedha zozote zinazowekwa kwenye Mfuko. Vile vile, Sehemu hii inaainisha mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251. Sehemu hii inakusudia kurekebisha Kifungu cha nne ili kuipa Bodi mamlaka ya kuomba na kupewa Mpango wa Maendeleo wa Wamiliki wa Viwanda vya Sukari kwa lengo la kuwezesha ufuatiliaji, usimamizi na kuifanyia tathmini Mipango ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii pia inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 7A na 7B kwa lengo la kuuboresha mfumo wa wakulima wadogo ili kuongeza ufanisi wa faida katika biashara ya sukari, kuboresha uwezo wa kufanya majadiliano ya mikataba pamoja na ununuzi wa miwa. Kuweka uwezo katika usimamizi na kuondoa ubadhirifu wa mali za wakulima wadogo zinazomilikiwa kwa pamoja. Vifungu vipya vinavyopendekezwa vitaiwezesha Bodi na Serikali kufuatilia utendaji kazi wa wakulima pamoja na mali zao. Vifungu vipya pia vinapendekeza uanzishwaji wa Baraza la Majadiliano kwa lengo la kuratibu shughuli za Umoja wa Wakulima Wadogo wa Miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa pia kuongeza Kifungu kipya cha 11A kinachoipa Bodi mamlaka ya kutoa bei elekezi ya miwa na sukari ili kuhakikisha Wakulima Wadogo wa Miwa wanapata bei inayoendana na soko kwa miwa wanayoiuza viwandani. Kifungu pia kinalenga kuipa bodi mamlaka ya kuwalinda watumiaji wa sukari na pia kuhakikisha kwamba viwanda vya miwa vinapata faida. Aidha, inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 17 kinachotoa wajibu wa wamiliki wa viwanda vya sukari kuwasilisha kwenye bodi mipango yao ya maendeleo ya upanuzi wa viwanda ili bodi iweze kufuatilia utendaji kazi wa viwanda vya miwa. Kifungu hiki pia kinapendekeza kuweka adhabu kwa mtu atakayekiuka masharti yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 34 kinachoweka kipindi cha mpito wa miezi sita ili kutoa muda wa shughuli za uchanganyaji wa sukari zilizokuwa zikifanyika kabla ya kifungu hiki kuanza kutumika. Pia kinatoa adhabu kwa mtu atakayekiuka masharti ya Kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane ya Muswada inafanya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283. Kifungu cha 101 cha Muswada kinarekebishwa kwa kuruhusu Mahakama, kwa maombi au ridhaa yake, kupokea ushahidi wa vitu vinavyooza kwa haraka, vinavyoharibika au kushuka thamani kabla au baada ya kuanza kwa shauri ili iwe ni uthibitisho wa suala linalogombaniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Jumla wa Muswada. Kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 na Sekretariati ya Kamati, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada wa Sheria kwa kupitia Vifungu vyote 45 vya Muswada tarehe 17/1/2017. Baada ya kufanya mapitio ya Vifungu vyote na kujiridhisha na Malengo na Madhumuni ya Sheria zinazobadilishwa katika Muswada huu, Kamati ilipokea hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 18/1/2017 ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu sababu za mapendekezo ya Mabadiliko haya ya Sheria kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 na 20 Januari 2017 Kamati ilikutana na Wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Taasisi za Elimu ya Juu, Vikundi vya Wakulima, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi ili kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kitaalam wa Sheria mbalimbali zinazofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maoni ya wadau, Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Kamati iliyapokea baadhi ya maoni ya wadau na kuyaacha mengine kwa sababu mbalimbali. Tarehe 24/1/2017 Kamati ilikutana na Mtoa hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kumpa nafasi ya kujibu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi iliofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikubaliana na mapendekezo ya Kamati, lakini pia, yapo maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakukuwa na masuala yoyote yaliyoibua hoja za msingi kati ya Kamati na Serikali katika vifungu vya 1, 2, 3, 7, 8, 10, 11, 15, 16, 17, 18, 19, 20, 21, 22 mpaka 29, 30, 31 mpaka vifungu vya 43 na 44. Baadhi ya hivi Vifungu ni vya Muundo zaidi *(Construction Provisions)* na havina madhara katika Maudhui ya Muswada na baadhi ya vifungu ni vya kimaudhui lakini visivyo na madhara katika kuathiri Malengo na Madhumuni ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kupitia kifungu kwa kifungu na baada ya kupokea na kuchambua madhumuni na malengo ya Muswada huu Kamati inakubaliana na kuunga mkono marekebisho ya sheria mbalimbali katika Muswada huu na hatua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa maelezo na ufafanuzi wa ziada wa baadhi ya maeneo ya Muswada kulisaidia Kamati kuwa na uelewa mpana kuhusu Muswada huu na kuiunga mkono Serikali, lakini yapo maeneo ambayo yalikinzana kati ya Serikali na Kamati ambayo baadaye yaliwekwa sawa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na masuala ya dhima *(content)* Kamati pia ilifanya uchambuzi wa *form (muundo)* na usahihi wa kisarufi wa maneno yaliyotumika katika Muswada huu. Yapo makosa machache ya kisarufi na kiuandishi yalionekana katika uandishi wa Muswada na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliahidi kuyafanyia kazi katika Jedwali la Marekebisho. N ilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishafanya marekebisho husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Ibara ya 19(3) ya Muswada huu badala ya kutumika neno "*Absent*" Kamati iliishauri Serikali neno "*Absence*" litumike ili sentensi isomeke katika muundo sahihi wa kisarufi. Katika Ibara ya 14, Kifungu kipya cha 12A(2)(a) badala ya neno "*demonstrate*" litumike neno "*demonstrates*" kwa ajili ya usahihi wa kisarufi wa sentensi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 40, Kifungu kipya cha 7(A)(1) Kamati ilipendekeza katika sentensi inayosomeka "*as a co-operative societies*" neno "*a*" liondolewe na sentensi isomeke "*as co-operative societies*". Makosa ya kisarufi na kiuandishi kama haya yameonekana katika baadhi ya maeneo ya Muswada na Kamati imeshauri yafanyiwe marekebisho ili Sheria iwe katika muundo sahihi wa kisarufi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura ya 134, Kamati inashauri kwamba maslahi ya

Zanzibar katika mikopo yazingatiwe kwa upana pale Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapochukua Mkopo kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika kutekeleza suala hili Kamati ilishauri mamlaka zinazohusika kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zifanye kazi kwa ukaribu kwa faida ya kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura 178, Kamati iliunga mkono marekebisho ya sheria hii kwa sababu itatoa nafasi kwa Watanzania wengi wa kipato cha chini kupata nafasi ya kusoma katika vyuo vya elimu ya juu. Kamati inakubaliana na mtazamo wa Serikali kwamba utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ajili ya ngazi ya Diploma utazingatia vipaumbele vya Taifa kulingana na wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya Sheria ya Mikopo yanayopendekezwa, Kamati ilihitaji ufafanuzi wa kitaalam kutoka kwa Waziri Mwenye dhamana, uwepo wa wanafunzi wa "*Higher Diploma*" katika vyuo na taasisi za elimu ya juu ya ufundi hapa Tanzania na kama mabadiliko yataongeza wigo wa wanafunzi wengi kupata mikopo kwa ajili ya kada ya kati. Kamati ilifahamishwa kwamba mpaka sasa ni Vyuo vya Ualimu Korogwe, Songea na Monduli ndio vinavyotoa mafunzo ya kiwango cha *Higher Diploma*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Kamati iliona kwamba marekebisho haya ya sheria yanaendana na malengo na mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Mikopo yaliyofanyika mwaka 2014 ambayo yalikuwa na lengo la kuongeza kiwango cha Elimu ya *Higher Diploma* yaani Astashahada ili wanafunzi wengi wapate mkopo kwa elimu ya juu na ufundi. Marekebisho haya yanaendana na malengo ya Sera ya nchi ya kuchukua jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu ya mafunzo ya ufundi kwa ngazi zote za shule na vyuo vinginevyo vya mafunzo, kwa mujibu wa Ibara ya 11(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pamoja na Serikali zimekubaliana kwamba Kifungu cha 25(c) kinachopendekezwa katika Sheria ya Bodi ya Mikopo kibaki kama kilivyo na kibebe maudhui yaliyomo ndani yake. Hata hivyo Kamati inashauri kwamba neno "*Higher Diploma*" lisitumike tena na badala yake liendelee kutumika neno "*Diploma*" ili kuondoa mkanganyiko wa maana ambao umekuwa unajitokeza mara kwa mara. Nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mabadiliko haya tayari yameshafanywa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Marekebisho ya Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220, Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kutekeleza Sheria hii kwa uangalifu kwa sababu zipo Mamlaka za Serikali ambazo zinaendelea kutoza tozo za mafuta ambayo tayari yameshalipiwa. Kamati iligundua kwamba wadau wa sekta ya usafirishaji wa mafuta hawakushirikishwa kwa kiwango cha kutosha katika marekebisho ya sheria hii. Kamati ilitoa rai kwa Serikali kuchukua hatua za kutosha kuwashirikisha Wadau wote ipasavyo kuhusu kiini cha marekebisho ya sheria hii na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwa kuwa, Serikali yetu hii sikivu ilisikia maoni haya ya Kamati. Niseme tu kwamba, kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya nane pamoja na Ibara ya 21 ambayo Wananchi wa Tanzania wana nafasi ya kushiriki katika shughuli ya Serikali, kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa Kikatiba, Sera hii ni muhimu sana katika mchakato wa sheria zote zinazopitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilitaarifu Bunge lako Kamati iliona kabisa kuendelea na Sehemu hii ya Sita ya Muswada tutakiuka Kanuni ya 84(1) mpaka ya (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika marekebisho yaliyopendekezwa katika Sheria ya Tozo ya Barabara na Mafuta, Sura ya 220, Kamati iligundua kwamba wadau hawakushirikishwa vya kutosha katika mapendekezo haya. Kwa wadau kutoka Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania *(TATOA)* na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania *(TABOA)* ambao walitoa maoni yao mbele ya Kamati, lakini pia hawakuelewa suala ambalo waliitiwa mbele ya Kamati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue Kanuni ya 18 ya Kanuni za Uongozi zilizowahi kutolewa na Professa Maxwell, "*The Law of Sacrifice*" ambayo inasema kwamba, *a leader must give up to go up.* Serikali iliitikia wito wa Kamati na iliafikiana na Kamati kuondoa sehemu hii ya sita ili iweze kujipanga vizuri kukaa na wadau na kushauriana nao ili sheria hii iweze kutungwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Kanuni za Kudumu za Bunge pamoja na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ulio bora wa Utungaji Sheria kwa Tanzania pamoja na Duniani kwa ujumla unahitaji wananchi washirikishwe katika Utungaji wa Sheria na Utengenezaji wa Sera za nchi. Kama nilivyosema Ibara ya nane kwamba, nchi ni ya wananchi. Kwa msingi huu Kamati inaishauri serikali kusitisha kwanza mchakato wa Marekebisho ya Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali

imeitikia wito wa Kamati na tayari Sehemu hii ya Sita ya Muswada imeondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kutokana na uchambuzi huu, Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Pili ya Muswada, Kamati inashauri kwamba katika suala la ukopaji, maslahi ya pande zote mbili za Muungano yazingatiwe; yaani Zanzibar ipewe uhuru mkubwa wa kukopa kwa kadri ya uwezo wake wa kulipa kwa mujibu wa Sheria na taratibu zinazotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri neno "*Resident Sources*" kama lilivyotumika katika Kifungu cha nne cha Muswada lipewe tafsiri ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza katika matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 5(b) Kamati inashauri matumizi ya neno *''Stock''* yaendelee kama ilivyo katika Sheria Mama kwa sababu ni moja kati ya dhamana zinazotumika katika mikopo ya Serikali. Neno hili ni la Kitaalam na Kamati inashauri kwamba lisifutwe katika sheria mama maana limebeba kiini na maudhui ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha tisa cha Muswada inapendekezwa kuongeza Kifungu kidogo cha (2) katika Kifungu cha saba cha sheria mama. Baada ya kufanya mapitio ya sheria mama na kujielekeza katika kifungu cha saba, Kamati iligundua kwamba hakuna kifungu kidogo chochote katika Kifungu cha saba cha sheria mama. Kamati inaamini kwamba hili ni kosa la kitaalam na inaishauri Serikali kutazama tena pendekezo hili na kujiridhisha nalo au kubadilisha kabisa pendekezo hili na kuliweka katika namna bora iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 14 cha Muswada, Kamati inashauri litumike neno *''any other public body corporate''* badala ya neno *''any other body corporate''* ili kuondoa utata wa kisheria unaoweza kujitokeza kuhusu kampuni au taasisi gani ilikusudiwa na sheria hii kati ya zile za binafsi au za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati inaunga mkono marekebisho yote ya sheria yaliyomo sehemu ya tatu (Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178), sehemu ya nne (Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332) na sura ya tano inayohusu marekebisho yanayohusu Sheria ya Ardhi,

Sura ya 113. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za kutosha kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Sheria hizi na kila mara inapokuwa na kusudio la kufanya marekebisho ya sheria yanayogusa sekta binafsi kuishirikisha sekta binafsi Tanzania ili kubeba maslahi ya watu na taasisi zilizo katika sekta binafsi kama vile biashara, viwanda na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikupata sababu za msingi za Serikali kuongeza viwango vya tozo za mafuta barabarani. Baada ya kuwasikiliza Wadau na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu nia ya kufanya marekebisho ya Sheria hii, Kamati inashauri Serikali kusitisha pendekezo hili kama nilivyosema hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada inayopendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Sekta ya Sukari, Sura ya 251 iliibua maswali mengi sana yaliyohitaji ufafanuzi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kipya cha saba katika Muswada huu kinataka Vyama vya Wakulima wa Miwa kupata kwanza idhini ya Bodi ya Sukari kabla ya kusajiliwa kama Vyama vya Ushirika chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013. Kamati inashauri hitaji la kupata idhini ya Bodi ya Sukari katika Kifungu hiki liondolewe kwani siyo utaratibu sahihi na ufuate utaratibu uliowekwa katika vyama vya ushirika. Haki ya kuanzisha Vyama vya Ushirika ni haki ya kikatiba ambayo inaruhusu watu kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza maslahi yake kwa mujibu wa Ibara ya 20(1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kipya cha 7(4) cha Muswada kinaipa Bodi mamlaka ya kupanga kiwango au kiasi cha sukari cha kila siku kinachotakiwa kutolewa na kila Chama cha Ushirika chini ya sheria hii. Kamati imeona kwamba kifungu hiki kinatoa mamlaka makubwa kwa bodi peke yake kupanga kiwango hiki cha sukari inayozalishwa kila siku na vyama vya ushirika vya miwa. Kamati inashauri kwamba upangaji wa viwango hivi ushirikishe bodi, wazalishaji na wakulima wa miwa wadogo wadogo kwa pamoja ili wadau wote wa sekta hii wahusishwe yaani *''Tripartite arrangement''* katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 41, kifungu kipya cha 11A kinachopendekezwa, bodi inapewa mamlaka, baada ya kushauriana na Waziri, kupanga bei elekezi ya sukari au mazao yatokanayo na sukari. Kamati inashauri kwamba upangaji wa bei hizi elekezi uwashirikishe wadau wote katika

sekta hii hasa vyama vya wakulima wadogo wadogo na wazalishaji wote wa miwa kwa kushauriana na bodi pamoja na Waziri mwenye dhamana. Jukwaa la wakulima wa miwa lililoanzishwa na kifungu kipya cha saba cha Muswada litumike pia katika mashauriano ya upangaji bei elekezi za sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 42, kifungu kipya cha 17(3) cha Muswada, bodi inapewa mamlaka ya kusimamisha au kufuta leseni zote za uzalishaji wa sukari kama amevunja matakwa ya Sheria ya Sukari. Kamati inashauri kwamba kifungu hiki kiboreshwe ili kutoa nafasi ya mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya bodi akate rufaa kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na sekta hii na kama hajaridhika pia awe na uwezo wa kukata rufaa katika Mahakama Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 45 cha Muswada kinafanya marekebisho katika Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283. Kifungu hiki kinakusudia kuruhusu Mahakama, kwa maombi au kwa ridhaa yake, kupokea ushahidi wa vitu vinavyooza haraka, vinavyoharibika au kushuka thamani kabla au baada ya kuanza kwa shauri ili iwe ni uthibitisho wa suala linalogombaniwa. Kifungu hiki kinakusudia kumpa Mkurugenzi wa Wanyamapori uwezo wa kutunza vitu vilivyotajwa katika Kifungu cha 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majadiliano mapana kati ya Serikali na Kamati, imeonekana kuwa ni vema Kifungu hiki kikatazamwa upya ili kuondoa hatari ya kusababisha makosa makubwa katika usimamiaji haki hapa Tanzania. Serikali imeahidi kuboresha kifungu hiki na kukiweka katika jedwali la marekebisho. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya marekebisho ya kifungu hiki na sasa kinasomeka vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yaliyotolewa na Kamati katika Muswada huu yamezingatia kwa kina maoni ya wadau, uchambuzi wa kitaalam uliofanywa na Sekretariati ya Bunge pamoja na majadiliano mapana kati ya Serikali na Kamati. Hivyo Kamati inaamini kwamba Sheria hii itakuwa bora na yenye manufaa kwa Tanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; nakushukuru wewe binafsi kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Masaju Mbunge, kwa ushirikiano wake wakati wa

kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na wajumbe waalikwa kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha muswada huu. Naomba yao yote yaingie katika *hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni na ushauri wao katika Muswada huu ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii. Naomba kutambua mchango wa Wadau mbalimbali wakiwemo *Tanganyika Law Society,* Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania *(TABOA),* Chama cha Wamiliki wa Malori *(TATOA),* Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA),* Mtandao wa Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria Tanzania, Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania, Jumuiya ya Wakristo Tanzania *(CCT),* Sekretarieti ya Msaada wa Sheria, Chuo Kikuu cha Dodoma, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Chuo cha Elimu ya Biashara, Tawi la Dodoma pamoja na Taasisi ya Uwezeshaji wa Misaada wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Masaidizi Ndugu Angelina Sanga, Mkurugenzi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndugu Pius Mboya, Wakurugenzi Wasaidizi Ndugu Mossy Lukuvi na Ndugu Prudence Rweyongeza, Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndugu Stella Bwimbo, Ndugu Dunford Mpelumbe, Wanasheria wa Bunge Ndugu Leocardo Kapongwa, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Mariam Mbarouk na msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA**

**YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI, (NA. 4) WA MWAKA 2016, [THE *WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, NO. 4 OF 2016]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI:

**1.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2016 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Act of 2016].

**1.2 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu Mwezi Novemba, 2016 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 10 Novemba 2016 ili iufanyie kazi, na tarehe 18 Januari, 2017, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu Malengo na Madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho katika Sheria Saba (7) mbalimbali kwa Madhumuni ya kuondoa mapungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho ni:

i) Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura ya 134
ii) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178;
iii) Kodi ya Mapato, Sura ya 332
iv) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113
v) Sheria ya Barabara na Tozo za Mafuta, Sura ya 220
vi) Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251
vii) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

**1.4 Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**1.5 Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Serikali Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja

na Wataalamu mbalimbali wa Wizara na Taasisi za Serikali zinazosimamia utekelezaji wa Sheria zinazofanyiwa marekebisho hayo.

**1.6 Mheshimiwa Spika**, Kamati pia iliona kuna umuhimu mkubwa, Kama ilivyo katika uendeshaji wa shughuli za Bunge lako Tukufu, kupokea na kuchambua maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kabla ya Muswada huu kusomwa Bungeni kwa mara ya Pili. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ilipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mhe.Tundu Lissu ambaye alihudhuria vikao vya uchambuzi wa Muswada huu kama Mjumbe Mwalikwa.

## 2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Katiba na Sheria inapenda kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu maelezo ya jumla ya Muswada ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati kwa kushirikiana na Idara ya Kamati za Bunge na Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Maelezo haya ya jumla yanaelezea malengo na madhumuni ya mabadiliko ya kila Sheria ambayo inaguswa na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane, kama ifuatavyo:-

## 2.1 SEHEMU YA KWANZA YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

## 2.2 SEHEMU YA PILI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 kwa kurekebisha Kifungu cha 2 ili kubainisha tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika ndani ya hiyo Sheria. Lengo la marekebisho hayo ni kurahisisha utekelezaji wa Sheria hiyo. Aidha, Kifungu cha 3, 6, 8, 10 na 13A (2) vinafanyiwa marekebisho ili kuweka sharti kwa Waziri wa Fedha kushauriwa na Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa kabla ya kufanya uamuzi wa kukopa pamoja na kuweka utaratibu kwa Serikali kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Sehemu hii pia inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7 ili kumpa uwezo Waziri wa Fedha kukasimu Mamlaka yake kwa Gavana wa Benki Kuu kuhusu kukopa

ndani ya nchi kupitia Amana za Serikali zinazotolewa na Benki Kuu. Vilevile, Sehemu hii inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 12 ili kuweka utaratibu kwa Serikali kuzikopesha kwa utaratibu maalum, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi za Umma pindi Serikali inapochukua mikopo kwa niaba yao, ambapo marekebisho husika yamebainisha taratibu zitakazotumika na Taasisi husika katika kurejesha mikopo hiyo.

Kifungu cha 12A na 12B vimeongezwa ili kuweka sharti kwa Wizara nyingine na Taasisi za Serikali ambazo zinaruhusiwa kwa mujibu wa Sheria nyingine kukopa, kupata idhini ya Waziri wa Fedha kabla ya kukopa.

Marekebisho ya Kifungu cha 13 kwanza, yana lengo la kumpa Mamlaka Waziri wa Fedha kuandaa Kanuni zitakazobainisha ada ya dhamana ambayo itatozwa kwa kiwango cha Mkopo ili kuiwezesha Serikali kukabiliana na athari zitakazojitokeza kwa dhamana iliyotolewa na kupunguza idadi ya wakopeshaji wanaoomba dhamana ya Serikali.

Pili kuweka utaratibu ili dhamana itakayotolewa na Serikali iwe ni kwa ajili ya Mikopo pekee bila kujumuisha gharama nyingine za mkopo na,

Tatu kumpa Mamlaka Waziri wa Fedha kutoa na kusimamia dhamana zitakazotolewa kwenye Miradi ya Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi.

Vilevile, inapendekezwa kurekebisha Kifungu 13A ili kuweka sharti kwamba Mkopo utakaochukuliwa kwa dhamana ya Serikali utumike kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi yenye uwezo wa kuzalisha mapato ya kulipia deni na gharama ya Mkopo. Aidha, kupitia marekebisho husika Waziri atatoa dhamana itakayofikia asilimi 85 kwenye masuala yanayohusu majanga ya Kitaifa kama mafuriko, tetemeko la ardhi n.k na hivyo kuondoa utata uliopo hivi sasa kuhusu mazingira ambayo Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana zaidi ya asilimia 70.

Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuipa majukumu Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa kumshauri Waziri wa Fedha katika kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Madeni ikiwemo mpango wa ukopaji wa Serikali kwa mwaka na kusimamia masuala yote yanayohusu usimamizi wa madeni, dhamana na misaada.

Kifungu cha 18 kinafanyiwa marekebisho ili kumuongeza Katibu wa Tume ya Mipango - Zanzibar kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya kusimamia Deni la Taifa. Vilevile, kupitia marekebisho katika Kifungu hiki, Kamati imepewa uwezo

wa kujumuisha Mjumbe mwingine yeyote pale itakapoona kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Kifungu cha 22 kinafanyiwa marekebisho ili kubainisha akidi ya vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa ambayo itakuwa ni nusu ya Wajumbe wa Kamati na kuweka sharti kwa Wajumbe kuhudhuria vikao vya Kamati wao binafsi, na endapo watashindwa kuhudhuria kutokana na ugonjwa au kutokuwepo ndani ya Tanzania, watateua Maafisa Waandamizi kuhudhuria kwa niaba yao.

Kifungu cha 30 kinafanyiwa marekebisho ili kumuwezesha Waziri wa Fedha kukasimu Madaraka yake ya upokeaji Misaada kwa Mawaziri wengine na Makatibu Wakuu.

Kifungu cha 30A kimeongezwa ili kubainisha adhabu kwa Wakuu wa Taasisi za Umma pindi watakapochukua mikopo bila kupata ridhaa ya Waziri wa Fedha. Aidha, kupitia marekebisho haya, Wakuu wa Taasisi za Umma watakaoshindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa na Serikali watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Vilevile Mtumishi mwingine yeyote wa Umma atakayekiuka masharti ya Sheria atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

## 2.3 SEHEMU YA TATU YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178. Marekebisho haya yanakusuidia kuruhusu Wanafunzi wa Stashahada na Astashahada katika Fani ambayo Waziri ataamua ili kupata mikopo inayotolewa kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa.

## 2.4 SEHEMU YA NNE YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Marekebisho haya yanakusudia kurekebisha Kifungu cha 10(3) ili kuruhusu Miradi ya Kimkakati au yenye Maslahi ya Umma kupata msamaha chini ya Sheria hii endapo kuna Mkataba uliofungwa na Serikali na kupata kibali cha Baraza la Mawaziri.

## 2.5 SEHEMU YA TANO YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113, ambapo Kifungu cha 19

kinarekebishwa ili kuipa Mamlaka ya EPZ uwezo wa kuitoa ardhi yake itumiwe na Mtu mwingine bila kutoa Hati Miliki. Utaratibu huu utapunguza urasimu unaojitokeza kwa Wawekezaji wakati wa kufuatilia Hati Wizara ya Ardhi.

## 2.6 SEHEMU YA SITA YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220. Kifungu cha 5 kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza Vifungu vipya vya 5A na 5B ambavyo vinaipa Mamlaka Bodi ya kukasimisha baadhi ya kazi zake kwenye Kamati. Vile vile, Bodi imepewa Mamlaka ya kutengeneza Miongozo na kuweza kuteua Mjumbe yeyote kuhudhuria kwenye vikao vyake lakini Mjumbe huyo aliyechaguliwa hatakuwa na haki ya kupiga kura. Kifungu cha 14 nacho kinarekebishwa kwa kukataza Wafanyakazi wa Mfuko wasiweze kutumia vibaya fedha zozote zilizowekwa kwenye Mfuko. Vile vile, Sehemu hii inaainisha Mtu yeyote atakayokiuka masharti ya Sheria hii.

## 2.7 SEHEMU YA SABA YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251. Sehemu hii inakusudia kurekebisha Kifungu cha 4 ili kuipa Bodi Mamlaka ya kuomba na kupewa Mpango wa Maendeleo wa Wamiliki wa Viwanda vya Sukari kwa lengo la kuwezesha ufuatiliaji, usimamizi na kuifanyia tathmini Mipango ya Maendeleo.
Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 7A na 7B kwa lengo la kuuboresha Mfumo wa Wakulima wadogo ili kuongeza ufanisi na faida katika Biashara ya Sukari, kuboresha uwezo wa kufanya majadiliano ya Mikataba ya Ununuzi wa miwa. Kuweka uwazi katika usimamizi na kuondoa ubadhirifu wa mali za Wakulima wadogo zinazomilikiwa kwa pamoja. Vifungu vipya vinavyopendekezwa vitaiwezesha Bodi na Serikali kufuatilia utendaji kazi wa Wakulima wadogo pamoja na mali zao. Vifungu vipya pia vinapendekeza uanzishwaji wa Baraza la Majadiliano kwa lengo la kuratibu shughuli za Umoja wa Wakulima wadogo wa Miwa.

Inapendekezwa pia kuongeza Kifungu kipya cha 11A kinachoipa Bodi Mamlaka ya kutoa bei elekezi ya Miwa na Sukari ili kuhakikisha Wakulima wadogo wa Miwa wanapata bei inayoendana na Soko kwa Miwa wanayoiuza Viwandani. Kifungu pia kinalenga kuipa Bodi Mamlaka ya kuwalinda watumiaji wa Sukari na pia kuhakikisha kwamba Viwanda vya Miwa vinapata faida. Aidha, inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 17A kinachotoa wajibu kwa Wamiliki wa Viwanda vya Sukari kuwasilisha kwenye Bodi Mipango yao ya Maendeleo na upanuzi wa Viwanda ili Bodi iweze kufuatilia utendaji kazi wa

Viwanda vya Miwa. Kifungu hiki kipya pia kinapendekeza kuweka adhabu kwa Mtu atakayekiuka masharti yaliyowekwa.

Mwisho, Sehemu hii pia inapendekeza kuongea Kifungu kipya cha 34A kinachoweka kipindi cha mpito cha Miezi Sita ili kutoa muda kwa shughuli za uchanganyaji wa Sukari zilizokuwa zikifanyika kabla ya Kifungu hiki kuanza kutumika. Pia kinatoa adhabu kwa Mtu atakayekiuka masharti ya Kifungu hiki.

## 2.8 SEHEMU YA NANE YA MUSWADA

Sehemu ya Nane ya Muswada inafanya marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283. Kifungu cha 101 cha Muswada kinarekebishwa kwa kuruhusu Mahakama, kwa maombi au ridhaa yake, kupokea ushahidi wa vitu vinavyooza kwa haraka, vinavyoharibika au kushuka thamani kabla au baada ya kuanza kwa shauri ili iwe ni uthibitisho wa suala linalogombaniwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

**3.1 Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana kwa Karibu na Idara ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016 na Sekretariati ya Kamati, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa Sheria kwa kupitia Vifungu vyote **45** vya Muswada tarehe **17/1/2017**. Baada ya kufanya mapitio ya Vifungu vyote na kujiridhisha na Malengo na Madhumuni ya Sheria zinazobadilishwa katika Muswada huu, Kamati ilipokea hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe **18/1/2017** ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu sababu za mapendekezo ya Mabadiliko haya ya Sheria kwa wakati huu.

**3.2 Mheshimiwa Spika**, tarehe **19 na 20 Januari 2017** Kamati ilikutana na Wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Taasisi za Elimu ya Juu, Vikundi Vya Wakulima, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi ili kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa Kitaalamu wa Sheria mbalimbali zinazofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

**3.3 Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maoni ya Wadau, Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya Wadau kwa kina ili kujiridhisha na Maudhui yake. Kamati iliyapokea baadhi ya maoni ya wadau na kuyaacha mengine kwa sababu mbalimbali. Tarehe **24/1/2017** Kamati ilikutana na Mtoa hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kumpa nafasi kujibu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi iliofanya.

**3.4 Mheshimiwa Spika**, yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikubaliana na Mapendekezo ya Kamati, yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

**3.5 Mheshimiwa Spika**, hakukua na masuala yoyote yaliyoibua hoja za Msingi kati ya Kamati na Serikali katika Vifungu vya **1,2,3,7,8, 10, 11, 15, 16,17, 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 26, 27, 28, 29, 30,31, 32, 33, 36, 37, 38, 39, 42, 43 na 44** . Baadhi ya hivi Vifungu ni vya Muundo zaidi (Construction Provisions) na havina madhara katika Maudhui ya Muswada na baadhi ya Vifungu ni vya Kimaudhui lakini visivyo na madhara katika kuathiri Malengo na Madhumuni ya Muswada.

**3.6 Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kupitia Kifungu kwa kifungu na baada ya kupokea na kuchambua Madhumuni na Malengo ya Muswada huu Kamati inakubaliana na kuunga Mkono Marekebisho ya Sheria mbalimbali katika Muswada huu. Hatua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa maelezo na ufafanuzi wa ziada wa baadhi ya maeneo ya Muswada kulisaidia Kamati kuwa na uelewa mpana kuhusu Muswada huu na kuiunga mkono Serikali.

**3.7 Mheshimiwa Spika**, pamoja na masuala ya Dhima (Content) Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Form ( Muundo) na Usahihi wa Kisarufi wa Maneno yaliyotumika katika Muswada huu. Yapo makosa machache ya Kisarufi na Kiuandishi yalionekana katika Uandishi wa Muswada (Typo and grammatical errors) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeahidi kuyafanyia kazi katika Jedwali la Marekebisho.

**3.8 Mheshimiwa Spika**, kwa mfano katika Ibara ya **19(3)** ya Muswada huu badala ya kutumika neno ''**Absent''** Kamati inashauri litumike neno ''**Absence**'' ili sentensi isomeke katika Muundo sahihi wa Kisarufi. Katika Ibara ya **14**, Kifungu kipya cha **12A (2)(a)** badala ya neno **''demonstrate''** litumike neno ''**demonstrates**'' kwa ajili ya usahihi wa Kisarufi wa sentensi. Katika Ibara ya 40, Kifungu kipya cha 7(A) (1) Kamati inapendekeza katika sentesi inayosomeka ''**as a co-operative societies''** neno **''a''** liondolewe na sentensi isomeke ''**as co-operative societies''**. Makosa ya Kisarufi na kiuandishi kama haya yameonekana katika baadhi ya maeneo ya Muswada na Kamati imeshauri yafanyiwe marekebisho ili Sheria iwe katika Muundo sahihi wa Kisarufi.

**3.9 Mheshimiwa Spika**, katika Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura ya 134 Kamati inashauri kwamba Maslahi ya Zanzibar katika

Mikopo yazingatiwe kwa upana wake pale Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inapochukua Mikopo kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika kutekeleza suala hili Kamati inashauri Mamlaka zinazohusika kwa upande wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zifanye kazi kwa ukaribu kwa faida ya kila upande.

**3.10 Mheshimiwa Spika**, katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura 178, Kamati inaunga mkono marekebisho ya Sheria hii kwa sababu itatoa nafasi kwa Watanzania wengi wa kipato cha chini kupata nafasi ya kusoma katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Kamati inakubaliana na Mtazamo wa Serikali kwamba utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ajili ya ngazi ya Diploma utazingatia vipaumbele vya Taifa kulingana na wakati husika.

**3.11 Mheshimiwa Spika**, katika marekebisho ya Sheria ya Mikopo yanayopendekezwa, Kamati ilihitaji ufafanuzi wa Kitaalamu kutoka kwa Waziri Mwenye Dhamana kuhusu uwepo wa Wanafunzi wa **''Higher Diploma''** katika Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu na Ufundi hapa Tanzania na kama mabadiliko haya yataongeza wigo wa Wanafunzi wengi kupata Mikopo kwa ajili ya Kada za kati. Kamati ilifahamishwa kwamba mpaka sasa ni Vyuo vya Ualimu Korogwe, Songea na Monduli ndio vinavyotoa mafunzo kwa kiwango cha Higher Diploma (Astashahada).

**3.12 Mheshimiwa Spika**, Baada ya kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati iliona kwamba marekebisho haya ya Sheria yanaendana na Malengo ya Mabadiliko ya Sheria ya Bodi ya Mikopo yaliyofanyika Mwaka 2014 ambayo yalikuwa na lengo la kuongeza kiwango cha Elimu ya **Higher Diploma** yani Astashahada ili Wanafunzi wengi wapate Mkopo wa Elimu ya Juu na Ufundi. Marekebisho haya yanaendana na Malengo na Sera ya nchi ya kuchukua jitihada kuhakikisha kwamba Watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika ngazi zote za Shule na Vyuo vinginevyo vya Mafunzo kwa mujibu wa **Ibara ya 11(3)** ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**3.13 Mheshimiwa Spika**, Kamati pamoja na Serikali zimekubaliana kwamba Kifungu cha 25(c) kinachopendekezwa katika Sheria ya Bodi ya Mikopo kibaki kama kilivyo na kibebe Maudhui yaliyomo ndani yake. Hata hivyo Kamati inashauri kwamba neno ''Higher Diploma'' lisitumike tena na badala yake liendelee kutumika neno ''Diploma'' ili kuondoa mkanganyiko wa maana ambao umekua unajitokeza mara kwa mara.

**3.14 Mheshimiwa Spika**, katika Marekebisho ya Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220, Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kutekeleza Sheria hii kwa uangalifu kwa sababu zipo Mamlaka za Serikali ambazo zinaendelea kutoza Tozo za Mafuta ambayo tayari yameshalipiwa. Kamati ilibaini kuwa Wadau wa Sekta ya Usafirishaji na Mafuta hawakushirikishwa kwa kiwango cha kutosha katika marekebisho ya Sheria hii. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuchukua hatua za kutosha kuwashirikisha Wadau wote ipasavyo kuhusu kiini cha marekebisho ya Sheria hii na utekelezaji wake.

**3.15 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya **8 (d)** na **21(2)** Wananchi wa Tanzania wana nafasi ya kushiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa Kikatiba. Sera hii ni muhimu sana katika mchakato wa Sheria zote zinazopitishwa na Bunge hili. Katika marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220, Kamati iligundua kwamba Wadau hawakushirikishwa vya kutosha katika mapendekezo haya. Kwa wadau kutoka Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) ambao walitoa maoni yao mbele ya Kamati suala hili lilionekana geni kwao na Serikali ilikiri kutowashirikisha Wadau katika suala hili.

**3.16 Mheshimiwa Spika**, utaratibu ulio bora wa Utungaji Sheria kwa Tanzania na Duniani kwa ujumla unahitaji Wananchi washirikishwe katika Utungaji wa Sheria na Utengenezaji wa Sera za nchi. Kwa msingi huu Kamati inaishauri Serikali kusitisha kwanza mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

**4.1 Mheshimiwa Spika,** katika Sehemu ya Pili ya Muswada, Kamati inashauri kwamba katika suala la ukopaji, maslahi ya pande zote mbili za Muungano yazingatiwe na Zanzibar ipewe uhuru mkubwa wa kukopa kwa kadri ya uwezo wake wa kulipa kwa mujibu wa Sheria na taratibu zinazotumika.

**4.2 Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri neno ''Non - Resident Sources'' kama lilivyotumika katika Kifungu cha 4 cha Muswada lipewe tafasiri ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza katika matumizi yake.

Katika Ibara ya 5(b) Kamati inashauri matumizi ya neno ''Stock'' yaendelee kama ilivyo katika Sheria Mama kwa sababu ni moja kati ya Dhamana zinazotumika katika Mikopo ya Serikali. Neno hili ni la Kitaalamu na Kamati

inashauri kwamba lisifutwe katika Sheria Mama maana limebeba Kiini na Maudhui ya Sheria hii.

**4.3 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 9 cha Muswada inapendekezwa kuongeza Kifungu kidogo cha 2 katika Kifungu cha 7 cha Sheria Mama. Baada ya kufanya mapitio ya Sheria Mama na kujielekeza katika Kifungu cha 7, Kamati iligundua kwamba hakuna Kifungu kidogo chochote katika Kifungu cha 7 cha Sheria Mama. Kamati inaamini kwamba hili ni kosa la Kitaalamu na inaishauri Serikali kutazama tena pendekezo hili na kujiridhisha nalo au kubadilisha kabisa pendekezo hili na kuliweka katika namna bora iliyokusudiwa.

**4.4 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 14 cha Muswada, Kamati inashauri litumike neno ''any other **public** body corporate'' badala ya neno ''any other body **corporate''** ili kuondoa utata wa Kisheria unaoweza kujitokeza kuhusu Kampuni au Taasisi gani ilikusudiwa na Sheria hii kati ya zile za Binafsi au za Serikali.

**4.5 Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati inaunga mkono marekebisho yote ya Sheria yaliyomo Sehemu ya Tatu (Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178), Sehemu ya Nne (Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332) na Sura ya Tano inayohusu marekebisho yanayohusu Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za kutosha kuishirikisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Sheria hizi na kila mara inapokua na kusudio la kufanya marekebisho ya Sheria yanayogusa Sekta Binafsi kuishirikisha Sekta Binafsi Tanzania ili kubeba maslahi ya Watu na Taasisi zilizo katika Sekta Binafsi kama vile Biashara, Viwanda na Kilimo.

**4.6 Mheshimiwa Spika**, Kamati haikupata sababu za msingi za Serikali kuongeza viwango vya Tozo za Mafuta Barabarani. Baada ya kuwasikiliza Wadau na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu nia ya kufanya marekebisho ya Sheria hii, Kamati inashauri Serikali kusitisha pendekezo hili kwa muda na kufanya majadiliano mapana na Wadau wote wanaohusika na Sekta ya Usafirishaji na hasa Makampuni ya Mafuta ili marekebisho ya Sheria hii yabebe maslahi ya Watu wote katika Sekta hii. Hivyo, baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, pande zote mbili zilikubaliana sehemu hii isitishwe kwanza mpaka Serikali itakapokaa na Wadau.

**4.7 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Mswada inayopendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Sekta ya Sukari, Sura ya 251 iliibua maswali mengi sana yaliyohitaji ufafanuzi wa Serikali.

**4.8 Mheshimiwa Spika**, Kifungu kipya cha 7A katika Muswada huu kinataka Vyama vya Wakulima wa Miwa kupata kwanza idhini ya Bodi ya Sukari kabla ya kusajiliwa kama Vyama vya Ushirika chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013. Kamati inashauri hitaji la kupata idhini ya Bodi ya Sukari katika Kifungu hiki liondolewe kwani siyo utaratibu sahihi katika Dunia ya Vyama vya Ushirika. Haki ya kuanzisha Vyama vya Ushirika ni haki ya Kikatiba ambayo inaruhusu Watu kujiunga na Vyama au Mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza maslahi yake kwa mujibu wa Ibara ya 20(1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**4.9 Mheshimiwa Spika**, Kifungu kipya cha 7(A) (4) cha Muswada kinaipa Bodi Mamlaka ya kupanga kiwango au kiasi cha Sukari cha kila siku kinachotakiwa kutolewa na kila Chama cha Ushirika chini ya Sheria hii. Kamati imeona kwamba Kifungu hiki kinatoa Mamlaka makubwa kwa Bodi peke yake kupanga kiwango hiki cha Sukari inayozalishwa kila siku na Chama cha Wakulima wa Miwa. Kamati inashauri kwamba upangaji wa viwango hivi ushirikishe Bodi, Wazalishaji na Wakulima wa Miwa kwa pamoja ili Wadau wote wa Sekta hii wahusishwe yaani **''Tripartite arrangement''** katika Sekta hii.

**4.10 Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 41, Kifungu kipya cha 11A kinachopendekezwa, Bodi inapewa Mamlaka, baada ya kushauriana na Waziri, kupanga bei elekezi ya Sukari au mazao yatokanayo na Sukari. Kamati inashauri kwamba upangaji wa bei hizi elekezi uwashirikishe Wadau wote katika Sekta hii hasa Vyama vya Wakulima na Wazalishaji wote wa Miwa kwa kushauriana na Bodi na Waziri Mwenye Dhamana. Jukwaa la Wakulima wa Miwa lililoanzishwa na Kifungu kipya cha 7A cha Muswada litumike pia katika mashauriano ya upangaji bei elekezi za sukari.

**4.11 Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 42, Kifungu kipya cha 17(3) cha Muswada, Bodi inapewa Mamlaka ya kusimamisha au kufuta Leseni ya Mzalishaji wa Sukari kama amevunja matakwa ya Sheria ya Sukari. Kamati inashauri kwamba Kifungu hiki kiboreshwe ili kutoa nafasi ya Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Bodi akate Rufaa kwa Waziri Mwenye Dhamana na Sekta hii na kama hajaridhika pia na maamuzi ya Waziri akate Rufaa Mahakama Kuu ya Tanzania.

**4.12 Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 45 cha Muswada kinafanya marekebisho katika Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283. Kifungu hiki kinakusudia kuruhusu Mahakama, kwa maombi au kwa ridhaa yake, kupokea ushahidi wa vitu vinavyooza haraka, vinavyoharibika au kushuka thamani kabla au baada ya kuanza kwa shauri ili iwe ni uthibitisho wa suala linalogombaniwa. Kifungu hiki

kinakusudia kumpa Mkurugenzi wa Wanyamapori uwezo wa kutunza vitu vilivyotajwa katika Kifungu cha 45.

**4.13 Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano mapana kati ya Serikali na Kamati, imeonekana kuwa ni vema Kifungu hiki kikatazamwa upya ili kuondoa hatari ya kusababisha makosa makubwa katika usimamiaji haki hapa Tanzania. Serikali imeahidi kuboresha Kifungu hiki na kukiweka katika jedwali la marekebisho.

**4.14 Mheshimiwa Spika**, maoni yaliyotolewa na Kamati katika Muswada huu yamezingatia kwa kina maoni ya Wadau, Uchambuzi wa Kitaalamu uliofanywa na Sekretariati ya Bunge pamoja na majadiliano mapana kati ya Serikali na Kamati. Hivyo Kamati inaamini kwamba Sheria hii itakuwa bora na yenye manufaa kwa Tanzania wote.

## 5.0 HITIMISHO

**5.1 Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe binafsi kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**5.2 Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. George Masaju Mb, kwa ushirikiano wake wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Kamati.

**5.3 Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha

**Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa,Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe

9. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, M - Mjumbe
20. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
21. Mhe.Selemani Nchambi, Mb - Mjumbe
22. Mhe.Ussi Pondeza, Mb - Mjumbe
23. Mhe.Tusker Mbogo,Mb - Mjumbe
24. Mhe.Wanu Hafidhi Ameir, Mb - Mjumbe
25. Mhe.Tundu Lissu,Mb, - Mwalikwa

**5.4 Mheshimiwa Spika**, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni na ushauri wao katika Muswada huu ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao:-

(i) Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS),
(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC),
(iii) Chama cha Wamiliki Mabasi wa Tanzania (TABOA),
(iv) Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA),
(v) Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA),
(vi) Mtandao wa Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria Tanzania (TANLAP)
(vii) Muungano wa Vikundi Vya Wakulima Tanzania (MVIWATA)
(viii) Jumuiya ya Wakristo Tanzania (CCT),
(ix) Sekretariati ya Msaada wa Sheria (LAS)
(x) Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
(xi) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF),
(xii) Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Tawi la Dodoma na
(xiii) Taasisi ya Uwezeshaji wa Msaada wa Kisheria (LSF).

**5.5 Mheshimiwa Spika**, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilillah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara

ya Kamati za Bunge Ndg. Athman Hussein, Mkurugenzi Masaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Mkurugenzi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndg. Pius Mboya, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Mossy Lukuvi na Ndg. Prudence Rweyongeza, Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe, Wanasheria wa Bunge Ndg. Leocardo Kapongwa, Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Mariam Mbarouk na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**5.6 Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

1 FEBRUARI, 2017

**MWENYEKITI:** Sasa tunamkaribisha Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ili aweze kuleta maoni yao. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu naomba kiti chako kisimamie kanuni hasa hasa katika masuala yanayohusu uwasilishaji wa majedwali ya marekebisho. Kanuni zetu zipo wazi kama utaratibu wa kutunga sheria utavurugwa, Bunge lako Tukufu litaishia kuwa la kupiga muhuri mambo ambayo yanatoka Serikalini, tusingependa iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujihusisha na sehemu kubwa ya maoni ya Kamati ambayo kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nilishiriki ipasavyo katika kuyatengeneza. Baada ya hapo sasa naomba uniruhusu niwasilishe maoni ya Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2016. Naomba nifanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4), 2016, ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 21 Oktoba, 2016 na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza wakati wa Mkutano wa Tano

wa Bunge lako Tukufu. Muswada huu ulikuwa unapendekeza marekebisho ya sheria mbalimbali saba. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali, Sura ya 134; Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178, na Sheria ya Barabara na Tozo za Mafuta, Sura ya 220.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni pamoja Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251; na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba mapendekezo haya yanahusu sheria nyingi na muhimu. Sio hivyo tu, vifungu vinavyopendekezwa kurekebishwa katika Sheria hizo ni vingi. Hivyo, kwa mfano, ukiachia vifungu tisa vya kiutangulizi, Muswada huu unapendekeza kurekebisha vifungu thelathini na saba vya msingi katika Sheria hizi saba. Kwa vyovyote vile, hii sio kazi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu imelalamikia utaratibu huu wa kuleta marekebisho mengi ya sheria nyingi namna hii katika Muswada mmoja. Kama tulivyosema mwaka jana wakati wa kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa 2016, utaratibu huu unalinyima Bunge lako Tukufu muda na uwezo wa kuyajadili kwa kina na kuyaelewa mapendekezo ya Serikali kabla ya kuyapitisha na kuwa sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utaratibu huu sio tu ni kuligeuza Bunge lako Tukufu kuwa *rubber stamp* ya kuhalalisha maamuzi ya Serikali, bali pia unapelekea Bunge hili kupitisha sheria mbovu zinazoathiri haki za wananchi wetu na ustawi wa Taifa letu na kusababisha migongano isiyokuwa ya lazima katika vyombo vya utekelezaji vya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni yetu ya mwaka tuliishauri Serikali hii ya CCM "kuacha utaratibu huu mbovu wa utungaji sheria." Kuletwa Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu leo ni ushahidi wa wazi kwamba ushauri wetu haukuzingatiwa na Serikali. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inakuomba utumie mamlaka yako kuhakikisha kwamba utaratibu bora zaidi wa utungaji sheria unafuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu bora zaidi ni ule unaolipatia Bunge lako Tukufu muda wa kutosha wa kujadili Miswada ya Sheria kabla ya kuipitisha na kuwa sheria za nchi. Utaratibu huo unataka mapendekezo ya marekebisho

makubwa ya sheria yoyote ile, yaletwe kwa njia ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria husika badala ya kuyaficha katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kama inavyopendekezwa na Muswada huu. Sasa tunaomba kuangalia, *under protest,* marekebisho ya sheria yanayopendekezwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali. Hii ni mara ya pili kwa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali kufanyiwa marekebisho makubwa. Mara ya kwanza ilikuwa tarehe 3 Aprili, 2003, wakati Bunge lako Tukufu lilipopitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali. Sheria hiyo iliongeza vifungu vipya kumi na mbili katika Sheria mama iliyokuwa na vifungu vya ishirini na tatu vya mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Muswada huu unapendekeza marekebisho makubwa zaidi ya Sheria hii. Jumla ya vifungu ishirini na moja kati ya vifungu thelathini na tano vya Sheria hii vinapendekezwa kurekebishwa. Hii ina maana kwamba asilimia 60 ya Sheria hii inapendekezwa kurekebishwa kwa njia hii ya *Miscellaneous Amendments Bill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile, haya ni mabadiliko ya Sera ya Serikali kuhusu mikopo, misaada na dhamana za Serikali. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, mapendekezo haya yanahitaji mjadala mpana zaidi ambao ungewezekana endapo mapendekezo haya yangekuja kama Muswada wa marekebisho ya Sheria mama, badala ya kuletwa kwa njia ya sasa ya marekebisho ya sheria mbalimbali. Bunge lako Tukufu linastahili kuhoji kwa nini Serikali haitaki kutumia utaratibu ilioutumia mwaka 2003 katika kurekebisha Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho ya jumla katika Sheria mama kwa kufuta maneno '*from outside* Tanzania', yaani 'kutoka nje ya Tanzania' na kuyabadilisha na maneno '*from non-resident sources'*, yaani kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani. Maneno yanayopendekezwa kufutwa yanapatikana katika vifungu vya pili na tatu vya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno '*from outside* Tanzania' yametumika katika kifungu cha pili cha sheria kama sehemu ya tafsiri ya maneno '*foreign loan*', yaani mkopo wa nje, ambayo maana yake ni mkopo wowote uliokopwa na Serikali kutoka nje ya Tanzania. Kwa mapendekezo haya ya marekebisho, maneno '*foreign loan*' sasa yatakuwa na maana ya "*any loan contracted by*

*the Government from non-resident sources*", yaani mkopo wowote uliokopwa na Serikali kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na mapendekezo ya marekebisho ya tafsiri ya '*foreign loan',* aya ya tano ya Muswada inapendekeza kurekebishwa kwa tafsiri ya maneno '*local loan',* yaani 'mikopo ya ndani.' Tafsiri mpya inayopendekezwa ni kwamba '*local loan'* ina maana ya "*any loan contracted by the Government from resident sources",* yaani mkopo wowote ambao umekopwa na Serikali kutoka vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha tatu cha Sheria mama kinampa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha mamlaka ya kuingia mikataba ya kupata mikopo kutoka nje ya Tanzania kwa niaba ya Serikali, kwa masharti kuhusu riba, utaratibu wa malipo au vinginevyo kama itakavyokubaliwa na Waziri, kwa lengo la kulipia matumizi yanayotakiwa kulipiwa kihalali. Kwa Marekebisho ya mwaka 2003, mamlaka hayo ya Waziri sasa yanatakiwa yatumiwe baada ya Waziri kupata ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, kifungu cha sita cha Sheria mama kinampa Waziri mamlaka ya kuingia mikataba ya kupata mikopo ya ndani kwa lengo hilo hilo la kulipia matumizi yanayotakiwa kulipiwa kihalali. Masharti ya Waziri kupata ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa yanahusika pia kwa mikopo hiyo ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau waliotoa maoni yao mbele ya Kamati walipendekeza maneno '*non-resident sources'* yapatiwe tafsiri rasmi kwa lengo la kuyapatia uelewa wa wazi. Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inafikiri tofauti. Vyanzo visivyokuwa vya ndani ni maneno ya kawaida katika matumizi ya kila siku ya lugha ya Kiswahili, kama yalivyo maneno '*non-resident sources'* katika lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inafahamu kwamba, katika mazingira ya matumizi yake, maneno mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani yana maana ya mikopo yote inayopatikana kutoka kwa Serikali, mabenki na taasisi nyingine za fedha zilizoko nje ya Tanzania. Kwa mantiki hiyo hiyo, maneno mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka vyanzo vya ndani yatakuwa na maana ya mikopo yote inayopatikana kwa mabenki ya kibiashara na taasisi nyingine za fedha za ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi ambalo Bunge lako Tukufu lina haki ya kupata majibu ni je, tafsiri inayopendekezwa na Muswada huu ina tofauti yoyote ya msingi na tofauti iliyopo kwenye Sheria ya sasa? Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, maneno mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka nje ya Tanzania yaliyopo katika sheria ya sasa yana maana ile ile ya mikopo inayopatikana kutoka kwa Serikali, mabenki ya kibiashara na taasisi nyingine za fedha za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo hiyo, maneno mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka ndani ya Tanzania hayawezi kuwa na maana tofauti na marekebisho yanayopendekezwa na Muswada huu. Kwa maneno mengine, marekebisho yanayopendekezwa hayabadilishi chochote na kwa hiyo, hayana sababu zozote za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya tano ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha pili cha Sheria kwa kuongeza tafsiri ya maneno *'Consolidated Fund.'* Tafsiri ya maneno haya inayopendekezwa ni *"The Consolidated Fund of the Government referred to in the Constitution."* Maneno *'Consolidated Fund'* yanapatikana katika kifungu cha tano cha Sheria kinachoelekeza kwamba fedha zinazotokana na mikopo kutoka nje ya Tanzania zitawekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inataka lipate majibu ni sababu ya kupendekeza tafsiri hii ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Hii ni kwa sababu Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, kama ilivyo kwa Sheria ya Mikopo, Misaada na dhamana za Serikali, haijayatafsiri maneno haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni tatizo gani ambalo limejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii tangu ilipotungwa miaka arobaini na tatu iliyopita kutokana na kukosekana kwa tafsiri inayopendekezwa? Je, ni Waziri gani wa Fedha au Mjumbe gani wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa au wa Kamati ya Wataalam wa Usimamizi wa Deni la Taifa ambaye hadi sasa hafahamu maana ya *Consolidated Fund* au asiyefahamu kwamba fedha zinazotokana na mikopo ya nje zinapaswa kuwekwa katika *Consolidated Fund* kwa mujibu wa kifungu cha tano cha sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, kwamba hakuna tatizo lolote la kimsingi ambalo

limesababishwa na kukosekana kwa tafsiri ya maneno *consolidated fund* katika sheria hii. Ndiyo kusema kwamba marekebisho yanayopendekezwa hayana sababu kwa maana hayabadilishi kitu chochote katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada unapendekeza tafsiri ya maneno *on-lending* katika kifungu cha pili cha sheria kinachohusu tafsiri ya maneno mbalimbali. Tafsiri inayopendekezwa kwa maneno haya ni utaratibu ambao Serikali inakopa kutoka vyanzo vya nje au vya ndani na inafaulisha mkopo huo kwa taasisi nyingine kama vile Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mashirika ya Umma, Serikali za Mitaa au taasisi nyingine yoyote ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri hii inaenda sambamba na mapendekezo ya aya ya 13 ya Muswada ambayo inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 12 cha sheria na kukibadilisha na kifungu kipya cha 12 ambacho kwayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaweza kukopa kwa kutumia utaratibu wa *on-lending* fedha ambazo zimekopwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, utaratibu wa kufaulisha mkopo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar utafanyika kwa makubaliano ya kufaulisha ambayo pamoja na mambo mengine, yatakuwa na masharti ambayo hayatakuwa chini ya masharti ya mkopo mama. Kwa maneno mengine, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itakopa fedha hizo kwa masharti yale yale ya mkopo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Hata hivyo, kabla ya kufaulishiwa mkopo huo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haitakuwa na budi kuhakikisha kwamba inakopa kutokana na nguvu yake ya kifedha na inaonesha uwezo itakaokuwa nao wa kuweza kutekeleza masharti ya mkopo mama. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itatakiwa kutumia fedha za mkopo huo kwa ajili ya vitegauchumi vikubwa kwa miradi ambayo ina manufaa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Mwaka 2003, Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali ilifanywa kuwa ni sheria ya Muungano. Kabla ya hapo na licha ya mikopo kuwa moja wapo ya mambo ya Muungano tangu mwaka 1964, masuala ya mikopo, misaada na dhamana za Serikali hayakuwa mambo ya Muungano bali yalikuwa kama ilivyokuwa inatamka sheria yenyewe, masuala ya Tanganyika. Ukweli ni kwamba jina Tanganyika liliacha kutumiwa kwenye sheria hii mwaka 2003 kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, licha ya kufanywa Sheria ya Muungano masuala ya misaada yaliendelea kuwa masuala ya Tanganyika, hii ni kwa sababu kifungu cha 1A cha sheria hii, kama kilivyorekebishwa mwaka 2003 kinatamka wazi kwamba sheria hii itatumika kwa Tanzania Bara na itatumika kwa Tanzania Zanzibar kuhusiana na mikopo na dhamana tu. Hii ina maana kwamba, kwa Zanzibar sheria hii haihusiani na masuala ya misaada kutoka nchi na taasisi za kifedha za nje inayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tafsiri yetu kuhusu kifungu cha 1A cha sheria hii ni sahihi, basi mapendekezo ya muswada kuhusu Zanzibar yatakuwa ni chanzo kingine kikubwa kwa kile kinachoitwa Kero za Muungano. Hii ni kwa sababu kwa miaka mingi, Zanzibar imelalamika kwamba inapunjwa na Tanganyika katika mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotolewa na nchi wafadhili na Taasisi za Kimataifa kwa Jamhuri ya Muungano. Kwa sababu ya malalamiko hayo, mwaka 2013 iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala ilipendekeza kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili ni vyema ukaangaliwa upya kwa Serikali zote mbili yaani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kamati hiyo ilishauri kwamba Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya tume ya pamoja ya fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu mwaka 2006 na kuwasilishwa tena mwaka 2010 kuhusu utaratibu wa mgao wa fedha za Serikali zote mbili. Serikali ilijibu mapendekezo na ushauri huo wa Kamati kama ifuatavyo na naomba kunukuu; "Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, kuhusu mgawanyo wa fedha zinazotoka kwa wafadhili, upo utaratibu wa mgawanyo wake ambapo kwa upande wa misaada na mikopo ya kibajeti isiyokuwa na masharti maalum Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hupata gawio la asilimia 4.5."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa Bungeni mwaka 2013 na 2014, Zanzibar imekuwa ikipunjwa sana katika mgao wa misaada na mikopo ya kibajeti. Kwa ushahidi wa nyaraka hizo, Zanzibar haijawahi kupata asilimia 4.5 ya mgao wa fedha hizo bali imekuwa ikipatiwa takribani asilimia 3 ya fedha hizo. Hali ni mbaya zaidi kuhusiana na fedha za misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti. Kwenye eneo hili, kwa mujibu wa takwimu za Serikali, fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo

zikijumuisha misaada na mikopo ya *Basket Fund* na misaada na mikopo ya miradi zimekuwa zinatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali iko hivyo kwa sababu masuala ya mikopo na misaada kutoka nje ni mambo ya Muungano, kwa sababu hiyo Zanzibar imenyang'anywa mamlaka ya kuomba mikopo au misaada kutoka nje bila kwanza kupata kibali cha Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya, sisi wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu tulitegemea Serikali ingeleta muswada utakaotatua matatizo haya ya muda mrefu, badala yake Serikali imeletwa muswada utakaoifanya Zanzibar kuwa mdeni wa Tanganyika kwa masharti ya mikopo ambayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haijashiriki kuyajadili na kuyaamua bali ni masharti yaliyokubaliwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taasisi za kifedha za nje au na Serikali za nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha sheria kama kilivyorekebishwa mwaka 2003, Zanzibar ina wawakilishi wawili tu kati ya kumi katika Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa ambayo ina wajibu wa kumshauri Waziri kuhusu masuala ya mikopo ya nje na ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kumwongeza Katibu wa Tume ya Mipango Zanzibar na nimesikia na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar katika kamati hiyo hakubadilishi *balance of power* ndani ya kamati hiyo kwani Tanganyika bado itakuwa na wajumbe nane kati ya kumi na mbili. Na kama inavyopendekezwa na aya ya 19 ya muswada, akidi katika kikao chochote cha kamati hiyo ni nusu ya wajumbe. Katika mazingira haya, kuna uwezekano mkubwa wa vikao vya kamati kufanyika bila uwakilishi wowote wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye kamati ya wataalamu iliyoundwa na kifungu cha 19, uwakilishi wa Zanzibar bado ni wajumbe wawili au watatu tu, kwa mujibu wa kifungu cha 19(3) cha sheria pamoja na marekebisho yanayopendekezwa katika aya ya 18 ya muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, muswada huu haujatoa jibu la kwa nini sheria hii inaihusu Zanzibar katika masuala ya mikopo na dhamana tu, na si katika masuala ya misaada ambayo ndiyo imekuwa chanzo kikubwa cha Kero za Muungano. Kwa sheria kama ilivyo sasa pamoja na mapendekezo ya marekebisho yaliyomo kwenye muswada huu, Zanzibar haina haki ya kupata mgao wa misaada inayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali na mapendekezo ya muswada huu, fedha zinazotokana na mikopo na misaada kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani itaendelea kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Hata hivyo, Ibara ya 133 ya Katiba yetu imeweka masharti kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza Akaunti ya Pamoja ya Fedha ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara ya 134 imeweka masharti kuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenye majukumu ya kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mojawapo ya Serikali hizo. Majukumu mengine ya tume hiyo ni kuchunguza mfumo wa shughuli za fedha kwa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile masuala ya mikopo na misaada kutoka nje ni masuala ya Muungano, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inapenda kufahamu kwa nini fedha za mikopo na misaada kutoka nje zisiwekwe katika Akaunti ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kambi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inapenda kujua kwa nini Tume ya Pamoja ya Fedha, ambayo ni chombo mahsusi Kikatiba kwa ajili ya masuala ya fedha za Muungano, haipo kabisa katika muundo mzima wa sheria hii na wala haipo katika mapendekezo ya marekebisho yaliyopo kwenye muswada huu?

Kwa kadri ya ufahamu wetu, Tume ya Pamoja ya Fedha iliundwa rasmi mwaka 2003 kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha iliyopitishwa na Bunge hili mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 14 ya muswada inapendekeza utaratibu wa kufaulisha mikopo kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani kwa Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kwa masharti yaleyale ambayo Serikali imekopa fedha hizo.

Aidha, masharti ambayo tumeyazungumzia kuhusu mikopo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yatazihusu pia Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Mapendekezo haya yanazua maswali mengi makubwa kuhusu uwezo wa Serikali za Mitaa na Mashirika yetu ya Umma kukopa fedha za kigeni kwa masharti yale yale ambayo Serikali inakopa fedha hizo. Hii ni kwa kuzingatia vyanzo vya mapato na uwezo wa kifedha wa Serikali zetu za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale ambayo sijayasema, naunga mkono yaliyosemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, naomba niishie hapa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MH. TUNDU A.M. LISSU, KUHUSU *MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI (NA. 4) WA 2016 [THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 4) ACT, 2016* - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Kanuni ya 86(6) ya *Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016*)

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,
*Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali (No. 4), 2016*, ulichapishwa kwenye *Gazeti la Serikali* la tarehe 21 Oktoba, 2016, na kusomwa kwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge lako tukufu. Muswada huu ulikuwa unapendekeza marekebisho ya sheria mbali mbali saba. Sheria hizo ni pamoja na *Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali, Sura ya 134*; *Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178*, na *Sheria ya Barabara na Tozo za Mafuta, Sura ya 220*.

Sheria nyingine zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni *Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332*; *Sheria ya Ardhi, Sura ya 113*; *Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251*, na *Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283*.

Ni wazi, Mheshimiwa Spika, kwamba mapendekezo haya yanahusu sheria nyingi na muhimu. Sio hivyo tu, vifungu vinavyopendekezwa kurekebishwa katika Sheria hizo ni vingi. Hivyo, kwa mfano, ukiachia vifungu tisa vya kiutangulizi, Muswada huu unapendekeza kurekebisha vifungu thelathini na saba vya msingi katika Sheria hizi saba. Kwa vyovyote vile, hii sio kazi ndogo.

Mheshimiwa Spika,
Kwa muda mrefu, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu imelalamikia utaratibu huu wa kuleta marekebisho mengi ya sheria nyingi namna hii katika

Muswada mmoja. Kama tulivyosema mwaka jana wakati wa kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali (Na. 3) wa 2016, yaani the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act (No.3), 2016, utaratibu huu "... *unalinyima Bunge lako tukufu muda na uwezo wa kuyajadili kwa kina na kuyaelewa mapendekezo ya Serikali kabla ya kuyapitisha na kuwa sheria za nchi yetu. Matokeo ya utaratibu huu sio tu ni kuligeuza Bunge lako tukufu kuwa rubber stamp ya kuhalalisha maamuzi ya Serikali, bali pia unapelekea Bunge hili kupitisha sheria mbovu zinazoathiri haki za wananchi wetu na ustawi wa taifa letu na kusababisha migongano isiyokuwa ya lazima katika vyombo vya utekelezaji vya umma.*"

Katika maoni yetu ya mwaka tuliishauri Serikali hii ya CCM "kuacha utaratibu huu mbovu wa utungaji sheria." Kuletwa Muswada huu mbele ya Bunge lako tukufu ni ushahidi wa wazi kwamba ushauri haukuzingatiwa na Serikali. Kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inakuomba utumie mamlaka yako kuhakikisha kwamba utaratibu bora zaidi wa utungaji sheria unafuatwa.

Utaratibu bora zaidi ni ule unaolipatia Bunge lako tukufu muda wa kutosha wa kujadili Miswada ya Sheria kabla ya kuipitisha na kuwa sheria za nchi. Utaratibu huo unataka mapendekezo ya marekebisho makubwa ya sheria yoyote ile, yaletwe kwa njia ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria husika badala ya kuyaficha katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali mbali kama inavyopendekezwa na Muswada huu. Sasa tunaomba kuangalia, under protest, marekebisho ya sheria yanayopendekezwa na Muswada huu.

SHERIA YA MIKOPO, MISAADA NA DHAMANA ZA SERIKALI

Mheshimiwa Spika,
Hii ni mara ya pili kwa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali kufanyiwa marekebisho makubwa. Mara ya kwanza ilikuwa tarehe 3 Aprili, 2003, wakati Bunge lako tukufu lilipopitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali.[1] Sheria hiyo iliongeza vifungu vipya kumi na mbili katika Sheria mama iliyokuwa na vifungu vya ishirini na tatu vya mwanzo.

Sasa Muswada huu unapendekeza marekebisho makubwa zaidi ya Sheria hii. Jumla ya vifungu ishirini na moja kati ya vifungu thelathini na tano vya Sheria hii vinapendekezwa kurekebishwa. Hii ina maana kwamba 60% ya Sheria hii inapendekezwa kurekebishwa kwa njia hii ya *Miscellaneous Amendments Bill*.

Kwa vyovyote vile, haya ni mabadiliko ya sera ya serikali kuhusu mikopo, misaada na dhamana za serikali.

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, mapendekezo haya yanahitaji mjadala mpana zaidi ambao ungewezekana endapo mapendekezo haya yangekuja kama Muswada wa marekebisho ya Sheria mama, badala ya kuletwa kwa njia ya sasa ya marekebisho ya sheria mbali

mbali. Bunge lako tukufu linastahili kuhoji kwa nini Serikali haitaki kutumia utaratibu ilioutumia mwaka 2003 katika kurekebisha Sheria hii.

Mheshimiwa Spika,
Aya ya 4 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya jumla katika Sheria mama kwa kufuta maneno 'from outside Tanzania', yaani 'kutoka nje ya Tanzania', na kuyabadilisha na maneno 'from non-resident sources', yaani 'kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani.' Maneno yanayopendekezwa kufutwa yanapatikana katika vifungu vya 2 na 3 vya Sheria hii. Maneno 'from outside Tanzania' yametumika katika kifungu cha 2 kama sehemu ya tafsiri ya maneno 'foreign loan', yaani 'mkopo wa nje', ambayo maana yake ni *"mkopo wowote uliokopwa na Serikali 'kutoka nje ya Tanzania.'"* Kwa mapendekezo haya ya marekebisho, maneno 'foreign loan' sasa yatakuwa na maana ya *"... any loan contracted by the Government from non-resident sources"*, yaani *"mkopo wowote uliokopwa na Serikali kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani."*

Sambamba na mapendekezo ya marekebisho ya tafsiri ya 'foreign loan', aya ya 5 ya Muswada inapendekeza kurekebishwa kwa tafsiri ya maneno 'local loan', yaani 'mikopo ya ndani.' Tafsiri mpya inayopendekezwa ni kwamba 'local loan' ina maana ya "... any loan contracted by the Government from resident sources", yaani "... mkopo wowote ambao umekopwa na Serikali kutoka vyanzo vya ndani."

Mheshimiwa Spika,
Kifungu cha 3 cha Sheria mama kinampa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha mamlaka ya kuingia mikataba ya kupata mikopo 'kutoka nje ya Tanzania' kwa niaba ya Serikali, kwa masharti kuhusu riba, utaratibu wa malipo au vinginevyo kama itakavyokubaliwa na Waziri, kwa lengo la kulipia matumizi yanayotakiwa kulipiwa kihalali. Kwa Marekebisho ya mwaka 2003, mamlaka hayo ya Waziri sasa yanatakiwa yatumiwe baada ya Waziri kupata ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa.[2]

---

[2] Kifungu cha 17(a)

Kwa upande mwingine, kifungu cha 6 cha Sheria mama kinampa Waziri mamlaka ya kuingia mikataba ya kupata 'mikopo ya ndani' kwa lengo hilo hilo la kulipia matumizi yanayotakiwa kulipiwa kihalali. Masharti ya Waziri kupata ushauri wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa yanahusika pia kwa mikopo hiyo ya ndani.

Mheshimiwa Spika,
Wadau waliotoa maoni yao mbele ya Kamati walipendekeza maneno 'non-resident sources' yapatiwe tafsiri rasmi kwa lengo la kuyapatia 'uelewa wa wazi.' Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inafikiri tofauti. 'Vyanzo visivyokuwa vya ndani' ni maneno ya kawaida katika matumizi ya kila siku ya lugha ya Kiswahili, kama yalivyo maneno 'non-resident sources' katika lugha ya Kiingereza.

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inafahamu kwamba katika mazingira ya matumizi yake, maneno 'mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani' yana maana ya mikopo yote inayopatikana kutoka kwa Serikali, mabenki na taasisi nyingine za fedha zilizoko nje ya Tanzania. Kwa mantiki hiyo hiyo, maneno 'mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka vyanzo vya ndani' yatakuwa na maana ya mikopo yote inayopatikana kwa mabenki ya kibiashara na taasisi nyingine za fedha za ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika,
Suala la msingi ambalo Bunge lako tukufu lina haki ya kupata majibu ni je, tafsiri inayopendekezwa na Muswada huu ina tofauti yoyote ya msingi na tafsiri iliyopo kwenye Sheria ya sasa? Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, maneno 'mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka nje ya Tanzania' yaliyopo katika Sheria ya sasa yana maana ile ile ya mikopo inayopatikana kutoka kwa Serikali, mabenki ya kibiashara na taasisi nyingine za fedha za kimataifa. Na kwa mantiki hiyo hiyo, maneno 'mkopo wowote unaokopwa na Serikali kutoka ndani ya Tanzania' hayawezi kuwa na maana tofauti na marekebisho yanayopendekezwa na Muswada huu. Kwa maneno mengine, marekebisho yanayopendekezwa hayabadilishi chochote na, kwa hiyo, hayana sababu zozote za msingi.

Mheshimiwa Spika,
Aya ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 2 cha Sheria kwa kuongeza tafsiri ya maneno 'Consolidated Fund.' Tafsiri ya maneno haya inayopendekezwa ni *"... the Consolidated Fund of the Government referred to in the Constitution."* Maneno 'Consolidated Fund' yanapatikana katika kifungu

cha 5 cha Sheria kinachoelekeza kwamba fedha zinazotokana na mikopo kutoka nje ya Tanzania zitawekwa katika 'Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.'

Swali ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inataka lipate majibu ni sababu ya kupendekeza tafsiri hii ya 'Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.' Hii ni kwa sababu Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, kama ilivyo kwa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali, haijayatafsiri maneno haya. Je, ni tatizo gani ambalo limejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii tangu ilipotungwa miaka arobaini na tatu iliyopita kutokana na kukosekana kwa tafsiri inayopendekezwa?

Ni Waziri gani wa Fedha au mjumbe gani wa Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa au wa Kamati ya Wataalamu ya Usimamizi wa Deni ambaye hadi sasa hafahamu maana ya 'Consolidated Fund' au asiyefahamu kwamba fedha zinazotokana na mikopo ya nje zinapaswa kuwekwa katika 'Consolidated Fund' kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria hii? Inaelekea, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, kwamba hakuna tatizo lolote la kimsingi ambalo limesababishwa na kukosekana kwa tafsiri ya maneno 'Consolidated Fund' katika Sheria hii. Ndio kusema kwamba marekebisho yanayopendekezwa hayana sababu kwa maana hayabadilishi kitu chochote katika Sheria hii.

Mheshimiwa Spika,
Muswada unapendekeza tafsiri ya maneno 'on-lending' katika kifungu cha 2 cha Sheria kinachohusu tafsiri za maneno mbali mbali. Tafsiri inayopendekezwa kwa maneno haya ni "utaratibu ambapo Serikali inakopa kutoka vyanzo vya nje au vya ndani na inafaulisha mkopo huo kwa taasisi nyingine kama vile Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mashirika ya umma, serikali za mitaa au taasisi nyingine yoyote ya umma."

Tafsiri hii inaenda sambamba na mapendekezo ya aya ya 13 ya Muswada ambayo inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 12 cha Sheria na kukibadilisha na kifungu kipya cha 12 ambacho kwayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaweza kukopa – kwa kutumia utaratibu wa 'on-lending' – fedha ambazo zimekopwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria hii.[3]

---

[3] Kifungu kipya cha 12(1)
Kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, utaratibu wa 'kufaulisha' mkopo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar utafanyika kwa makubaliano ya

kufaulisha ambayo, pamoja na mambo mengine, yatakuwa na masharti ambayo hayatakuwa chini ya masharti ya mkopo mama.[4] Kwa maneno mengine, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itakopa fedha hizo kwa masharti yale yale ya mkopo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Hata hivyo, kabla ya kufaulishiwa mkopo huo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haitakuwa na budi kuhakikisha kwamba inakopa kutokana na nguvu yake ya kifedha na inaonyesha uwezo itakaokuwa nao wa kuweza kutekeleza masharti ya mkopo mama.[5] Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itatakiwa kutumia fedha za mkopo huo kwa ajili ya vitega uchumi vikubwa kwa miradi ambayo ina manufaa kiuchumi.[6]

Mheshimiwa Spika,
Kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Marekebisho ya mwaka 2003, Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali ilifanywa kuwa ni Sheria ya Muungano. Kabla ya hapo, na

licha ya 'mikopo' kuwa mojawapo ya Mambo ya Muungano tangu mwaka 1964, masuala ya mikopo, misaada na dhamana za serikali hayakuwa Mambo ya Muungano, bali yalikuwa – kama ilivyokuwa inatamka Sheria yenyewe – masuala ya 'Tanganyika.' Ukweli ni kwamba jina 'Tanganyika' liliacha kutumiwa kwenye Sheria hii mwaka 2003 kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Marekebisho.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, licha ya kufanywa Sheria ya Muungano, masuala ya 'misaada' yaliendelea kuwa masuala ya Tanganyika. Hii ni kwa sababu, kifungu cha 1A cha Sheria hii, kama ilivyorekebishwa mwaka 2003, kinatamka wazi kwamba "*Sheria hii itatumika kwa Tanzania Bara, na itatumika kwa Tanzania Zanzibar kuhusiana na mikopo na dhamana.*" Hii ina maana kwamba, kwa Zanzibar, Sheria hii haihusiani na masuala ya misaada kutoka nchi na taasisi za kifedha za nje inayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano.

---

[4] Kifungu kipya cha 12(2)
[5] Kifungu kipya cha 12(3)(a)
[6] Kifungu kipya cha 12(3)(b)
[6] Kifungu kipya cha 12(3)(b)

Mheshimiwa Spika,

Kama tafsiri yetu kuhusu kifungu cha 1A cha Sheria hii ni sahihi, basi mapendekezo ya Muswada kuhusu Zanzibar yatakuwa ni chanzo kingine kikubwa kile kinachoitwa 'Kero za Muungano.' Hii ni kwa sababu, kwa miaka mingi Zanzibar imelalamika kwamba inapunjwa na Tanganyika katika mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotolewa na nchi wafadhili na taasisi za kimataifa kwa Jamhuri ya Muungano. Kwa sababu ya malalamiko hayo, mwaka 2013, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge lako tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala ilipendekeza kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba: *"Utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili ni vyema ukaangaliwa upya kwa Serikali zote mbili yaani SMZ na SMT."* Aidha, Kamati hiyo ilishauri kwamba *"Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu mwaka 2006 na kuwasilishwa tena mwaka 2010 kuhusu utaratibu wa mgao wa fedha za Serikali zote mbili."*

Serikali ilijibu mapendekezo na ushauri huo wa Kamati kama ifuatavyo: *"Serikali zetu mbili bado zinaendelea kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, kuhusu mgawanyo wa fedha zinazotoka kwa wafadhili, upo utaratibu wa mgawanyo wake ambapo, kwa upande wa misaada na mikopo ya kibajeti isiyokuwa na masharti maalum, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ... hupata gawio la asilimia 4.5."*

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, kwa nyaraka mbali mbali zilizowasilishwa Bungeni mwaka 2013 na 2014, Zanzibar imekuwa ikipunjwa sana katika mgawo wa misaada na mikopo ya kibajeti. Kwa ushahidi wa nyaraka hizo, Zanzibar haijawahi kupatiwa 4.5% ya mgawo wa fedha hizo, bali imekuwa ikipatiwa takriban 3% ya fedha hizo.

Hali ni mbaya zaidi kuhusiana na fedha za misaada na mikopo isiyokuwa ya kibajeti. Kwenye eneo hili, kwa mujibu wa takwimu za Serikali, fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha misaada na mikopo ya Basket Fund na misaada na mikopo ya miradi zimekuwa zinatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tanganyika. Hali iko hivyo kwa sababu masuala ya mikopo na misaada kutoka nje ni Mambo ya Muungano. Kwa sababu hiyo, Zanzibar imenyang'anywa mamlaka ya kuomba mikopo au misaada kutoka nje bila kwanza kupata kibali cha Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika,
Katika mazingira haya, sisi wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu tulitegemea Serikali ingeleta Muswada utakaotatua matatizo haya muda mrefu. Badala yake, Serikali imeleta Muswada utakaoifanya Zanzibar kuwa

mdeni wa Tanganyika kwa masharti ya mikopo ambayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haijashiriki kuyajadili na kuyaamua bali ni masharti yaliyokubaliwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taasisi za kifedha za nje na/au Serikali za nchi za nje.

Ikumbukwe hapa kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria kama kilivyorekebishwa mwaka 2003, Zanzibar ina wawakilishi wawili tu kati ya kumi katika Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa, ambayo ina wajibu wa kumshauri Waziri kuhusu masuala ya mikopo ya nje na ndani. Pendekezo la kumwongeza Katibu wa Tume ya Mipango ya Zanzibar katika Kamati hiyo[7] hakubadilishi *balance of power* ndani ya Kamati hiyo kwani Tanganyika bado itakuwa na wajumbe nane kati ya kumi na moja.

Na kama inavyopendekezwa na aya ya 19 ya Muswada, akidi katika kikao chochote cha Kamati hiyo ni nusu ya wajumbe. Katika mazingira haya, kuna uwezekano mkubwa wa vikao vya Kamati kufanyika bila uwakilishi wa Zanzibar. Hata kwenye Kamati ya Wataalamu iliyoundwa na kifungu cha 19, uwakilishi wa Zanzibar bado ni wawili au watatu tu, kwa mujibu wa kifungu cha 19(3) cha Sheria pamoja na marekebisho yanayopendekezwa katika aya ya 18 ya Muswada.

Vile vile, Mheshimiwa Spika, Muswada huu haujatoa jibu la kwa nini Sheria hii inaihusu Zanzibar katika masuala ya mikopo na dhamana tu, na sio katika masuala ya misaada ambayo ndio imekuwa chanzo kikubwa cha 'Kero za Muungano.' Kwa Sheria kama ilivyo sasa pamoja na mapendekezo ya marekebisho yaliyomo kwenye Muswada huu, Zanzibar haina haki ya kupata mgawo wa misaada inayokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali na mapendekezo ya Muswada huu, fedha zinazotokana na mikopo na misaada kutoka 'vyanzo visivyokuwa vya ndani' itaendelea kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Hata hivyo, ibara ya 133 ya Katiba yetu imeweka masharti kwamba *"Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza 'Akaunti ya Pamoja ya Fedha ... ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha ... kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano."*

---

[7] Aya ya 18

Aidha, ibara ya 134 imeweka masharti ya kuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenye majukumu ya *"kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo."* Majukumu mengine ya Tume hiyo ni *"kuchunguza ... mfumo wa shughuli za fedha kwa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili."*

Mheshimiwa Spika,
Kwa vile masuala ya mikopo na misaada kutoka nje ni masuala ya Muungano, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inapenda kufahamu kwa nini fedha za mikopo na misaada kutoka nje zisiwekwe katika Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Pili, Kambi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inapenda kujua kwa nini Tume ya Pamoja ya Fedha, ambayo ni chombo mahsusi kikatiba kwa ajili ya masuala ya fedha za Muungano, haipo kabisa katika muundo mzima wa Sheria hii na wala haipo katika mapendekezo ya marekebisho yaliyopo kwenye Muswada huu. Kwa kadri ya ufahamu wetu, Tume ya Pamoja ya Fedha iliundwa rasmi mwaka 2003, kufuatia kutungwa kwa *Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha*, iliyopitishwa na Bunge hili mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika,
Aya ya 14 ya Muswada inapendekeza utaratibu wa kufaulisha mikopo kutoka vyanzo visivyokuwa vya ndani kwa serikali za mitaa na mashirika ya umma kwa masharti yale yale ambayo Serikali imekopa fedha hizo. Aidha, masharti ambayo tumeyazungumza kuhusu mikopo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yatazihusu pia Serikali za Mitaa na mashirika ya umma. Mapendekezo haya yanazua maswali makubwa kuhusu uwezo wa serikali za mitaa na mashirika ya umma kukopa fedha za kigeni kwa masharti yale yale ambayo Serikali inakopa fedha hizo. Hii ni kwa kuzingatia vyanzo vya mapato na uwezo wa kifedha wa serikali zetu za mitaa na mashirika ya umma.
Mheshimiwa Spika,
Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha.

---

TUNDU A.M. LISSU (MB)
MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIBA NA SHERIA

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa maoni yenu. Kwa vile bado tuna muda tuanze na wachangiaji, na tutaanza na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Japhet Hasunga. *(Makofi)*

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii nikiwa mtu wa mwanzo kuchangia muswada huu, nikushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia kile ambacho nilitaka kukisema hapa, nimpongeze Mnadhimu na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa kile ambacho amekiwasilisha kwa ufasaha mkubwa sana. Lakini pia niunge mkono hotuba ya Kamati ya Katiba na Sheria na mimi nikiwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie muswada huu nijielekeze kwenye Ibara ya 13 ya muswada huu inayohusiana na masuala ya mikopo ya Serikali pamoja na misaada na dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu kubwa kuona kwamba miaka 50 ya uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini hadi leo tunakuja kupitisha sheria ambayo inaifanya sasa Zanzibar, maana tunaweka masharti ya kukopa Zanzibar kama vile Serikali ya Mtaa, tunaipa mamlaka kama Serikali ya Mtaa, masharti ambayo inawekewa kukopa Serikali ya Mtaa ndiyo masharti ambayo leo tunaiwekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hili ni jambo la aibu na ni jambo la masikitiko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tupo katika mjadala, si mara moja wala mbili, kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, tumelizungumza suala hili lakini bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Mwanasheria Mkuu kaendelea kubakia na msimamo wake, kaendelea kifungu kile kile kukibakisha na masharti yale yale, alichokibadilisha ni matumizi ya lugha tu. Lakini masharti yako palepale kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili ipate mkopo wa aina yoyote, kwa matumizi yoyote ni lazima ikakopewe au Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikakope halafu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ianze sasa *procedure* ya kuomba mkopo ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni aibu na ni aibu ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo ambalo limezungumzwa hapa kwa kina na Mnadhimu na Msemaji wa Kambi ya Upinzani limezungumzwa kwa ufasaha. Ni miaka mingi suala hili limekuwa ni kero kwa Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar, ni kero kwa Wazanzibari, kwamba leo, miaka 50 mtoto kakua tayari, kwa nini Serikali ya Jamhuri ya Muungano isianze kufikiria sasa kuipa angalau mamlaka Zanzibar ya kuanza kutembea kwa miguu yake? Kuna tatizo gani? Kuna ubaya gani sasa Zanzibar kuanza kuiachia kidogo kidogo ikatembea kwa miguu yake? Mpaka leo tunaendelea, maana mnaandaa sheria ya kuendelea tu, maana kile kinachozungumzwa kwamba kilichopo hapa ni…

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiifafanua kwa kina Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya sasa inatambua mamlaka tatu. Tujiulize, hivi mamlaka ya Tanganyika ambayo imo ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi inakopewa na nani? Inaenda kumsujudia nani ikakopewe, maana yake ni mamlaka ambayo imejivisha koti la Muungano, huoni sehemu yoyote, huoni sheria yoyote kwamba sasa yale mambo ambayo yanagusa Tanganyika, si mambo ya Muungano, ni ya Tanganyika, yanaomba ruhusa kwa nani kwenda kujitafutia mkopo, msaada na kitu kingine chochote nje ya Tanzania au ndani ya Tanzania. Mamlaka hii ya Tanganyika inaomba ruhusa kwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mamlaka ya Zanzibar ambayo kuna Serikali kamili, kuna Rais, kuna Baraza la Wawakilishi, kuna kila kitu. Kwa nini kila siku iombe ruhusa? Kwa nini kila siku ije ipige magoti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuomba ruhusa eti ikakopewe? Huo msingi wa kukopa, kwamba sio ikakopewe tu lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikakope halafu waje waanze sasa kuiwekea masharti Zanzibar kwamba baada ya Serikali ya Muungano kukopa ikapewa masharti haya, huko ambako imeenda kukopa, na hiyo ikija sasa inapanga masharti mapya kuipangia Zanzibar kama vile ambavyo Serikali ya mtaa fulani imewekewa masharti, hivi mnatuelekeza wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani muda umefika sasa, miaka 50 si kidogo, muda umefika sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba Pendekezwa ukisoma Ibara ya 254(1), (2) na ya (3) imezungumzia vizuri suala hili na tayari ilikuwa imeshaipa Zanzibar kutaka kutembea kwa miguu yake, na wanazungumza kwamba kuna matatizo ya Kikatiba. Matatizo ya Kikatiba ya nchi hii hayakuanza leo, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mpaka leo inatambua uwepo wa Waziri Kiongozi kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijavunja Katiba ya Muungano? Kimsingi tayari imevunja Katiba ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuna mambo yameorodheshwa kama mambo ya Muungano, utekelezaji wake hautekelezwi kama mambo ya Muungano, Zanzibar inatekeleza kivyake na Tanzania Bara inatekeleza kivyake. Kwa nini leo tuambiwe kwamba kurekebisha kifungu hiki, kutoa mamlaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenda kukopa, kwenda kuomba misaada nje ya nchi, nje ya Tanzania inavunja Katiba ya Muungano, kwa hili tu? Kwa nini tusiseme kukusanya kodi sasa, kwa sababu ni suala la Muungano ile *ZRB* kule Zanzibar ifutwe, kwa nini tusiseme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiseme masuala ya hali ya hewa sasa Zanzibar isiwe na kitengo kinachotabiri masuala ya hali ya hewa? Kwa nini tusiseme kwamba hapa tunavunja Katiba tuje tuseme tunavunja Katiba eti kwa sababu tunaomba sasa Zanzibar ipewe mamlaka ikakope nje ya nchi. Kwa nini tunasema tunavunja Katiba eti kwa sababu tumesema Zanzibar sasa iende ikaombe misaada nje ya nchi, hapo tunavunja Katiba. Tulijiunga na *OIC* kwenda kuomba misaada tukaambiwa tunavunja Katiba tujitoe, kwa nini kila sehemu ambapo kuna maslahi ya Zanzibar tunaambiwa tunavunja Katiba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe wawazi na tuwe wakweli, muda umefika sasa kuiachia Zanzibar ianze angalau kutambaa kama si kutembea. Zanzibar nayo ina mahitaji, leo inafika mahali Serikali ya Jamhuri ya Muungano inataka kwenda kukopa eti halafu waje waikopeshe Serikali ya Zanzibar, pia tunawekewa masharti kwamba tunakwenda kuwakopea lakini mtumie kwa matumizi haya na haya, hee! jamani, hata huyo mke *time* nyingine unampa nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mke uliyemuoa ukamtolea mahari wakati mwingine akikwambia nipe laki moja wala humhoji unaenda kutumia nini. Mambo mengine ni yake yeye, wewe si utakuja kuyaona tu? Huwezi kumwambia kwamba nakupa laki moja lakini katumie kwa hiki na hiki na hiki. Hii ndoa au ujeshi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimalizie kwa nia njema kabisa. *AG* akubali kwamba kile kifungu ambacho kiliwekwa ndani ya Katiba Pendekezwa ambalo bado halijamaliza mchakato wake basi kinyofolewe kiwekwe katika maeneo haya, na kilizungumza wazi kwamba Zanzibar sasa ina mamlaka ya kwenda kukopa nje na ndani ya nchi, halafu haya masharti mengine yatafuata baadaye. Si lazima na wala si wajibu na kama Katiba hii, hii Katiba ni yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii haijatufunga kwamba sasa Zanzibar lazima tuikabe koo hata pa kusema, hata pa kufurukuta haina. Lazima tujipangie mikakati kama ni kweli tuna nia njema ambayo haipo ya kuendeleza na kuudumisha Muungano huu. Hiyo nia haipo na ndiyo maana vifungu hivi vya Katiba ndiyo kwanza vinaandaliwa ili kuendelea kuibana Zanzibar ili Zanzibar iendelee kuja kusujudia Bara kwa maslahi ya watu fulani. Ahsante sana, nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kombo. Tunaendela na Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kupata hii nafasi ili niweze kuchangia katika muswada huu ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta muswada huu mzuri, muswada ambao unakwenda kutatua matatizo mengi ambayo yamekuwa yakiikabili nchi yetu, kwa kweli tunampongeza sana.

Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa jinsi ambavyo wamechambua muswada huu na maoni yake ambayo wameyatoa ili kuboresha muswada huu, na nadhani kwa kweli wamefanya kazi nzuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa nichangie maeneo machache, lakini la kwanza ambalo ningependa nianze nalo ni hili suala la mikopo yenye dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wowote duniani una masharti yake, mkopo wowote ambao mtu anahitaji au taasisi inahitaji una masharti ambayo lazima kigezo hicho kizingatiwe. Sasa kwenye nchi yetu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba kuna Serikali mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hilo, imeweka mipaka baadhi ya masuala ambayo yanashughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na masuala ya fedha ni mojawapo ya suala la Muungano, kwa hiyo hili ni lazima lishughulikiwe na sheria za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na matatizo kwa muda mrefu na kumekuwepo na malalamiko ya pande hizi mbili kwamba katika baadhi ya mikopo ambayo imekuwa ikitolewa imekuwa haizingatii sheria, imekuwa haizingatii masharti na kanuni za mikopo. Mimi naona hii Sheria inayoletwa mbele yetu sasa inakuja kutatua haya. Sasa hatuwezi kuzungumzia ya nyuma, tukasema miaka mingi imepita, aaa, sasa wakati umefika ndiyo maana sasa Serikali ya Awamu ya Tano inataka kutatua haya ili tuweze kusonga mbele, kwa hiyo mimi nadhani hii ni nia njema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema taasisi yoyote ambayo inaomba mkopo wa aina yoyote; kumekuwepo na tabia ya taasisi nyingi katika nchi hii zimekuwa zikiomba mikopo na zinaomba dhamana ya Serikali lakini inapokuja kulipa zimekuwa zinasuasua hazilipi, sasa hii sheria inaboresha, sheria hii sasa inakuja kutatua haya matatizo. Inasema taasisi yoyote ambayo itakopa ambayo ina miradi ya maendeleo, maadamu miradi hiyo itakubalika, basi ikope lakini tuangalie wana uwezo wa kulipa? Kama hawana uwezo wasipewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sheria jinsi ilivyoweka mimi nakubaliana nayo kabisa kwamba lazima tuangalie uwezo wa kulipa wa taasisi yenyewe na taasisi ikionekana ina uwezo ndiyo ipewe mkopo, haina iwezo isipewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri hii sheria tena imeweka masharti magumu. Imeweka masharti kwamba kama taasisi itakopa na itashindwa kulipa, basi wale viongozi wachukuliwe hatua hii sheria ni nzuri sana, wachuliwe hatua kweli kwa sababu dawa ya kukopa ni kulipa. Huwezi ukasema unakopa halafu unakimbia kulipa, dawa ya deni ni kulipa na ndiyo maana tunasema, hata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa inaruhusiwa kukopa katika miradi ile ambayo inaona kwamba ina manufaa kwa nchi yao, lakini pia lazima tuzingatie uwezo wa Zanzibar wa kulipa hayo madeni, ndicho kinachoelezwa katika hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wakope halafu wasilipe, kwa hiyo kama watakopa, sheria hii inawaruhusu lakini tunasema tuangalie *balance sheet* yao wana uwezo wa kulipa maana ni masuala ya Muungano? Sasa wasipolipa itakuja kuwa ni tatizo la Muungano. Ili lisiwe tatizo lazima tuangalie uwezo wao. Tukiona hiki wana uwezo tutawaruhusu wakope, walipe, waiendeleze Zanzibar hilo mimi sidhani kama lina tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo hili mimi naunga mkono kabisa Sheria hii ilivyokaa imekaa vizuri na Wazanzibar nadhani ni wakati muafaka sasa wataendelea vizuri, watafanya vizuri lakini tunawashauri wakope na walipe na watalipa kwa taratibu zilizopo, watalipa *principle,* watalipa na riba ile inayotakiwa. Hatutazidisha riba, riba iliyokubalika ndiyo hiyo hiyo walipe. Kwa hiyo, mimi nadhani sheria imekaa vizuri. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo ningependa nichangie ni suala marekebisho ya hii sheria inayohusu mikopo ya elimu ya juu

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Mikopo ya Elimu ya Juu, hii sheria sasa imesema vijana wetu...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** …vijana wetu ambao….bado hujaruhusiwa kwa hiyo wewe subiri niendelee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu wa kutoa mikopo kwa vijana wetu wanaosoma kwenye vyuo vya elimu ya juu kulikuwa na malalamiko mengi. Kulikuwa na mambo mengi ambayo yapo. Sheria hii sasa inarekebisha inasema; hata vijana sasa wenye *diploma* waruhusiwe kukopa mimi nadhai hii sheria ni nzuri sana ya kuiunga mkono. Maana yake tuna vijana ambao wana stashahada katika fani mbalimbali, kwa mfano; fani za afya, mafundi mchundo tunahitaji, hatuhitaji watu wawe na *degree,* tunahitaji hawa wote wapate elimu itakayotusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kuwa nchi ya viwanda hao ndio wanaohitajika kwenda kufanyakazi, sasa ili tuwapate lazima wapate mikopo. Kwa hiyo huu utaratibu mimi naomba niseme kwamba nauunga mkono kabisa, sheria hii irekebishwe, vijana wetu wale wote wenye stashahada wapate mikopo na ikiwezekana badala ya kusema fani fulani fulani, fani zote ziruhusiwe kukopa, maana ni mikopo, watalipa. Watalipa hawa, wakikopa watalipa. Kwa

hiyo, mimi nashauri kabisa kwamba hawa vijana ni wakati muafaka waangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, hebu tuangalie masharti yaliyowekwa kwenye mikopo; kuna haja ya kupitia. Tunaweza tukaweka kwa mfano katika hii fani ya stashahada tukasema mtu yoyote ambae ana-*upper second and above* au ana-*first class,* ana-*upper second* uruhusiwe kukopa badala ya kuwawekea kwenye taaluma kwamba taaluma fulani ndiyo wakope wengine wasikope. Wote waruhusiwe washindane ili kuwe na uwazi katika utoaji wa hii mikopo. Mimi nadhani hili litatusaidia sana katika kuweza kuleta maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nichangie kidogo kuhusu misamaha ya kodi. Sheria hii imezungumzia juu ya misamaha ya kodi ambayo imekuwa ikitolewa na Waziri na imeweka utaratibu mzuri kwa jinsi Waziri anavyoweza kutoa misamaha ya kodi. Mimi nadhani hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu sana. Nchi yetu tunashindwa kuendelea kwa sababu ya misamaha mingine isiyokuwa na tija, na niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano imepunguza sana misamaha ya kodi kwa kweli nawapongeza sana, imepunguza sana hii. Lakini tuendelee kuboresha kabisa ili misamaha ya kodi itakayokuwa inatolewa…..

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** …….itolewe iwe ni ile yenye tija tu, iwe yenye tija tu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unavunja Kanuni, Kuhusu Utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Umefanyaje? Endelea.

**MBUNGE FULANI:** Hujaruhusiwa, kaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaogopa nini?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kanuni inaruhusu niombe utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba tuvumiliane tumalize Mheshimiwa amalizie.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akimaliza utaratibu unaisha, kanuni….

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wanaozungumzia Kuhusu Utaratibu, ndiyo maana sisi tumeshinda Kata 22 kati ya ngapi, tunawapongeza. Sisi tumeshashinda hapa tunazungumzia kuleta maendeleo, jinsi ya kuwatumikia Watanzania hayo Kuhusu Utaratibu…mimi nachangia. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mweyekiti, mimi nadhani waangalie kitu cha kufanya haya mambo ni ya msingi, tunazungumzia maendeleo ya nchi hii. Kwa hiyo, misamaha ya kodi itakayokuwa inatolewa tuangalie wale wote wanao-*qualify* zile taasisi……

**MHE. JOHN W. HECHE:** Wewe mwenyewe Jimboni huendi unasema umeshinda.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** …ile misamaha ya kodi iwe ni misamaha yenye manufaa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Jimboni hukanyagi unanuka Jimboni.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Atakanyagia wapi huyo?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti mimi nadhani haya ni masuala ya msingi sana ambayo sheria hii iliyoko mbele yetu inaenda kuyatatua, lazima sote tuiunge mkono kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimalizie kwa kusema nawapongeza Wabunge wapya ambao wameteuliwa na ambao wameapa jana, washirikiane nasi katika kusukuma gurudumu la maendeleo. Nchi yetu hii wananchi wanahitaji maendeleo ya kweli na naomba tushirikiane tulete maendeleo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ndiyo maana ulishindwa uchaguzi wewe ukatangazwa na polisi muangalie vile.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Tulia, hata mimi naishi Msasani, Mdee sijawahi kukuona.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tunapochangia jamani tuwe na uvumilivu, najua utaratibu na taarifa zimo kwa mujibu wa Kanuni lakini naomba pia muelewe mamlaka hayo yapo kwenye kiti, tafadhali kwa sababu wenzenu wanapozungumza wengine wanavumilia kwa hiyo maoni ni haki ya kila mtu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa ni Kanuni bwana.

**MWENYEKITI:** Naomba tuelewane hivyo Waheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo maana Kanuni zipo Mheshimiwa Mwenyekiti

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Na wewe Ditopile wewe!!

**MWENYEKITI:** Sawa, Waheshimiwa tunaendelea.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Sijawahi kukuona Msasani.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Wewe Ditopile...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tafadhali hakuna anayepotoshwa tunaenda vizuri. Kabla hatujamaliza jamani nina tangazo moja. Mheshimiwa Ester Bulaya una tangazo hapa naomba nilisome. Mheshimiwa Ester Bulaya anatangaza kupotelewa na saa yake ya rangi ya *gold* kwa hivyo yeyote atakayeiona tafadhali airejeshe kwa mwenyewe

**MBUNGE FULANI:** Amehonga hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa yote kwa mchana huu, naomba nitangaze majina ya ambao watachangia jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, tutaendelea na Mheshimiwa Tundu Lissu na baadaye Mheshimiwa Andrew Chenge na kumalizia na Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nawashukuru sana, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

Hadi saa kumi jioni.

**MBUNGE FULANI:** Alisahau saa...

**WABUNGE FULANI:** Saa kumi na moja jioni.

**MWENYEKITI:** Samahani hadi saa kumi na moja jioni.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefika saa moja hapa, wa kwanza, Mheshimiwa Mwenyekiti unabeba watu.

*(Saa 6.54 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa 2016 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2016***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu na sasa tunamkaribisha Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta muswada wa muhimu katika kujenga mustakabali wa nchi yetu hasa hasa kwenye maeneo ya usimamizi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wao ambao wameutoa katika kuboresha muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nijikite kwenye kipengele cha mikopo, msaada na dhamana, hasa kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu sasa hivi kuna ushindani mkubwa katika *International Capital Markets.* Muswada huu umelenga kuzisaidia Serikali zote mbili, kwa maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili ziweze kushirikiana katika kuhakikisha ukienda kukopa kwenye Masoko ya Kimataifa ya Mikopo basi sheria zetu zinatusaidia kupata mikopo hii kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye *International Capital Markets* bila sheria za namna hii tunaweza tukawa tuna mipango mizuri, tukapitisha bajeti zenye mipango mizuri ya maendeleo lakini sheria zikatukwamisha. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuangalia hili, kwa sababu maboresho ya muswada yanalenga kusaidia Serikali zetu ziweze kupata mikopo ya bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuwasihi Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa jicho la tofauti kwamba pengine muswada huu unalenga kukandamiza maslahi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mimi siioni hivyo, kwa sababu ukikopa katika utaratibu wa pamoja tunapata riba nafuu. Sasa muswada huu umelenga kutusaidia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama ninavyofahamu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni *sovereign country* na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, muswada huu umelenga kusaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iweze kukopa kwenye *International Capital Markets* kupitia Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru kwenye muswada katika kuhakikisha tunasimamia vizuri fedha za umma kuna *checks and balances.* Hii Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Madeni ya Taifa, mapendekezo yake yanalenga kumsimamia Waziri wa Fedha asiwe na mamlaka ya peke yake kujiamlia mikopo mikubwa ambayo tunakopa katika *International Capital Markets* bila kuwa na chombo ambacho kitamsimamia na kumshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kuwa na hii *The National Debt Management Committee* ni mpango mzuri na utasaidia dhamira ya Serikali kuhakikisha fedha za umma zinasimamiwa ipasavyo ili Watanzania waweze

kupata maendeleo ambayo tumewaahidi katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia muswada umelenga kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kuwa na msingi wa sheria wa kukasimisha madaraka kwa Gavana wa Benki Kuu kwa sababu sheria zilizokuwepo hazikuwa na kifungu ambacho kinaruhusu mamlaka ya kumkasimisha Gavana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia muswada umetoa msingi wa kisheria ambao utamruhusu Waziri wa Fedha kuweza kukasimisha madaraka kwa Gavana ili aweze kutoa dhamana za Serikali kwa mujibu wa sheria. Kabla ya hapo kulikuwa hamna kifungu ambacho kinampa madaraka hayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, hili ni eneo lingine ambalo linaonesha muswada huu umelenga kuboresha usimamizi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Muswada umeweka mapendekezo mazuri, umepanua wigo ili hata wale wanafunzi ambao wapo kwenye elimu ya juu ambao wanachukua *diploma* waweze kupata fursa ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili nipende kushauri, kwa sababu tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda, uchumi wa kati *(middle income country)* pia tuangalie hata hizi *Vocational institutions* hasa taasisi kama *Dar es salaam Technical Institute, Arusha Tech.,* hivi vyuo vya ufundi tusiviache pembeni katika mpango mzima wa kuboresha na kupanua wigo kwa ajili ya vijana wetu wanaosoma masomo ya elimu ya juu. Tuangalie hata *Vocational Training Institutions* kwa sababu tunalenga kuwa na uchumi wa viwanda, hivyo tukiwasaidia vijana ambao wanaenda kujifunza ufundi stadi, wakapata mikopo, tutakuwa tunawasaidia kupata ujuzi ambao watatusaidia kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pamoja na maboresho mazuri kwenye upande wa kuwezesha vijana ambao wanaenda kwenye vyuo vya ufundi stadi muswada haujawatendea haki vijana hawa. Nipende kuomba marekebisho haya yafanyike ili tupanue wigo vijana wengi wa Tanzania waweze kupata mikopo ya elimu ya juu zikiwepo *Vocational Technical Institutions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho ya sheria pia kuna Sheria ya Kodi ya Mapato. Najua sasa hivi *Tanzania Revenue Authority* chini ya Wizara ya Fedha wanajitahidi sana kukusanya mapato ili tuweze kupata fedha za kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo. Hata hivyo katika udhibiti wa utumiaji

wa msamaha wa kodi Taasisi za Dini zimejikuta katika wakati mgumu sana. Nipende kuiomba Serikali si kwamba taasisi zote zilitumia vibaya misamaha ya kodi, taasisi nyingi za Dini zinatumia hii misamaha ya kodi vizuri. Sasa Serikali iweke utaratibu mzuri ili wale ambao ni waaminifu katika Taasisi za Dini waweze kupata misamaha ya kodi kwasababu misamaha hii inawasaidia Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato pia kuwekwe utaratibu mzuri ambao utazisaidia Taasisi za Dini ziweze kuendelea kuwasaidia Watanzania walio wengi kupitia hizi taasisi, ziendelee kusaidiwa katika misamaha ya kodi ambayo ilikuwepo kipindi cha nyuma lakini ikafanyiwa marekebisho ili kudhibiti matumizi mabaya ya msamaha wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi ila nilipenda kusisitiza jinsi gani wenzetu wachache ambao wanapinga huu muswada. Sisi tumekuja hapa Bungeni kutunga sheria, kuishauri na kuisimamia Serikali. Sasa ukiangalia muswada huu una nia njema kabisa ya kusaidia Serikali ili iweze kusimamia vizuri fedha za umma, iweze kusaidia Serikali zetu mbili - Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna wengine wanasema vitu ambavyo vimelenga kupotosha. Si kwamba muswada una nia yeyote mbaya ya kuweza kukandamiza Serikali yoyote. Muswada umelenga kusaidia Serikali zetu ziweze kujipanga na kupata fedha katika nyanja mbalimbali ikiwemo kwenye *International Capital Markets* ili tuweze kutekeleza yale ambayo tumewaahidi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kwa kiasi kikubwa katika Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali na kama bado muda utatosha nitazungumza kidogo kuhusu marekebisho ya Sheria ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo wa kiingereza unasema unaosema *the road to hell is paved with good intentions* (njia ya kwenda jehanamu imepambwa kwa nia njema). Sasa nia njema peke yake haiwezi ikatosha tunapotunga sheria. Lazima tuangalie *potential consequences* za hiyo sheria tunayoitunga. Kwa hiyo, kutuambia kwamba lengo la muswada ni zuri kwa hiyo tupitishe ni kutuelekeza jehanamu kwa kutegemea tu nia njema. Hatuwezi tukafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu unapendekeza hivi; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwe mdeni wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Serikali ya Jamhuri ya Muungano inakopa pesa *say* kutoka Benki ya Dunia au kutoka Mabenki ya Kibiashara ya Kimataifa au nchi za kigeni, masharti ya mkopo huo yanadai kwamba ulipwe kwa muda fulani, kwa riba fulani, kwa fedha za kigeni. Halafu kwa Muswada huu, Serikali ya Zanzibar tunaikopesha sisi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaikopesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa masharti yale yale ambayo tumepewa sisi na Benki ya Dunia au Mabenki ya Biashara au Taasisi zingine za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tuulizane tu. Tusitegemee tu nia njema, *what if they do not pay? What if they are unable to pay, for whatever reasons.* Itakuwaje Serikali ya Zanzibar ikishindwa kulipa huo mkopo kwa masharti yale yale ambayo sisi tumekopa nje (Serikali ya Jamhuri ya Muungano) itakuwaje? Tutakamata mali zao? Tutawashtaki? Tutafanyaje? Wakishindwa kulipa itakuwaje? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, muswada unapendekeza vilevile kwamba Serikali inakopa pesa nje kwa masharti hayo, masharti ya mikopo ya kimataifa sio marahisi sana, inakopa nje halafu linakuja Shirika la Umma kwa mfano UDA au Shirika la Elimu Kibaha au *National Insurance Corporation* au *Air Tanzania,* Serikali inaikopesha kwa masharti yale yale ambayo imekopa nje ilipe kwa dola, ilipe riba, ilipe kwa muda fulani; ndiyo masharti yanayozungumzwa kwenye muswada huu. Tusizungumzie nia njema, nia njema itatupeleka kuzimu.

Mheshikmiwa Mwenyekiti, itakuwaje *Air Tanzania* wakishindwa kurudisha hiyo hela Serikalini? Itakuwaje Shirika la Elimu Kibaha wakishindwa? Itakuwaje Halmsahauri ya Wilaya ya Ikungi, imekopa pesa Serikalini kwa utaratibu huu ikishindwa kulipa? Kwa sababu Halmashauri za nchi hii karibu zote zinaitegemea Serikali kwa karibu asilimia 90, zimenyang'anywa vyanzo vya mapato, hazitozi kodi za majengo na mapato mengi zimenyang'amywa, zikishindwa kulipa itakuwaje? Kwa hiyo, haitoshi tu kuwaambia watu nia njema, nia njema, tunaunga mkono nia njema ya Serikali, tutaenda kuzimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye suala la utaratibu huu kwa Serikali ya Zanzibar kwa sababu watu hawaelewi matatizo makubwa ambayo yanakabili Muungano wetu kwa sababu ya matatizo kama haya. Kumekuwa na mgogoro kwa wasiofahamu (mwalimu wangu anafahamu vizuri sana) kumekuwa na mgogoro nchi hii kwa zaidi ya miaka 40 juu ya mapato ya Muungano, zaidi ya miaka 40. Jumbe aling'olewa madarakani mojawapo kwa sababu ya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wamekuwa wanadai kwamba pesa zinazokuja kwa jina la Jamhuri ya Muungano hawazipati. Tukatengeneza utaratibu unaosema wapate asilimia 4.5 ya fedha zinazokuja kama misaada ya kibajeti. Kwa misaada ya bajeti wapate asilimia 4.5; hawajawahi kupata hata hiyo, haijawahi kutokea. Kwenye misaada ile ambayo sio ya kibajeti, hela za *basket fund* na hizo tunawapa kwenye *budget support* na *budget support* wazungu wameiondoa, hiyo *general budget support* imeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Zanzibar miaka yote wanasema hatupati mgao wetu halali na ndiyo maana iliundwa Tume ya Pamoja ya Fedha mwaka 1984 wakati Jumbe anaondolewa madarakani. Ndiyo maana Katiba iliingizwa maneno kwamba kutakuwa na *A Joint Account* (Akaunti ya Pamoja) ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ili kutatua hili tatizo la Zanzibar kutopata mgao wake miaka yote, tangu mwaka 1984 halijashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha ilipendekeza tangu mwaka 2006 ikarudia tena mwaka 2010, tutatue matatizo ya mgawanyo wa mapato ya Muungano, haijatokea. Na kama kuna sababu kubwa ya *resentment* juu ya Muungano ya Wanzanzibari ni hii. Sasa badala ya kutibu magonjwa hayo, badala ya kutibu matatizo hayo, tunapendekeza hivi, wawe wadeni wetu wa kudumu. Wakitaka hela za maendeleo waje tuwakopeshe. Tuwakopeshe sawa na UDA, tuwakopeshe sawa na *ATCL,* tuwakopeshe sawa na Halmashauri ya Wilaya ya Newala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza utaratibu ambao utazaa matatizo makubwa zaidi ya Muungano na hatuwezi tukafanya hivi tukiwa; *we can only do this if we are blind.* Tunaweza tukafanya hivi kama ni vipofu, na kama hatujui lakini kama tunafahamu matatizo ya mgawanyo wa mapato ya Muungano *this is not the way to go.* Tafadhali sana tusitegemee nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chombo cha Kikatiba kimeundwa tangu mwaka 2003 lakini kilitungiwa sheria mwaka 1996, miaka 20 iliyopita. Tume ya Pamoja ya Fedha, chombo cha Kikatiba, hiki ndicho kinatakiwa kifanye

maamuzi juu ya masuala haya; mikopo, misaada na dhamana za Serikali ya Muungano kwa fedha za Muungano kwa ajili ya mambo ya Muungano; haijawahi kufanya kazi, badala yake tunaletewa vitu kama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mimi sijui nisemeje, lakini naomba niwaambieni Waheshimiwa Wabunge tunatengeneza bomu, na tunalitengeneza tukiwa na macho meupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho la mapendekezo ya Sheria ya Wanyamapori. Ni hivi, muswada huu unapendekeza kwamba mtu akituhumiwa kwa nyara ya Serikali, amekamatwa na nyamapori, kabla hajapelekwa mahakamani, kabla hajashtakiwa, hakimu atoe kibali, hiyo nyamapori iuzwe au ipikwe iliwe au iwe *otherwise disposed*. Halafu hakimu akishaamua kumbuka kesi haijafunguliwa, kibali cha hakimu tayari ni ushahidi kamili wa jambo litakalobishaniwa, endapo hiyo kesi itafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijawahi kuona ni mwanasheria kidogo, wanasheria waliomo humu ndani hebu nisaidieni hiyo ni ya wapi ambapo ushahidi unakubaliwa kabla kesi haijafunguliwa? Ni ya wapi hiyo? Mwanasheria Mkuu wa Serikali *seriously* unatuletea hii, nani atakayepona? Maana utafungwa tayari hakimu ameshakubali ushahidi, kabla mwenyewe hujashtakiwa, nani atakayepona? Kuna *safeguard* zipi dhidi ya watu watakaosingiziwa? Nchi hii kama hamfahamu magereza yamejaa, yamefurika kwa watu wanaosingiziwa kesi za ajabu ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunahalalisha mambo hayo Waheshimiwa kwa kuleta mapendekezo kama haya. Nyamapori, hakimu anasema eeh nimeshaona hii ni ushahidi tayari, kabla kesi haijafunguliwa umekwenda na maji.

Waheshimiwa Wabunge, hili si tatizo la CHADEMA, sio tatizo la UKAWA, tunawatengenezea Watanzania mazingira ambayo watakandamizwa sana, tusikubali. Tusikubali kuambiwa nia njema itawaumiza watu wetu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Tundu Lissu, tunaendelea na Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kuchangia, napenda nichukue nafasi hii na mimi kuwapongeza Wabunge wenzetu hawa wanne; Mbunge wa Jimbo la Dimani Mheshimiwa Juma Ali Juma, na walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, rafiki yangu Profesa Palamagamba Kabudi na rafiki yangu Abdallah Bulembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme tu mimi na ninaamini kwa Wabunge wote tunawahakikishia ushirikiano wa karibu na niwatakie kila lililo jema katika shughuli zenu za Ubunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili niishukuru sana Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa muswada huu, amewasilisha vizuri shabaha ya muswada huu, marekebisho yote ambayo yamebebwa na muswada huu katika sehemu mbalimbali. Ni muswada mzuri na huwa nasema mimi mara nyingi humu Bungeni, uzuri wa sheria yeyote ni pale unapoanza kuitumia ndipo utaona. Mojawapo kazi kubwa ya Bunge hili ni kutunga sheria, hatuwezi kuogopa kutunga sheria kwa kusema kwamba kitu hiki kimeletwa haraka sana, lakini tunapaswa sasa tuwe watulivu na tujenge hoja ambazo zinaweza zikaboresha muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namheshimu sana rafiki, msomi mwenzangu Tundu Lissu, kayasema mazuri tu mengine. Lakini mimi ningesaidia kama angeenda *step further* kutusaidia hapa kifanyike nini? Ame-*fall shot* ya hiyo, *because* hata mimi hapa naweza nikalalamika tu hapa, lakini nikishamaliza kulalamika hatujalisaidia Bunge, hatujasaidia nchi, lakini bado tuna muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu mimi nitajielekeza kwenye eneo moja tu hili la mikopo, dhamana na misaada ya Serikali. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mikopo ya nje na dhamana inayotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mikopo hiyo, suala la Muungano, hasa utatungaje au utaletaje sheria ambayo inakinzana na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana inayoweza kwenda kukopa nje, ni ile *sovereign* inayotambulika Kimataifa, ambayo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kupitia muswada huu inapendekezwa angalau tufanye utaratibu ambao utawezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenda kupata mikopo hii, lakini kupitia mgongo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 kilichoandikwa, tena kimeandikwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yaweza *(may),* mahali ambapo yule mkopeshaji anataka aone kwamba kuna mkataba wa kuhamisha zile pesa kwenda kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni matakwa ya *lender* yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali halisi uendeshaji wa Serikali na kutafuta mikopo duniani hauendi katika hili mnalotuambia hapa. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza ikaenda mahali pa *source* ambayo haihitaji kupitia mlango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama *lender* yule hahitaji masharti hayo, hakuna tatizo kabisa! Hakuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwadanganye Watanzania kwamba eti mlango umefungwa, ni pale tu ambapo mkopeshaji yule anasema, hapana mimi nadhani wewe unapaswa upitie mlango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni masharti ya mkopaji kwa sababu yeye anasema wewe nataka uje na kofia ya *sovereign state*. Sasa mimi hata tungeliongea mpaka asubuhi misingi ya sheria za kimataifa ndiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapo *on-lend* (kufaulisha) lazima yale masharti ya mkopo, ule mkopo mama, lazima uyazingatie unaweza ukayapeleka yakawa juu zaidi, tumefanya kwa mashirika mengi ya umma hapa. Kile ambacho Serikali ya Jamhuri ya Muungano inakopa kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Afrika au kokote kule, kwa sababu kuna gharama ya kutoa ule mkopo kwenda kwa yule. Lakini pia kama una uwezo unaweza ukatoa kwa masharti nafuu, maana yule wa nje yeye hajali, mkopo unapoiva lazima ulipwe *in full*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada kiko wazi. *Lender* yeyote wala hahitaji kujua kama ukopaji wenu umezingatia matakwa ya sheria ya Tanzania, na ndio uzuri wa sheria hii kwamba inawalinda wale waiamini Tanzania kwamba ukiikopesha Tanzania hata yule aliyetoa zile pesa uka-*on-lend* aki-*default* lakini bado unaikamata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huo ndio utaratibu. Kwahiyo, nadhani Mheshimiwa Tundu Lissu unanielewa ninachokisema iki-*default* ni nini anaye-*default* katika hali hiyo ime-*default* Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yetu ya ndani tuyaache ya ndani, katika hali hiyo inakuwaje, itakuwa ni mara ya kwanza hii? Mbona tunadaiana tu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa inatudai nafahamu mimi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaidai Zanzabar na mashirika mengine, wanadaiana ni

masuala ya biashara mengine mengi hayo. Sasa ukiongelea *TANESCO* tunadaiana, *TANESCO* wanaidai bilioni 60 lakini yote haya Tanzania itaendelea kuwepo tu leo na kesho na kesho kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi ni kuweka utaratibu ambao mhusika ataambiwa kwamba tulikubaliana haya na haya, wataketi kitako. Suala la misaada nakubaliana na Mheshimiwa Lissu lilikuwa na maneno neno sawa, lakini mimi siamini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina wasemaji wake. Msemaji wake mkuu ni Rais wa Zanzibar na washauri wake. Lakini mimi ushauri wangu kama mnasumbuka kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekwa kwenye sehemu ya *parastal local government* unaweza ukaiondoa tu ukaipatia kifungu cha peke yake. Lakini lengo likawa ni ku-*on lend*, misingi ni ile ile, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisaidie kwenye maeneo machache ya kiuandishi. Ili tuende pamoja na Waheshimiwa Wabunge nitumie muswada kama ilivyokuwa *published* na Serikali tarehe 21 Oktoba, 2016. La kwanza nimemsikia *AG* wakitoa *definition* mpya ya mikopo inayotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametoa *definition* ambayo katika *schedule of amendment* mnaiona *resident sources* lakini *nonresident sources* haipewi *definition*. Pamoja na kwamba hii ni *definition* ya *IMF* lakini mimi napata shida kidogo kwa sababu mikopo, tunayoiongelea ni mikopo ya *sovereign state, sovereigh borrowing*. Sasa unaposema *non-residents* tutakapoenda kwenye ukurasa unaofuata maana yake ni nini? Mnatuchanganya kweli kweli. Mimi ningelipenda ile *non-residents source* na yenyewe ipewe *definition*, ili tukae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya marekebisho kwa sheria iliyopo, na lazima tutumie *terminology* ambazo zimo na zimepewa *definition* au zimetumika *throughout* kwenye sheria ya sasa, sheria mama. Ukichukua *schedule of amendment primary loan* wanasema *means any loan secured by the government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *secured* hatujawahi kulitumia katika sheria hii, tunatumia neno *raise, you raise a loan*. Nimeona maneno mengine utayaona *contracted* haya maneno hatujawahi kuyatumia katika sheria hii. Ni vyema tukawa na mtiririko ulio sahihi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, nimemsikiliza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu alipokuwa anasoma hotuba yake nzuri, anasema neno

*stock or stocks* vifutwe lakini maelezo sikuyapata vizuri, labda naweza nikasaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wanasheria na wafanyabiashara, kwa ngazi za kimataifa, na kule tulikotoa sheria hii neno *bonds* ukienda kwa Waingereza *traditionally* maana yake ni *stocks* na ndiyo maana sheria hii ilikuwa inatumia yote na kwa vile sasa tunataka kwenda kukopa kwenye Soko la Fedha la Kimataifa mimi ninaomba sheria hii ichukue sura pia za nchi nyingine ambao tutaenda kwenye masoko yao ya fedha, nashauri tusiiondoe *definition* ya *stock or stocks.* Lakini kama mnaiondoa, sasa msiiondoe kwa utaratibu mliotumia wa *short hand* maana tutapata matatizo, ningependa wanasheria wa ofisi yako wakusaidie *AG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukienda ukurasa wa 7, 8 na 15 unapokuta maneno hayo yalivyotumika ukifuta tu neno *stock* yanayobaki hayana maana. Kwa hiyo, kama mnataka kwenda kwa namna hiyo lazima muifuatilie sheria kila kifungu muone ilivyokaa na muionyooshe ikae vizuri, ndio ushauri wangu katika eneo hilo. Lakini ningekuwa mimi ningeomba sana tusi-*disturb environment* ya mikopo na hasa tu kule tunakoelekea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja ukurasa wa tano wa muswada. Nimeyaeleza yaliyoko kwenye tano pale, kama tungependa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isionekane, *or* tuandike ka-*paragraph* kanakosimama peke yake; lakini inaongeza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashuka kidogo ya *stocks* nimeiongelea, nashuka tena kidogo *foreign loan means any loan contracted;* nimesema tutumie maneno *raised throughout* ambayo ndio maneno ambayo yako kwenye sheria ya mikopo. Tunashuka kidogo, kwenye 6(b), mimi hapa nakubaliana sana na Serikali kwa sababu *concession loan* zimepungua sana, mikopo ya masharti nafuu, na Mheshimiwa Waziri wa Fedha huwa anatukumbusha mara nyingi hapa Bungeni.

Sasa hivi dunia hii inaenda kwenye mikopo ya kibiashara zaidi, lazima tuyakubali haya; mimi nayakubali hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposhuka chini kwenye kile kifungu kipya cha 2 kinachopendekezwa hapo ndio sasa nimepata shida sana, pamoja na marekebisho ya Serikali yaliyoletwa. Kinasema *foreign loan* ambapo walipashwa waanze *a foreign loan may be raised.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge muda wako umemalizika naomba umalizie dakika moja tu.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nina matatizo na hapo hayajakaa vizuri yatatuchanganya. Maana tunapaswa tuseme, moja, *a foreign loan by direct borrowing,* pili, *non-resident*, sasa na hapo nimeshtuka kidogo, *non-residents* tuna maana gani hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unasema futa neno *issue or issue* ingiza maneno ambayo mnayaona katika ile *schedule of amendments,* inapoteza *meaning* mpaka uje tena uhangaike kuingiza *issuance of bonds* halafu ndipo uendelee. Ndiyo maana ikiandikwa vizuri inaweza ikatusaidia labda *AG* atatusaidia anapo-*windup* kumalizia kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeni-*warn* kuhusu muda wangu. Nimalizie la mwisho ni la msingi sana, ukurasa wa *6 clause* ya 8(b) kwenye *provisory* wanasema uingize neno *not* naombeni sana mkisome kifungu hicho, *is mirror image* ya kifungu cha 3 cha sheria hii. Ukisoma vizuri ule mtiririko ningekuwa na muda wote mngeona, lakini *AG* na *team* yako mimi naona mtaliona hilo hakuna haja ya kuongeza neno *not* yanajitosheleza yalivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja hii mia kwa mia, lakini ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu mojawapo ya kufanya ni kutunga sheria za nchi yetu, tuziboreshe pale tunapoona panahitaji maboresho na tunafanya vizuri, lakini tusiwe tunaendelea kulalamika katika Bunge lako haitasaidia Watanzania na Bunge lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chenge, tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye amegawana muda wake na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, tunaanza na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kwa haraka niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais pia Mheshimiwa Mbunge aliyeshinda katika mapambano makali kule Dimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nikipongeze Chama changu cha Mapinduzi kwa kuchukua karibu Kata zote katika Uchaguzi ule wa Madiwani. Hiyo imeonesha kwamba sasa kazi imeanza na njia huko mbele ni nyeupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende kwenye muswada ambapo ninataka niangalie tu katika Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato *(Income Tax Cap. 332)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sheria iliyokuwepo uamuzi wa kusamehe kodi ulikuwa mikononi mwa Waziri wa Fedha, katika marekebisho ambayo tunataka kuyafanya sasa hivi ni kwamba kwa ile miradi ambayo tunaona kwamba ni ya kimkakati na ina maslahi ya Kitaifa, basi maamuzi takwenda kufanywa katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina pingamizi lolote na hicho, lakini kimsingi maamuzi ya Baraza la Mawaziri hayawezi kupelekwa kwenye Kamati yoyote na hayawezi kuhojiwa na Kamati yoyote, kama ambavyo vile tulikuwa tunaweza kumhoji Waziri wa Fedha pale ambapo misamaha inaenda, au akivuka kile kiwango ambacho tulikuwa tunakitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba kwa kufanya katika Baraza la Mawaziri na tumesema kwamba tutaangalia miradi ile ambayo ni ya kimkakati, sasa ipi ni miradi ya kimkakati na ipi ina maslahi ya Kitaifa? Wasiwasi wangu ni kwamba inaweza ikaongeza wigo wa misamaha. Waswahili wanasema wasiwasi ni akili! Ni wasiwasi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile maamuzi ya Baraza la Mawaziri hayawezi kuombwa kwenye Kamati na hayawezi kuhojiwa kwenye Kamati, nilikuwa napendekeza kwamba basi Baraza la Mawaziri lifanye mapema maamuzi yake kabla ya mwaka wa fedha au bajeti ya mwaka unaokwenda haijapitishwa ili yale yaweze kuingizwa katika Jedwali la Misamaha ya Kodi wakati wa kujadili pamoja na *Finance Bill,* ili kusiwe na mgongano na kusiwe na matatizo yoyote. Lakini tukisema wakati bajeti inaendelea, halafu ndiyo Baraza la Mawaziri lifanye maamuzi ya kutoa misamaha ya kodi katika hiyo miradi ambayo itaonekana kimsingi ni ya kimkakati, itakuwa kwa kweli kidogo kuna matatizo kwa sababu Kamati haitaweza kuhoji wala Baraza la Mawaziri halitaweza kuhoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri, ninakubaliana na mapendekezo ya Serikali, lakini nilikuwa nashauri tu kwamba maamuzi ya

kusema miradi ipi isamehewe, itakayowezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kwa maslahi ya Taifa yafanywe mapema kabla ya mwaka wa fedha haujafika na yajadiliwe pamoja na *Finance Bill. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, sina matatizo nayo, ushauri wangu ulikuwa ni huo. Nimalizie tena kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa ushindi tuliojizolea. *(Makofi)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na nikushukuru wewe kutupa nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii ambayo iko mbele yetu. Pia kuwapongeza Wabunge wapya wa Chama cha Mapinduzi ambao wamekuja katika Bunge hili, tunaahidi kushirikiana nao kwa hali na mali. Pia ninakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa wa kishindo kilioupata katika chaguzi za Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi nijikite katika hoja hii ya mkopo na msaada. Kusema kweli, kuna msemo wa kiarabu unasema, "*maa-filbidh illa-l-barasi.*" Kwenye weupe ukisugua utatia doa. Mheshimiwa Chenge alivyozungumza Mheshimiwa Chenge nafikiri watu wote hapa wameshaelewa kitu gani kinatakiwa. Kwa kuwa niliomba kuzungumza nitarejea baadhi ya maeneo ambayo nitayazungumza kama nilivyoyaelewa mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kitu kimoja ambacho ninapenda watu waelewe katika Bunge hili Tukufu, mwanzo nilipoona baadhi ya Wajumbe wanawasilisha ile hoja nikaona labda wanaionea huruma Zanzibar kwenye mikopo, lakini kumbe wanaona itafaidika, wanaona kumbe itafaidika sasa wakaona waeleze wazi. Kwa kushangaa baadhi ya watu wengine wakapanda yule punda wa bao, hawakujua kama wanapandishwa punda wa bao, wakaunga mkono na wao. Sasa kumbe unanyimwa maendeleo katika nchi yako, unanyimwa maendeleo katika eneo ambalo umetoka wewe kwa kukosa mkopo na msaada. Kwa hiyo, sikuelewa pale mwanzo kumbe walikuwa wako *dilemma!* Sasa hivi tumeshafahamu, nafikiri acha tuendelee mbele kuwajulisha Watanzania dhamana ambayo tumepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono katika kifungu cha 12 pamoja na marekebisho ya Serikali ambayo wamekujanayo kwa sababu ya kitu kimoja. Zanzibar siyo *sovereign state* ambayo inaweza ikakopa yenyewe, tunakoelekea sasa hivi tunaenda kukopa mikopo ya kibiashara ni lazima kufanyike *sovereign credit rating* ambayo itafanyika kwa nchi na hakuna *sovereign credit rating*

ambayo itaweza kufanyika kwa Zanzibar. Kwa hiyo, kukopa kwa Jamhuri ya Muungano ni sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni muhimu ni kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watu hawaifahamu. Wanahisi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kitu mbali kabisa. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Serikali ya Muungano, kama tulivyoseme, kwa hiyo, Zanzibar imo humo humo ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hii kumetajwa Wizara ya Fedha na Waziri wa Fedha; kwa mujibu wa sheria hii kumetajwa Taasisi ya Benki Kuu na Gavana; kwa mujibu wa sheria hii kumetajwa Kamati ambayo itakuwa inashughulikia masuala ya Mikopo na Deni la Serikali. Sasa hivi vitu vyote ni vyombo vya Muungano, wakati wowote kiongozi wake inawezekana ikawa ni kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, kutokana na hayo ina maana kwamba moja kwa moja Zanzibar inaweza ikafaidika na mikopo hiyo kwa kiasi kikubwa na inaweza ikafanya shughuli zake za maendeleo na kuwapatia maendeleo wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo nilipomsikia mzungumzaji mmoja anazungumza aliposema kwamba Katiba Pendekezwa ilitaka suala hili Zanzibar iwe na uwezo wake wa kukopa, sasa leo unazungumzia Katiba Pendekezwa ambayo siyo Katiba tunayoizungumzia hapa, siyo Katiba iliyopo sasa hivi. Hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni Serikali inayoongozwa chini ya Serikali mbili, kwa hiyo mipango ambayo imo humu ni chini ya Serikali mbili, siyo kwa mujibu wa Katiba Pendekezwa. Katiba Pendekezwa au Katiba siku zote ni sheria mama kwa hiyo, haiwezekani azaliwe mtoto kwanza kwamba ili Sheria hii tuiweke hivyo kama ilivyo kwenye Katiba Pendekezwa halafu baadaye ndiyo aje azaliwe mama, hicho kitu ni cha ajabu sana! Hicho kitu ni cha ajabu sana na nilishangaa sana kumsikia mtu huyo anazungumza masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine katika masuala hayo ya kuhusiana na mikopo, kuna faida ambayo tunaweza tukaipata. Siku zote unapoenda kukopa yule anayekukopesha anaangalia *default risk* yako, kwa hiyo, kwa vyovyote vile kwa Zanzibar inapata faida kwa sababu *default risk* kwa Zanzibar ingekuwa kubwa, sasa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *default risk* haiwezekani ikawa kubwa kuliko ambayo ingekuwa kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la misaada. Ingawa kuna changamoto katika suala hili misaada, lakini sote sisi tunafahamu kwamba kuna kitu kikubwa zaidi ambacho kinaweza kikakingwa kutokana na sheria hii, sote

tunafahamu, kuna watu hatujui kama wameoteshwa au waliambiwa mzimuni kwamba, wewe kuna siku utakuwa Rais. Anapokosa tu anazunguka nchi zote kudai kwamba, Zanzibar inyimwe misaada, lakini kwa Tanzania hawezi! Kwa hiyo, faida hiyo ya misaada kwa Jamhuri ya Muungano ikiwepo na Zanzibar ni vizuri ili kuepukana na watu hao vitimbakwiri walioota au waliopata hicho kitu kutoka huko mzimuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siku zote *political risk* kwa Zanzibar baada ya chaguzi zetu zinatokea na zinasababisha suala hili kuyumba, kwa hiyo, inapokuwepo katika sheria hii itasaidia. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hiyo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania labda kuzikopesha taasisi mbalimbali. Serikali yenyewe ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania humu sote tunajua sisi ni Wabunge, pengine inakopa *NMB,* lakini hata humu Wabunge nao wamekopa *NMB.* Sasa je, wewe mtu binafsi umekopa *NMB* na Serikali imekopa *NMB!* Je, hapa kuna kasoro gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ikiwa Halmashauri, ikiwa taasisi yoyote, ikiwa kampuni yoyote, kukopa, mkopeshaji ni hiyari yake mwenyewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wako umemalizika.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika!

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa lakini wakumbuke…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mmemdundishia mpira Abeid Mziba golini....

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza mjadala huu. Sasa tunamuomba mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ili aweze kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakupa dakika chache ili uweze kuchangia, baadaye tuweze kumsikiliza Mwanasheria Mkuu ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba niwapongeze sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya kuchambua mapendekezo ya Serikali ya kurekebisha Sheria ya Mikopo na Dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ufafanuzi kidogo katika masuala mawili, matatu. Kwanza kwa lile la kufaulisha mkopo kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba niseme tu kwamba baadhi ya wanaotukopesha fedha hizi mathalani Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakupa dakika 15 na dakika 45 atamalizia Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba baadhi ya mashirika ambayo yanatukopesha, kama Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *Saudi Fund* na kadhalika wao kama sehemu ya *primary loan agreement* wanaweka sharti kwamba kabla SMT haijahamisha fedha za mkopo kwenda SMZ, yaani kwenda kwa mnufaikaji, wanahitaji kuona kwamba pana utaratibu wa kuhakikisha kwamba mnufaikaji atawajibika kurejesha zile fedha za mkopo. Kwa hiyo, ni muhimu tuelewane tuna nia njema kabisa, baadhi ya haya wala hata siyo masharti ya SMT, ni masharti ya wale wanaotukopesha. Kwa hiyo, mkiyakataa yale maana yake ni kwamba tumejifungia kupata chanzo hicho cha mkopo wa fedha nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni moja ambalo nadhani nilitaka niliweke vizuri. Lengo ni jema tu, ni kuhakikisha kwamba unawekwa sasa utaratibu wa kisheria ambao haupo kwenye sheria ya sasa ilivyo kuhakisha kwamba fedha ambazo zinakopwa na SMT kwa ajili ya miradi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinawasilishwa kama ilivyokusudiwa.

Pia lengo la pili ni kuhakikisha kwamba mkopo ule unalipwa. Tatu, ndiyo hiyo niliyoanza kueleza kwamba ni kuhakikisha kwamba yale masharti au kwa kiingereza, *condition precedent* ambayo yanatolewa na baadhi ya wakopeshaji yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia, napenda tu nisisitize kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikipelekewa asilimia 4.5 ya mgao wa *General Budget Support*. Nadhani tofauti

ni fedha za mkopo ambazo zinaelekezwa kwenye sekta maalum kulingana na mkataba kati ya mkopeshaji na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda tena nirejee kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeendelea na itaendelea kupokea mgawo wake wa asilimia 4.5 ya fedha zote za *GBS* ambazo zimepokelewa kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa miradi tumeangalia namba hizi na kwa leo mchana huu nimejaribu kuangalia deni la nje; deni la nje linaonesha kwamba kuanzia mwaka 1993 mpaka mwaka jana 2016, fedha ambazo zimekopwa na SMT kwa ajili ya Zanzibar zilifikia takribani dola milioni 772.396 ambayo ni takribani sawa na asilimia 2.59 ya deni lote la nje kwa Taifa letu. Kwa hiyo, bado tumeendelea na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, tunafanya *on landing* kwa Zanzibar. Tunachoweka ni masharti sasa ya kisheria kuhakikisha kwamba, mikopo hii inalipwa kama ambavyo tunakubaliana na wanaotukopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze pia jambo lingine la tatu kuhusu utaratibu wa Serikali ku-*on lend to Zanzibar,* kwamba itakuwaje kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itashindwa kulipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria imeweka sharti, ukitazama kifungu cha 12(3) kwenye *schedule of amendment,* tumeweka masharti kwamba kabla ya kuwasilisha mkopo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itabidi idhihirishe, i-*demonstrate prudent projections* za mapato yake hasa kwa kutazama *balance sheet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutuwezesha kujua kwamba inaweza kweli ikafikia *primary loan obligations.* Kwa hiyo, upo utaratibu ambao umewekwa, vilevile kuhusu sharti la kuishirikisha *National Debt Management Committee* ambayo itafanya uchambuzi wa lile deni kabla ya Serikali ya Muungano kufaulisha mkopo kwenda SMZ. Masharti haya yatatumika pia kwa Halmashauri na Mashirika, ni lazima kupitia ukiangalia kifungu cha 12(4)(i) cha hii sheria kinasema wazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeweka utaratibu mzuri kwa nia njema ili tuhakikishe kwamba kweli mikopo hii inalipwa na nchi yetu inaendelea kunufaika na mikopo nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze tena kuhusu madai kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imenyang'anywa mamlaka ya kupokea misaada kutoka nje. Ukitazama kifungu cha 15 cha sheria hii kimetoa mamlaka kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupokea misaada pasipo ridhaa ya Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, siyo kweli kabisa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imenyang'anywa hayo mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tulipokea mapendekezo kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kuhuisha ushiriki wa Zanzibar katika *National Debt Management Committee* na hili limezingatiwa katika mapendekezo ambayo tumeweka mbele ya Bunge lako Tukufu ambapo Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa SMZ, lakini pia Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar wote hawa sasa tunapendekeza kwamba waingie kwenye *National Debt Management Committee*. Tunadhani ni jambo jema la kuhuisha utaratibu uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni pendekezo la Mheshimiwa Chenge, kuhusu kuondoa neno *debt stock,* neno *stock*. Sisi tunakubali upande wa Serikali kama ilivyoshauriwa kwamba neno hili linaweza kuendelea kubaki, tunadhani kwamba halina madhara yoyote katika kutekeleza sheria hii. Baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na sasa namkaribisha Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ili aweze kuhitimisha hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa na kuniwezesha na mimi kuhitimisha hoja hii na kujibu baadhi ya hoja mbalimbali ambazo zimechangiwa katika Bunge lake Tukufu na Wabunge.

Kwanza niwatambue Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia muswada huu nawapongeza sana. Kwanza nitambue mchango wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ambayo ilichambua muswada huu na kuujadili na ikatoa taarifa yake kwa mujibu wa ukurasa wa 23 wa taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yaliyotolewa na Kamati katika muswada huu yamezingatia kwa kina maoni ya wadau, uchambuzi wa kitaalam uliofanywa na Sekretariati ya Bunge na majadiliano mapana kati ya Serikali na Kamati. Hivyo, Kamati inaamini kwamba sheria hii itakuwa bora na yenye manufaa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na Kamati nitambue pia mchango wa taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani na ambaye yeye pia amekiri kwamba anakubaliana na taarifa ya Kamati na niwatambue pia Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Tundu Lissu, Andrew Chenge, Hawa Ghasia, Ali Hassan Omar King na hatimaye Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo Wabunge ambao wamechangia hoja hii kwa maandishi nao naomba niwatambue. Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Mary Deo Muro na Mheshimiwa Juma Othman Hija. Kwa hiyo, hawa wote pamoja na Wabunge wote naomba kuwapongeza kwa kuweza kuchangia katika muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa niende moja kwa moja kujibu hoja ambazo zimeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa wakati wakichangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kumekuwa na dhana potofu ambayo imekuwa ikijirudia katika Bunge hili Tukufu kwamba pengine hii Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali siyo miswada mizuri. Ukweli ni kwamba miswada hii inafaa na miswada ni halali inayotambulika na mpaka sasa hakuna katazo lolote la Kikatiba au la kisheria au la kikanuni linalopiga marufuku uwasilishaji wa Miswada ya mabadiliko ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niseme kwamba Miswada hii ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ni muhimu kwa sababu siyo wakati wote inalazimika sasa Waziri alete muswada hapa unaojitegemea kwa sababu mabadiliko yenyewe hata katika sheria yanaweza yakawa ni madogo madogo; lakini mengine pia tunayoyaleta Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu yanatokana na michango na ushauri na mapendekezo ya Wabunge, badala ya kusubiri utaratibu mrefu wa kuandaa miswada inayojitegemea basi huwa tunaona kwamba tulete kwa utaratibu huu wa Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imezungumzwa juu ya tafsiri katika sheria hii. Tunavyojua ni utaratibu wa kawaida kwamba katika sheria yoyote inayotungwa kwa kawaida huwa ina kifungu au ibara ya tafsiri ni jambo jema na hili linaletwa ili kurahisisha matumizi mazuri ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sisi tunayo sheria, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, ndiyo Sura ya Kwanza ya Sheria za Tanzania, ni kuonesha

umuhimu wa kutafsiri maneno ambayo yanatumika na hasa maneno mahsusi yanayotumika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maneno ambayo yameletwa kama kutafsiri kwenye sheria hii ambayo tunaifanyia mabadiliko Sehemu ya Pili ya Muswada ya *Government Loans Guarantees and Grants Act* ni muhimu sana yakawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wameshajibu baadhi ya hoja na mimi nawapongeza. Kulikuwa na hoja kwamba Zanzibar sasa inawekwa kwenye wigo sawa na *Local Government Authorities* na mashirika mengine ya umma. Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona katika Jedwali la Marekebisho kifungu kile kimeandikwa upya sasa Zanzibar inasimama peke yake na masharti yake na tumeondoa katika sehemu vifungu vile vilivyokuwa vinatajwa pamoja na hizi taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali letu la Marekebisho limeeleza vizuri na Mheshimiwa Chenge amefafanua vizuri juu ya hoja hii inayosema kwamba Zanzibar sasa itakuwa pamoja sawa hadhi na hayo mashirika, hapana. Kwenye Jedwali la Marekebisho tumeiandika upya ile Ibara ya 12 ambapo wala hata siyo lazima, tumetumia neno "*may*" isipokuwa Zanzibar pale ambapo tu huyo mkopeshaji anataka tuwe na utaratibu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar kuwa na mamlaka ya kukopa hili nalo nimeshalitolea ufafanuzi humu, bado suala la mikopo ya nje ni la Kikatiba, muda utakapofika basi Zanzibar itakuwa na mamlaka yake ya kukopa ikiwa imejitegemea yenyewe. Mheshimiwa Chenge ametoa ufafanuzi mzuri kuhusu suala hili, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ametoa ufafanuzi kuhusu suala hili. Kwa hiyo, Waheshimiwa naomba muunge mkono hoja hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa Mheshimiwa Juma Othman Hija akiunga mkono hoja hii, yeye ameshauri kwamba kutokana na uchumi wa Zanzibar kutokua imara sana basi wakati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapokuwa na utaratibu huu waaangalie uwezekano wa kuiwekea Zanzibar masharti yenye wepesi na hiyo ni hoja nzuri, itategemea labda masharti pia kutoka kwa huyo anaetukopesha anasema nini. Lakini ni mchango mzuri na sisi Serikali tunaupokea ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Bashungwa kwa mchango wake mzuri, kiujumla tunakubaliana na ushauri wake na tunakubaliana na mchango wake, isipokuwa tu tuseme kwamba kwenye hili

suala la elimu kwa ajili ya mikopo ya juu, kupanua wigo; lengo la muswada huu katika sehemu ya tatu inaporekebisha hiyo Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni kuongeza huo wigo kwa sababu sheria jinsi ilivyo sasa hivi imefunga kwenye hayo maeneo yanayotajwa kwenye hicho kifungu, lakini kwa kumpa Waziri sasa mamlaka kwa kuangalia vipaumbele vya Taifa; wigo kwa watu wanaostahili kupata mikopo utaongezeka, ni ushauri mzuri kwa Serikali na sisi tunaupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa hili la kwamba taasisi za kidini kupata msamaha wa kodi pengine hili naomba kushauri kwamba hili ameliwahisha sana labda tutalifikiria wakati wa Muswada wa Sheria ya Fedha, linapaswa ombi kama hilo lije labda wakati wa Muswada wa *Finance Act* wakati wa kutunga Sheria ile ya Bajeti, lakini haliwezi likaingizwa kwenye muswada huu wa sasa na hiyo pia itakuwa kama Wizara yenye dhamana na kusimamia hii sheria itakubaliana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye alitumia muda wake mrefu kuzungumza juu ya Sheria hii ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada. Lakini pia ndani ya Bunge hili tumepata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Ali King na Wabunge wengine waliochangia kwamba, moja, Zanzibar haifanywi sasa kuwa mdeni wa kudumu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu kwanza tulishakubaliana tangu mwanzo kwamba suala la mikopo ya nje ni suala la Muungano, hiyo ni sababu ya kwanza kwamba inaifanya Zanzibar isiwe mdeni wa kudumu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, siyo wakati wote Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa inakopa na utaratibu huo uliowekwa kama ambao tumekwisha ufafanua ni pale ambapo hata hao wanaotukopesha watakapokuwa wameweka kwamba hili nalo ni sharti la mikopo na Zanzibar kwa maana ya kifungu kilichoandikwa pale inao utashi wa kukataa au kukubali. Lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hizi ni Serikali ndugu. Kama kuna jambo lolote la maslahi ya Zanzibar hizi pande mbili huwa zinakaa na kuelewana. Mheshimiwa Chenge amelifafanua vizuri sana hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii ya kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishindwa kulipa itakuwaje, hata jinsi muswada ulivyoandikwa pale hakuna sehemu yoyote ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema ikishindwa kulipa inawajibika, uwajibikaji umewekwa kwenye taasisi za Serikali. Kwa hiyo, Wabunge naomba tuelewane kwenye hili, hakuna

sehemu katika muswada huu pale ambapo inatolewa adhabu, ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshirikishwa. Zilizoshirikishwa hapa ambazo zimehusishwa ni taasisi za umma ambazo kwa mujibu wa sheria hii ni Mashirika ya Umma na *Local Government Authorities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaenda kuwajibishwa, utaiwajibishaje? Hawa ni ndugu na nchi moja, hakuna namna ya kuiwajibisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na mchango hapa kuhusu *Joint Finance Commission.* Katika muswada huu hakuna hata sehemu yoyote tunayozungumzia hili suala. Kwa hiyo, ni mchango ambao pia umeletwa pengine mapema zaidi haukuwa sehemu yake na wala hapa pia hatuzungumzii *General Basket Fund*, haiingii kwenye sehemu yoyote ya muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii hoja Mheshimiwa Tundu Lissu pia kulikuwa na mchango kuhusu hoja ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ambapo ilidaiwa kwamba sasa ushahidi ukishakuwa *tendered* tu pale mahakamani, mtuhumiwa anapatikana na hatia na kufungwa, hiyo siyo kweli. Lakini msingi wa sheria yenyewe hii nini? Ni kwamba kuna vitu vinaharibika haraka kwa mfano nyara za Serikali, sasa hizi nyara za Serikali zinazoharibika haraka, mpaka usikilize kesi ianze kuisha yule mnyama atakuwa ameshaharibika na hajulikani, kesi itamalizika lini?

Kwa hiyo, tumeweka utaratibu hata pale ambapo kesi haijaanza badala ya hayo mambo kufanywa na Mkurugenzi wa Wanyamapori kama ilivyokuwa na Mahakama ya Rufaa ikakataa, iende Mahakamani sisi tutoe pale huyo mnyama kama ni mnyama hiki kitu ambacho kinaweza kikaharibika haraka, Mahakama iamue ikione itoe maamuzi kwamba hiki sasa jinsi kilivyo kikikaa hivi kitaharibika, kiharibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itatumika kama ushahidi wa kuwepo kitu hicho siyo ushahidi wa kwamba huyo anayekwenda kushtakiwa kama atashtakiwa itakuwa ni ushahidi wa kuthibitisha dhidi yake kwamba ametenda lile kosa. Kwa sababu kama ni masuala ya wanyamapori, kwanza kosa hapa ni suala la kukutwa na umiliki, kukutwa na vile vitu isivyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ni ushahidi ambao utakuja kutolewa Mahakamani baadae kwamba je, huyu mnyama alieletwa hapa

Mahakamani wewe Bwana ndiyo ulikutwa naye huyu? Kwa hiyo, ni kitu kingine tofauti na huo ushahidi kama atashtakiwa utakuja kutolewa huko baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wayakubali mapendekezo ya muswada huu kama yalivyowekwa. Kusema ukweli kwenye Kamati namshukuru Mheshimiwa Tundu Lissu walitusaidia sana walipokuwa anahoji jinsi muswada huu ulivyokuwa umeandikwa na mimi nikawaahidi kwamba naenda kuuboresha, nimeuboresha muswada huu vizuri kabisa na Kamati imeridhika na Mheshimiwa Tundu Lissu naye amekubaliana na Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi ilivyo sasa hivi na sisi tunaleta uwazi, Mheshimiwa Tundu Lissu angeweza kuona ile sheria ya Kenya angeogopa, maana hata wakati natafuta kuboresha muswada huu nilipata hiyo sheria ya Kenya wenzetu wanafanyaje, ila Waheshimiwa Wabunge siyo vema kusema kusema sheria za nchi nyingine lakini ile isingetusaidia. Sisi tunataka *transparency and accountability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema hapana, hii *scheme* ya Kenya tuiache tutumie hii ya leo ya sasa na ndiyo maana tunaenda hata mahakamani, ni lazima Waheshimiwa Wabunge tuiheshimu mahakama. Sasa Mahakama nae ataenda kumbambikiza huyo mtu? Kwa sababu kwanza pale mbele wakati huo hakuna hata ushahidi, lakini pia utaratibu huu kwenye kifungu cha 2(d) ndiyo utaratibu ambao upo kwenye Sheria yetu ya Mashauri ya Mwenendo wa Jinai, kwenye kifungu cha 353 kinaweka utaratibu wa aina hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kukubaliana na hoja ya Serikali kwamba haya nayo jinsi yalivyoletwa Muswada huu na kama unavyoonekana kwenye Jedwali pale tukubaliane. Pia Serikali imewasilisha Jedwali la ziada kwenye hiki kipengele maana kilikuwa kiko wazi tu hivi; sasa tumesema hapana, mahakama iseme atakayekwenda kuharibu hiyo basi awe ni Mkurugenzi wa Wanyamapori na siyo mtu mwingine yeyote yule na ndiyo utaratibu na *scheme* ya sheria hiyo. Waheshimiwa Wabunge naomba mkubaliane na hoja hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa ujumla ameunga mkono hoja hii na ametoa ushauri na haya mambo mengine ni ya msingi sana tutayazingatia ndani ya Serikali. Pia Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ameunga mkono hoja hii na akafafanua vizuri sana ninamshukuru.

Mheshimiwa Chenge pamoja na kuunga mkono ametushauri vizuri matumizi ya maneno *"secured"* popote pale yanapoonekana kwenye Muswada huu yaondolewe *"secured or contracted"* na badala yake yaingizwe maneno *"raised"* na sisi tunakubaliana na ushauri huu wa mchango wa Mheshimiwa Andrew Chenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nifafanue kwamba Mheshimiwa Chenge hakuwa na uhakika tulipokuwa tunasema kwamba tunafuta yale maneno *stock,* ukweli ni kwamba kwenye Muswada ulivyoandikwa mara ya kwanza tulikuwa tunaondoa lakini tulipoenda kwenye Kamati tukashauriwa, hivyo kwenye Jedwali la Marekebisho hayo maneno *stock* yaani tunayafuta hayapo tena, yaani hatuyaondoi kwenye sheria, yanabaki yalivyo. Inaonekana vizuri zaidi kwenye hili Jedwali la Marekebisho, tunaondoa kwenye ule Muswada ndiyo maana ya kwamba tunayafuta pale, kwa hiyo Mheshimiwa Chenge kwenye hili tupo pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mary Muro, Mbunge wa Viti Maalum, ameishauri Serikali kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kukopesha wanafunzi wote. Serikali inaupokea ushauri huu ni ushauri mzuri, kama mnavyoona wakati fulani Serikali inakuwa na mambo mengi, lakini pale ambapo uwezo unaruhusu haya ni mambo mazuri ya kutekelezeka. Nia ya Serikali ni kwamba watu wake wote wapate elimu, kwa hiyo, ushauri huu wa Mheshimiwa Mary Deo Muro, tunaukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunakubali ushauri wake kuhusiana na marekebisho ya Sheria ya Sukari, ameshauri kwamba wakulima wadogo wadogo wa miwa washirikishwe kikamilifu katika kuandaa sheria zinazowahusu. Hili ni jambo jema na tumeambiwa na Kamati asubuhi umuhimu wa kuwashirikisha wadau wote wakati tunapotunga sheria, ushauri huu nao ni mzuri Mheshimiwa Muro tunaukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, amependekeza kifungu cha 7A kinachoweka masharti ya wakulima kupata kibali cha bodi kabla ya kujiunga katika Vyama vya Ushirika kirekebishwe ili kuondoa masharti hayo, na sisi tumekubali, hili limezingatiwa kwenye Jedwali la Marekebisho. Alishauri pia kuhusu Ibara ya 41 ambayo inapendekezwa kifungu cha 11A kinachoweka masharti ya kushauriana kabla ya kupanga bei elekezi kifanyiwe marekebisho ili kuwahusisha wadau wote. Huu ni ushauri mzuri tumeuzingatia uko kama unavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho. Pia alishauri Ibara ya 42 inayopendekeza kifungu cha 17A kirekebishwe ili kuweka hatua mbalimbali za ukataji wa rufaa kutoka kwa Bodi

kwenda kwa Waziri na kutoka kwa Waziri kwenda kwa Mahakama Kuu. Ushauri huu pia tumeuzingatia kama unavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ushauri pia kupitia hayo Majedwali ya Marekebisho na haya yanamhusisha Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, amependekeza Ibara ya 40, kifungu cha 7A kirekebishwe kwa kuondoa neno *may* na kuweka neno *shall* ili Bodi ilazimike kuongeza muda wa kusajili wakulima wa miwa. Marekebisho haya ni mazuri lakini kuna shida moja. Moja, tukikubali hili pendekezo maana yake ni kwamba itakuwa ni lazima tu Bodi iwe inaongeza hata pale ambapo hakuna sababu, ndiyo msingi wa kutumia neno *may*. Kwa hiyo, mamlaka ya Bodi ya kuongeza muda wa usajili yatategemea mazingira yaliyopo, hivyo ni sahihi kuacha neno *may* kama ilivyo kwenye kifungu hicho cha 7A(3) ili huu muda uongezwe pale ambapo mazingira yataruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Sware pia alikuwa na mapendekezo kwenye Ibara ya 42 ambapo inapendekezwa kifungu cha 17A(1) kifanyiwe marekebisho kuongeza muda wa miezi isiyozidi 12 kwa ajili ya kuwasilisha mpango wa maendeleo. Mapendekezo haya japokuwa yalikuwa na nia njema, kwa kuwa tayari kifungu cha 17A kinaipa Bodi mamlaka ya kupanga muda wa kuwasilisha mpango wa maendeleo kwa kadri Bodi itakavyoona inafaa, hivyo basi, Bodi inaweza kupanga miezi hiyo inayopendekezwa au vinginevyo kutegemea na hali itakavyokuwa kwa sababu hili ni suala linalohusisha wadau wengi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba Bodi imepewa mamlaka pia ya kuwa inasimamia utekelezaji wa mpango huu, pendekezo hili japokuwa lilikuwa zuri, lakini sheria jinsi ilivyoandikwa sasa hivi inakidhi matokeo ambayo Mheshimiwa anayapendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Dkt. Sware pia amependekeza kwamba Ibara ya 17A inapendekeza aya ya (b), (c) na (d) zifutwe. Mapendekezo hayo tunasita kuyakubali kwa kuwa aya hizo zinaainisha mambo muhimu ambayo yanatakiwa kuzingatiwa katika mpango wa maendeleo ili kuweka muundo wa andiko la mpango huo kufaa. Pia Mheshimiwa Dkt. Sware alikuwa na mapendekezo kuhusu Ibara ya 45, inapendekezwa kifungu cha 45(1)kifanyiwe marekebisho kuondoa neno *Director* na badala yake kuweka Kituo cha Polisi *(Police Station)*. Tunakubali kwamba haya ni mapendekezo muhimu lakini kwa sababu mtekelezaji wa sheria hii ni Mkurugenzi wa Wanyamapori, badala ya kuweka Polisi tumuweke Mkurugenzi wa

Wanyamapori na ndicho ambacho tumefanya Serikali kupitia hili jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Mdee naye alipata fursa ya kuchangia kwa kuboresha alipoleta Jedwali la Marekebisho ambapo yeye alipendekeza kwamba Ibara ya 19(3) kifanyiwe marekebisho kinachoweka masharti ya mtu mwingine kuhudhuria kikao cha Kamati ya Taifa kwa niaba ya Mjumbe aondolewe ili Mjumbe mhusika ahudhurie mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yalikuwa muhimu kwa kutaka kuwawajibisha watu wa-*take this matter seriously,* lakini ukiweka utaratibu huo itafikia hatua tutakwama kwenda na utaratibu wa uwakilishi ni utaratibu wa kawaida isipokuwa tumeweka masharti kwamba huyo anayeenda kumwakilisha huyu Mjumbe wa Kamati tumeweka zile sababu za msingi pale, basi awe ni Afisa Mwandamizi, kwa mfano kama *Attorney General* hivi ni Mjumbe wa ile Kamati, kama hayupo basi aende *Deputy Attorney General* ndiyo msingi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mdee tunashauri ukubali tu ushauri wa Serikali Muswada jinsi ulivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa na mapendekezo pia kuhusu Ibara za 35 na 36, kwamba marekebisho yafanyike katika vifungu hivi ili kuondoa tozo inayopendekezwa. Kama utakavyoona mapendekezo haya hayahitajiki tena kwa sababu Serikali tayari imeshaondoa sehemu hii katika muswada ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 41 pia alipendekeza kwamba kifungu cha 11A kiongezwe masharti ya kuitaka Bodi izingatie mazingira ya uzalishaji kabla ya kupanga bei ya sukari. Nia yake ilikuwa njema lakini mapendekezo haya yanaweza kuleta athari kama yatakubalika kwa sababu masharti yanaweza kuzingatia wakati wa mashauriano baada ya Waziri, Bodi na wadau kama ilivyo katika Jedwali la Marekebisho. Pia jambo la pili hapo, hatuangalii tu masharti ya *production,* kuna vitu vingi vinatazamwa pale, siyo uzalishaji tu kwa hiyo tuiache sheria jinsi ilivyo ibaki hivyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 42 alikuwa na mapendekezo kwamba kifungu cha 17A kirekebishwe ili kuweka hatua mbalimbali za ukataji wa rufaa kutoka kwa Bodi kwenda kwa Waziri na

kutoka kwa Waziri kwenda kwa Mahakama Kuu. Pendekezo hili limeridhiwa na Serikali kama inavyoonekana katika Jedwali hili la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa mara nyingine tena nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kusimamia Mkutano huu vizuri na kwa hekima na ninawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia na Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia amani na kuwabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Katibu tuendelee na utaratibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2016 *[The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.4) Bill, 2016]***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa)*
*(Ibara zinazofuata zimebadilika namba kwa kuwa Ibara ya 7 imefutwa)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 18

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa *AG* alikuwa anajaribu kunijibu, nimeomba yafanywe mabadiliko kwa kufuta maneno mapya yote yaliyoongezwa ambayo yanasomeka kama ifuatavyo; *In sub clause (3), by deleting the words "and where a member by reason of illness, infirmity or absent from the United Republic, is unable to attend any meeting, he may appoint a Principal Officer to attend such meeting on his behalf."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bunge hili tumekuwa tukitunga sheria mbalimbali ambapo, ama tunaanzisha Bodi, Mabaraza ya Ushauri au Kamati mbalimbali zenye Wajumbe, lakini sijawahi kuona katika sheria yoyote tuliyopitisha kwenye Bunge hili ambapo Wajumbe wa Bodi ambao wameteuliwa na sheria wanapewa jukumu la kukasimu yale mamlaka yao kwa mtu mwingine, hii ni mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Kamati Maalum ya Kitaifa ya Usimamizi wa Deni la Taifa, na kwa unyeti wake, hii sheria katika kifungu cha 18 kimeeleza Wajumbe wake ni akina nani ambao ni Makatibu Wakuu wa Wizara nyeti mbalimbali zaidi ya kumi. Sasa hivi nchi yetu ina *crisis* kubwa ya Deni la Taifa, deni limekuwa likiongezeka, tumekuwa tukipata majibu yasiyoridhisha Serikalini, lakini Kamati hii nyeti tunaambiwa i-*delegate* majukumu yake kwa watu wengine kwa kigezo cha ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kifungu cha 22 hawa watu wanakutana kwa *quarterly basis* tu, sasa watu wanaokutana mara moja kwa miezi mitatu ama katika mazingira machache ambayo kuna ulazima, kuna haja gani ya kutoa fursa pana ya kutoa ombwe la kuita watu wengine ambao utasababisha vikao hivi nyeti kunakuwa hakuna *continuity,* tunazungumzia kutoa *Government guarantees,* tunazungumzia mikopo mikubwa ya ndani na nje. Amewekwa Katibu Mkuu, sheria inasema Katibu Mkuu asipokuepo, sijui anaumwa, sijui amekwenda nje na tumeambiwa sasa hivi Rais si hasafiri, akienda sana anaenda Ethiopia pale, sasa hao Makatibu Wakuu watakuwa wanaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii sheria hizi *amendments* ambazo amezileta, *quorum* ya kikao ni *half of the members.* Sasa hawa Wajumbe kwa mujibu wa sheria hii wako kumi, *half of the members* ni watano, yaani mnatuambia katika hivi vikao vya miezi mitatu, mitatu ambavyo vinajulikana viko kwenye ratiba, hao watu watano wote watakuwa ni wagonjwa ama wamesafiri ama wana sababu nyingine yoyote.

Ninaomba Serikali watoe hiki kifungu kwa sababu hakina mantiki, sana sana kinaenda kutengeneza ombwe kwa watu wengine kushiriki kwenye vikao ambavyo vinahitaji watu ambao wako *sober* na wamepewa nyadhifa kubwa na ni ma-*Accounting Officer* kwenye Wizara zao ili kuweza kulisimamia suala hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia muda umekwisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu au Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya tumeyaleta kwa kweli kwa kuangalia hali halisi ilivyo. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amejaribu kutoa, maana yeye ni Mjumbe wa ile Kamati, *practically* kumtarajia kwamba kila kikao Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwepo ni vigumu kabisa.

Kwa hiyo, kilicho cha muhimu ni kuhakikisha kwamba anayekasimiwa kwenda kwenye hicho kikao anakuwa ni Afisa wa Serikali ambaye ana hadhi ya kwenda kule na amelitolea mfano vizuri kabisa kwamba kwa nafasi yake yeye *Deputy Attorney General* ambaye ni *very Senior Government Official* ndiye anamkasimu aende, pale ambapo hataweza kupata nafasi, kadhalika Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania ukimtarajia awepo kwenye kila kikao cha *National Debt Management Committee* haitawezekana.

Kwa hiyo, mimi namuomba sana Mheshimiwa Halima Mdee, ni suala la kuwa *practical,* siyo suala la kuwa mtu anaacha madaraka haya ambayo ni makubwa na yenye thamani kubwa katika kusimamia Deni la Taifa, imewekwa tu hivyo na hawa ni *responsible officers,* napenda kuamini kwamba hataacha kwenda wakati yupo Dar es Salaam au yuko Dodoma kwa kuwa tunahamia hapa, akaacha kwenda kwenye kikao kama kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuomba tu atukubalie mapendekezo tunayoleta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, unakubaliana na Mheshimiwa Waziri?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Waziri hajanielewa. Nimesema hivi, kwanza ukiangalia kwenye sheria *quorum* ya kikao

ni Wajumbe watano, Wajumbe ambao wametajwa kwenye hii sheria ni Wajumbe kumi, kwa hiyo katika mazingira yoyote yale haiwezekani katika Wajumbe kumi, Wajumbe watano wasiwepo. Kama *AG* hayupo wengine watamwakilisha, kama Gavana hayupo, wengine watamwakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelizungumza hili kwa unyeti wa kitu anachokisimamia. Hakuna mtu ambaye hajui nchi yetu na Deni la Taifa sasa hivi, hakuna mtu ambaye hajui kwamba tuna shida ya kulipa Deni la Taifa. Hata taarifa zenu zinaoneshwa kwa sababu uchumi wetu hauko katika utaratibu wa kuweza kulipa vizuri, hauwezi kujiendesha vizuri. Tunahitaji watu *sober*, tunahitaji mwendelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo anakuja Katibu Mkuu, kesho anaenda Afisa Mwandamizi, kwa sababu tumeambiwa ni Maafisa Waandamizi, leo anaweza akaja Mussa, kesho kutwa akaja Rajabu, lakini hawa watu wamepewa hizi nafasi kutokana na *title* zao, hivyo Katibu Mkuu akiondoka anakuja mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa hii Sheria ya *Government Loans Guarantees and Grants,* kifungu cha 22 kimesema; mnakutana *on quarterly basis* na *quarter* ya Kiserikali inajulikana. Kwa mwaka ni miezi mitatu, mitatu, kwa suala nyeti la Deni la Taifa, tutaambiwa watu mnashindwa kupanga ratiba zenu kuna nini cha muhimu zaidi ya Deni la Taifa la nchi hii? *(Makofi)*

Mimi nadhani tusikae tunabishana hapa *for nothing*. Kubalini hiki kitu, hawa watu ambao wamepewa hizi dhamana watekeleze wajibu wao. Rais amesema kwa awamu yake ya Tano hakuna biashara ya kwenda nje. Ndiyo maana yeye mwaka umeisha ndiyo amekwenda zake Ethiopia hatutaki kuamini kwamba anakimbia nje kwa sababu ya ngeli, hapana. Tunataka kuamini kwamba anataka tubaki ndani tujenge nchi yetu. Sasa kama Rais hasafiri, hawa Makatibu Wakuu wanaenda wapi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee kama hujakubaliana na Mheshimiwa Waziri naomba utoe hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe hoja ili Wabunge wenzangu waweze ku-*debate,* waone hizi hoja nyepesi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu sheria iko wazi na imeeleza haki na wajibu wa kila mmoja, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa John Heche.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mbogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu na Mheshimiwa Chenge. Tunaanza na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kutia tu sherehe, lakini mtoa hoja alivyoelezea kama kuna mtu anafikiri vizuri na ana nia njema kwa Taifa hili maelezo yake yanajitosheleza. Kama tuna nia kweli ya kulisaidia Taifa, Taifa ambalo limekwama, Deni la Taifa kubwa, sheria imetungwa, imewapa mamlaka Makatibu Wakuu kwa kuangalia unyeti wa suala lenyewe. Leo tunataka tuidhinishe Katibu Mkuu akitoka ampeleke Afisa yoyote anayeona anafaa aende akajadili suala hili, mimi nadhani *we are not fair* na hatulitendei haki Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sina mengi ya kueleza kwa sababu mtoa hoja ameeleza vizuri na watapinga wenzetu wa upande wa pili kwa sababu wamezoea tu kwamba kila kinachoongelewa huku wanakiona ni kibaya, lakini kwa maelezo na hoja aliyotoa Mheshimiwa Mdee na ndiyo maana unaona CCM wote walikaa kule, wakasimama wenyewe waliotoa hoja, walihisi kwamba maneno ya Mheshimiwa Mdee yanakidhi haja, lakini watapinga kwa sababu wameamua kuja kupinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mdee, ni hoja ambayo inazingatia maslahi ya Taifa, endeleeni na mila yenu. Nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi naungana na muswada wenyewe ulivyoandikwa na sikubaliani na *amendment* kwa sababu ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana wote kwamba Deni la Taifa ni suala nyeti sana, kunapokuwa na mahitaji ya kuwa na mkutano, ule mkutano haupaswi kutokufanyika kwa sababu Gavana hayupo au *Attorney General* hayupo au hao wengine ambao wako kwenye sheria hawapo. Kwa hiyo, suala la kuwa na mtu Mwandamizi anayejua *subject* hiyo ni muhimu sana. Wale wengine ambao wanakuwepo hawawezi kumwakilisha ambaye hayupo, Kwa

mfano, tuna Gavana mmoja wa Benki nchi hii anayejua masuala ya uchumi na ya fedha na sera za kifedha, huwezi ukamfanya mwingine ambaye hana *knowledge* ile akamwakilisha. *(Makofi/Kicheko)*

Kwanza, nawashukuru sana kwa makofi lakini mnapiga makofi bila kunielewa, hamkunielewa kwa sababu hamna utaalamu huo. *Attorney General* hawezi kumwakilisha Gavana wa Benki Kuu hajui mambo ya sera za fedha kwa hivyo lazima aende *Deputy Governor* ili amuwakilishe kufuatana na *knowledge* aliyonayo. Kama kweli tunaona unyeti wa Deni la Taifa, sioni namna ambavyo utataka *Attorney General* amwakilishe sasa kule ndani Gavana ambaye anatakiwa na Benki ya Dunia kule Washington.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu naomba tusibishane tena namshukuru Mheshimiwa Halima kasema humu ndani tunabishana kwa sababu tunataka kubishana, mimi sibishani kwa sababu nataka kubishana, nabisha suala lake la *amendment* kwa sababu najua unyeti wa Deni la Taifa.

Kwa hiyo, ndugu zangu ninaombeni sana muone umuhimu wa mkutano unapofika usiachwe kwa sababu wale wanaotakiwa kule ndani hawapo kwa kukubali *amendement* hii na mimi naomba wengi wakubaliane na Muswada huu kwamba Afisa Mwandamizi mwenye utaalamu huo amwakilishe yule ambaye yuko kwenye Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mary, umeeleweka, tunaendelea na Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie alichokisema Mheshimiwa Bobali. Kuna wakati tunabishana humu lakini ukitafuta *logic* ya mabishano hayo haipo. Kwa miezi sita Deni la Taifa limepanda kwa asilimia tatu na sasa Deni la Taifa ni zaidi ya trilioni 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua nimemsikiliza hata Mama pale anajaribu kutetea mpaka yeye mwenyewe anaona aibu, kwa sababu...

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Usinisemee mimi. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Wewe mbona umemsema Halima *(Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hakuna sehemu yoyote kwenye sheria hii ambayo imesema lazima Gavana awepo. Kinachozungumzwa ni *quorum* ya watu watano dhidi ya watu kumi. Sasa huyu Mama alikuwa Waziri na Mheshimiwa Magufuli amemkataa kipindi hiki ndiyo maana anatafuta nafasi hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo siyo kauli nzuri tafadhali naomba uifute.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa siyo Mama.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni nini hapa? Hoja ya Halima inaeleweka *unless* mseme kuna watu mnataka wawe wanachungulia vitu ambavyo hawajui halafu tukitafuta watu tuwawajibishe kwenye kusababisha mambo haya tunakosa kwa sababu leo ameingia yule, kesho ataingia huyu, kesho kutwa yule. Kimsingi ni lazima watu wawepo ambao watakuwa *accountable* tutakapokuwa na matatizo ya kuonesha kwamba kuna kitu kilifanyika ndivyo sivyo, kwa sababau nchi hii ni ya kwetu sote. Deni hili linapopanda hamlipi ninyi wenyewe tu tunalipa mpaka sisi. Kwa hiyo, kuna wakati mwingine ni lazima msikilize na hivi vitu ni rahisi tu kuelewa. Jambo kama hili la Mheshimiwa Halima ni jambo ambalo hata ukimwambia mtoto mdogo na akaangalia *logic* ya kitu kinachozungumzwa kwamba watu kumi ipo siku ambayo kikao ambacho kipo kwenye ratiba watakosekana watu watano inawezekanaje? Vikao hivi vinawekwa kwenye ratiba vinajulikana mwezi wa kwanza, mwezi wa pili au mwezi wa tatu tutakuwa na kikao, kwa hiyo watu watano ambao wanapaswa kuwepo ili *quorum* itimie kikao kiweze kuendelea lazima wawepo. Haijasema Mwanasheria Mkuu au Gavana ni lazima wawepo kati ya wale watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Halima na namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali achukue hoja ya Halima ina-*hold water* kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHANGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kupinga tu hoja ya Mheshimiwa Halima kwa sababu ukisoma mapendekezo ya muswada, mapendekezo ya Serikali yako wazi kabisa na wametumia neno ambalo ni *enabling* (aweza) Mamlaka husika yaani anayepaswa kuhudhuria vikao hivyo aweza katika hali hiyo akamteua siyo katika hali yote ile lazima ateue, hapana. Tukielewana hivyo *that the starting entry point*.

Sasa ukichukua ofisi ambayo mimi nimekaa muda mrefu kuna nafasi ya *Deputy Attorney General* ambayo iko Kikatiba na huwezi ukasema Naibu Mwanasheria Mkuu ni mtumishi mdogo na kuna *Deputy Governor* wa Benki Kuu na siyo mmoja. Unaye *Deputy Permanent Secretary* Wizara ya Fedha, hawa ndiyo *critical* na Zanzibar hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza tatizo liko wapi? Kama Waheshimiwa Wabunge nisingependa maneno yaliyotumika kwamba tunapoteza muda kwa kubishana bishana. Tunatunga sheria hiki ni kipindi kizuri sana tuelezane ukweli kwamba mapendekezo ya Mheshimiwa Halima hayatusaidii. Tutakuwa Kamati ya ajabu sana kama tutasema tuyafute kama anavyopendekeza maneno haya, ukiyafuta iwe nini sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chenge umeeleweka. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti alichosema Mheshimiwa Chenge nakubaliana nacho, muswada huu ubaki jinsi ulivyo kwa sababu kwanza mtu halazimiki. Matumizi ya neno "*he may*" sasa asipoenda maana watakuwa wanakwamisha utaratibu tu wa kawaida, kwa hiyo kila mmoja lazima awepo pale kulinda maslahi ya sehemu anayowakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kwamba Muswada huu jinsi ulivyo Wabunge waukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashangaa Mtemi Chenge anavyosema mabadiliko ya kwangu hayafai, wakati haya mabadiliko yaliyoletwa na Serikali kabla hayajaletwa hiki ninachokisema ndicho kilikuwa kinafanyika. Ukisema hayafai maana yake wakati wewe ulipokuwa *AG* mlikuwa mnafanya nini wakati sheria hii ndiyo mlikuwa mnaitumia kufanya hayo mambo? Kama Mzee wamekushtukiza kujibu hoja nashauri usidandie hoja kwa sababu nakuheshimu sana. *(Makofi)*

Jambo la pili, ninamshukuru sana Mama Nagu alisema Gavana hawezi kuwakilishwa na mtu mwingine, hayo ndiyo yalikuwa ni maneno yako hata *Hansard* itasema. Hebu niache nimalize mbona unapaparika? Ndiyo ulisema wewe. Gavana hawezi…kaa chini bwana. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Unaingilia kazi yangu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Unaingilia kazi ya Mwenyekiti tulia umeambiwa. Ni hivi Mwenyekiti….Mama Nagu kaa mimi nakuheshimu. Ni hivi, Mheshimiwa Nagu hata *Hansard*…

**MBUNGE FULANI:** Bangi hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee nilikuwa nakuambia wewe unaingilia kazi yangu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ahaa basi, tunaangaliana.

**MBUNGE FULANI:** Chukua taarifa hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Mama Nagu hajatoa taarifa.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nagu naomba uendelee tafadhali.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa naeleza ni kwamba Wajumbe wale wameingia kwenye Bodi kutokana na utaalamu wao na kwa hiyo utaalamu wa sheria hauwezi kusimamia utaalamu wa fedha, hivyo sijasema kwamba *Attorney General* hawezi kumwakilisha Gavana ila nasema wameingia *by virtue of their expertise*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nagu umeeleweka, tuendelee Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema alisema kwa maneno yake na *Hansard* inamnukuu kabla hajabonyezwa pale kwamba Gavana hawezi kuwakilishwa na mtu mwingine na ndiyo maana hii sheria ilitambua, ikamtambua *AG,* ikamtambua Gavana na ikawatambua na *Permanent Secretaries* wa Wizara mbalimbali, hiyo mosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hakuna popote kwenye sheria hii paliposema kikao hakiwezi kuendelea asipokuwepo Gavana, asipokuwepo

Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ingekuwa ndiyo hivyo, wangesema *quorum* ni watu kumi ili wale watu wote wawepo. Unaposema *quorum* ni watu watano hata kama mkiongeza mbingu na dunia, hata kama mkisema *Principal Officers* wawepo wanaweza wakawepo watano kwa sababu *requirement* ya kisheria ni *quorum* ya watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli unajiweka tu huru yaani sitaki kutumia *energy* nyingi kwa watu ambao tayari wameshajilipua, yaani kuamua kile kinachotaka kuletwa na Serikali wakipitishe, lakini ukweli unabaki pale pale. Narudia kwenye Bunge hili, tunapitisha Bodi mbalimbali, tunapitisha Mabaraza ya Ushauri mbalimbali, tunapitisha Wajumbe wa Kamati mbalimbali, sijawahi kuona kwenye sheria yoyote Wajumbe wa hizo Kamati, Wajumbe wa hizo Bodi wanapewa mamlaka ya ku-*delegate some of their powers* kwa watu wengine, hii ni mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kuna kitu mnaficha kwa sababu mnajua Deni la Taifa litakuja ku-*back fire* ili muweze kujua kutokumshika mchawi ni nani, siku hazigandi tutafika, lakini mwenye kusikia amesikia, mwenye kuona ameona. Huo ndiyo mwisho wa hoja yangu, Bunge liamue, waamue watakavyojiona akili zao zinawatuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.

**MWENYEKITI:** Sasa naihoji Kamati.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waliokataa wameshinda na hoja imekataliwa. Katibu tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa Kamati ya Bunge*
*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizoyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizoyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizoyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Sehemu ya Sita ya Muswada imefutwa hivyo Ibara zinazofuata zimebadilika namba)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 31

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, kifungu sasa hivi kimekuwa *redundant*.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sware.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 32

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki marekebisho ya Serikali yaliyo-*accomodate* hoja za Kamati, kime-*accomodate* pia ile *spirit* ya hoja yangu, kwa hiyo, sitaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Halima Mdee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 33

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hiki kinatakiwa kabisa kiwe *deleted* lakini *suggestion* zangu zimeandikwa vinginevyo, kwa hiyo kimekuwa *redundant*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sware.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 34
Ibara ya 35

*(Ibara zilizoyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu hiki pia kiko *redundant*.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja naomba uje utoe taarifa.

**TAARIFA**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 4) Act, 2016)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2016, *(The*

*Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 4) Act, 2016,* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imekubaliwa nawashukuru sana. Katibu hatua inayofuata.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend certain Written Laws)*.

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, natangaza rasmi kwamba Muswada huo wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 4 umepitishwa na Bunge hili. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa jitihada ilizochukua katika kufanya marekebisho mpaka kufikia kupitishwa Bungeni na pia niwashukuru Wabunge wote kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya, Mungu awabariki sana, pia Mwenyezi Mungu aibariki Serikali yetu pale ambapo Muswada huu utakwenda kupitishwa au kupata kibali cha Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Katiba ili tuweze kuitekeleza kwa namna inavyotakiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tumekamilisha shughuli zetu za siku ya leo, ninawatakia kila la kheri na naliahirisha Bunge hadi kesho asubuhi saa tatu. *(Makofi)*

*(Saa 1.07 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 2 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*